

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 19 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA NA MUUNGANO:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2010/2011 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Tume ya Mipango (Fungu 66), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67) na Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na Mpango wa Kazi kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Fedha za Ofisi za Rais: Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Mipango, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Makamu wake Mheshimiwa Ramadhan Athman Maneno, Mbunge wa Chalinze, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2010/2011, hatua ambayo imetuwzesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu tangu alipochaguliwa kushika wadhifa huo mwaka 2005. Katika kipindi cha uongozi wake ametekeleza yale aliyoahidi kwa wananchi kwa wakati, wakati wa uchaguzi na mengi yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa kwa mafanikio makubwa. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini na wadau wa maendeleo kuona haja ya kuendelea kutuunga mkono. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima katika uongozi wake ili aendelee kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais kwa kumsaidia na kumshauri Rais kwa hekima katika

utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo. Nampongeza pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa kuendelea kuongoza vyema shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, hotuba aliyoitoa mbele ya Bunge lako tukufu wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2010/2011 ni kielelezo cha upevu wake katika uongozi na imesaidia kuonyesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2010/2011. Nampongeza pia Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Kilosa na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake ambayo imeainisha misingi na mwelekeo wa bajeti na uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti, na wewe kwa busara zenu katika kuliongoza Bunge letu Tukufu ambalo kwa kipindi cha miaka mitano limetoa maamuzi mazito yaliyohibitisha uwezo wake katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini.

Mheshimiwa Spikai, kwa namna ya pekee naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais akiwemo Mheshimiwa Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu (CUF) na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (CCM). Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa (CCM), Mbunge wa Biharamulo Magharibi kwa kuchaguliwa kwake. Naamini kuwa mchango wao umeongeza ufanisi wa Bunge lako katika kuwatumikia wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba (MB), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora kwa ushirikiano wake mkubwa katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii. Aidha, namshukuru Bwana Phillemon Lutangilo Luhanjo, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Michael Peter Mwanda, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu; Bwana George Daniel Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; DR. Philip Isidor Mpango, Katibu Mtendaji Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango; Bwana Eric Francis Shitindi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Makamishna na Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais; Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Taasisi zake ambao wamefanya kazi kubwa katika kuwezesha hotuba hii kukamilika.

Napenda nitumie fursa hii pia kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wenzetu wa Wizara, Mikoa na Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma kwa ushirikiano na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii. Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini ambao walinichagua na pia kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo mbalimbali ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio mbalimbali tuliopata. Hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yafuatayo: Australia, China, India, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Malaysia, Misri, Norway, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji,

Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Marekani, Ireland, Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japani (Japanese Social Development Fund), CIDA (Canada), DANIDA, DFID, JICA, NORAD, OPEC, SIDA (Sweden), UNDP, UNIDO, UNFPA na USAID. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa familia na jamaa za Waheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa aliyefariki dunia tarehe 31 Desemba 2009 na Sigfrid Seleman Ng'itu (Mb.) wa Jimbo la Ruangwa aliyefariki tarehe 2 Novemba, 2009. Pia natoa pole kwa wote walioondokewa na wenzi wao, ndugu, jamaa na marafiki katika kipindi hiki. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi na awajalie ndugu wa marehemu moyo wa subira.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo manne ambayo ni: Mapitio ya utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005, utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha 2009/2010, Mpango wa Kazi wa Mwaka 2010/2011 na maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Ikulu, Utawala Bora. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaelekeza kuwa:-

Utawala Bora uimarishwe ili kuhakikisha kwamba nchi inaendeshwa kwa misingi ya Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa za Kidemokrasia nchini kote kuanzia ngazi ya Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata, Wilaya, Mikoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Spika kama nilivyoeleza katika hotuba ya bajeti ya mwaka uliokwisha, utekelezaji wa mpango wa Awamu ya Pili wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP II: 2006-2011) uliozinduliwa Desemba, 2006, uliendelea vizuri katika kipindi hiki. Mpango huo wa utekelezaji ulilenga katika kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kurekebisha kasoro zilizojitokeza wakati wa kutekeleza mpango wa Awamu ya Kwanza ya Mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Awamu ya Pili ya Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP II) unakaribia kufikia mwisho, Serikali imeagiza Taasisi zote katika Utumishi wa Umma kuanza kupitia shughuli na mipango waliojiwekea kwa ajili ya kuziba mianya ya rushwa katika maeneo yao ya kazi ili kuboresha na kuweka mikakati mipya na madhubuti zaidi ya kuendeleza mapambano hayo ya kudumu katika kipindi cha miaka mingine mitano.

Kuendelea kutoa mafunzo juu ya utawala bora kwa watendaji katika ngazi zote na kuhakikisha kwamba matokeo ya mafunzo haya yanaiweka Serikali katika utendaji ulio wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kuhusu utawala bora kwa Viongozi na Watendaji katika ngazi mbalimbali yaliendelea kutolewa katika kipindi hiki. Mafunzo hayo yamejikita zaidi katika kuhimiza uadilifu, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi na utekelezaji wa shughuli za umma. Hadi mwezi Machi, 2010, jumla ya wajumbe 376 wa Kamati za Uadilifu katika Taasisi za Umma walipatiwa mafunzo ya utawala bora na namna ya kutekeleza majukumu yao. Mafunzo ya utawala bora pia yameendelea kutolewa kwa Watendaji Wilayani na katika Vijiji kupitia mfumo wa ugatuuji madaraka unaosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ambazo zimechukuliwa katika kuimarisha Utawala Bora ni pamoja na kukamilishwa kwa Tathmini ya Hali ya Rushwa na Utawala Bora nchini. Hivi sasa Serikali inaendelea kupitia Ripoti ya Tathmini hiyo na kujiandaa kuweka mikakati madhubuti zaidi ya kudhibiti rushwa na kuimarisha utawala bora. Mwezi Februari mwaka huu, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na.6 ya mwaka 2010 ambayo inalenga kudhibiti rushwa katika chaguzi zetu. Nina imani sheria hii itasaidia sana kuzuia vitendo vya rushwa na kufanya chaguzi zetu kuwa za haki na huru zaidi.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kuimarisha Utawala Bora na kujenga Utamaduni wa uwajibikaji na kuipiga vita rushwa na maovu mengine katika jamii ifikapo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa na kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya 2005, TAKUKURU imetekeleza yafuatayo:-

Imetoa mafunzo ya kuimarisha uadilifu kwa kamati za uadilifu zilizoanzishwa katika Wizara 25, Idara Zinazojitegemea 35, Wakala wa Serikali 68, Taasisi za Umma 84, vyuo vya elimu ya juu tisa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 117 kwa lengo la kujenga misingi ya utawala bora, uadilifu na uwajibikaji wa watumishi wa umma na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mafunzo ya uadilifu yalitolewa pia kwa Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mtandao wa Wabunge wanaopambana na Rushwa Afrika (APNAC), Wajumbe 238 toka Sekta Binafsi, wajumbe 418 toka Asasi za Kiraia na wajumbe 40 toka vyombo vya habari.

Aidha, TAKUKURU kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilitoa mafunzo ya uadilifu kwa wajumbe wa bodi za zabuni kutoka Wizara nne.

Kongamano la Kitaifa lililoshirikisha wadau 200 wa mapambano dhidi ya rushwa kutoka sekta zote nchini lilifanyika, hivyo wadau kupata nafasi ya kutoa taarifa za utekelezaji na kujadili mbinu bora za namna ya kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa katika maeneo yao.

Kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kutungwa kwa Sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza kwenye mapambano dhidi ya rushwa, ushirikiano kati ya TAKUKURU, Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umeanzishwa na tayari makubaliano rasmi na Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma yamefanyika. Lengo la ushirikiano huo ni kuongeza kasi ya kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa katika eneo la ununuzi na maeneo mengine kadri yanavyoainishwa na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Aidha, Serikali ilitunga Sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007 ambayo imeainisha makosa 24 badala ya makosa manne yaliyokuwa kwenye Sheria ya zamani ya Kuzuia Rushwa Na.16 ya mwaka 1971.

Sheria hii mpya imepanua wigo wa kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi mwaka 2010 kesi 755 zilifikishwa mahakamani na kufanya jumla ya kesi 813 kuendeshwa mahakamani zikiwemo kesi za miaka ya nyuma. Kati ya kesi hizo Serikali ilishinda kesi 155 na washtakiwa kuhukumiwa vifungo mbalimbali.

Aidha, jumla ya Shilingi 28,827,667,374 ziliokolewa katika kipindi hicho.

Mheshmiwa Mwenyekiti, kuendeleza mafunzo na elimu kwa wananchi kuhusu rushwa. Aidha, vikundi vya kijamii vitahamasishwa kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa. Kupitia ushirikiano na wadau mbalimbali kama vile Asasi za Kiraia, Vyama vya Hiari, Wasanii na Vyombo vya Habari, elimu na mafunzo yalitolewa kwa wananchi kwa njia mbalimbali kama ifuatavyo: Mijadala ya wazi, makongamano, midahalo na maonesho 3,126, semina 6,022 na Klabu za wapinga rushwa 3,787 zilianzishwa katika shule za sekondari na katika vyuo sita kwa lengo la kujenga uadilifu na kuhamasisha jamii kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (*MKURABITA*). Serikali ibuni utaratibu wa kuzipa uhai wa kisheria ardhi na nyumba ambazo hadi sasa hazitambuliwi kisheria. Kwa utaratibu huu wenye ardhi na nyumba wanaweza kupata mikopo kwa kuweka ardhi na nyumba hizo dhamana. Lengo lake ni kuwafanya wananchi waliokuwa hawakopesheki sasa wakopesheke na hivyo kuingia katika mchakato wa uchumi hai.

Mheshmiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, *MKURABITA* imeunda Kikosi Kazi kwa ajili ya kupitia maboresho yanayohusu Sheria za Ardhi. Kikosi kazi hiki kimeshakamilisha kazi na Taarifa yake imewasilishwa katika Wizara hiyo kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kurekebisha sera na hatimaye sheria na kanuni mbalimbali zinazohusu ardhi. Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko *MKURABITA* imeunda Kikosi Kazi cha kupitia maboresho yanayohusu Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za Biashara. Kazi hii imekamilika na Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko inaendelea na taratibu za kurekebisha Sera, Sheria na Taratibu husika. Aidha, urasimishaji wa ardhi na biashara umeanza na unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund - TASAF*). Katika kipindi cha mwaka 2005–2010 *TASAF* kwa kushirikiana na wananchi, imewezesha utekelezaji wa miradi 9,321 iliyoibuliwa na makundi ya jamii yenyewe ambako kuna upungufu wa huduma za jamii kama vile afya, elimu, maji n.k. kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa zote na Visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, kaya zenye uhaba wa chakula, makundi maalum kama yatima, wajane, wagane, watu wenye ulemavu na wazee yalijumuishwa katika miradi hii. Miradi 215 inayotoa ajira za muda mfupi na uzalishaji mali inayolenga kuongeza kipato ilipatiwa fedha ili walengwa wapate fedha za kuwasaidia kununua chakula kukabiliana na tatizo la njaa.

Mheshmiwa Mwenyekiti, katika kipindi husika, kazi zifuatazo zimetetelezwa:-

Miradi 5,865 imekamilika na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa walengwa kote nchini.

Vikundi 1,778 vyenye wanachama 22,712 vya Kuweka Akiba na Kuwekeza vimeundwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 44 za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba.

Vikundi 1,000 vya Kuweka Akiba na Kuwekeza vimepewa mafunzo na vifaa vya kutunzia akiba zikiwemo kasiki za kutunzia fedha na vitabu vya kumbukumbu.

Mheshmiwa Mwenyekiti, katika kuwapatia walengwa elimu ya kusimamia shughuli zao za maendeleo, TASAF imetoa mafunzo kwa wakufunzi 3,492 wa ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafunzo haya yalitolewa kwa wakufunzi wa kamati za usimamizi wa miradi ya jamii. Aidha, wajumbe 267,953 wa Kamati za usimamizi wa miradi wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa miradi, uendeshaji na matengenezo ya miradi iliyokamilika na ambayo inatoa huduma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti Ya Utumishi Wa Umma. Kuongeza kasi ya kukua kwa teknolojia ya Abarrí na Mawasiliano katika kujenga uwezo wa kuratibu na kuimarisha mfumo huo. Katika kuongeza kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imefanya yafuatayo:-

Mkakati wa utekelezaji wa Serikali Mtandao umeandaliwa na kuanza kutekelezwa. Uanzishwaji wa Wakala wa Serikali Mtandao kama chombo cha kusimamia matumizi ya *TEKNOHAMA* Serikalini upo katika hatua za mwisho. Mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara umeimarishwa katika Wizara na Idara Zinazojitegemea. Tovuti Kuu ya Serikali inakamilishwa kwa kufanyiwa majaribio kabla ya kuanza kutumika. Taasisi saba za Serikali zimeunganishwa katika Mtandao wa mawasiliano ya Serikali na zinafanyiwa majaribio.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kuona kwamba ajira mpya zaidi ya milioni moja zinapatikana. Ili kutekeleza agizo hilo, Serikali iliajiri watumishi 128,174. Aidha, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*Tanzania Employment Services Agency - TaESA*) imeanzishwa ili kuunganisha waombaji kazi na waajiri katika soko la ajira; na Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeanzishwa kwa lengo la kurahisisha mchakato wa upatikanaji wa watumishi katika taasisi za umma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kuweka na kusimamia utaratibu mzuri zaidi wa kupokea kero za wananchi na kuhakikisha kuwa zinapatiwa ufumbuzi wa haraka. Maelekezo haya yalitekelezwa kwa kufanya yafuatayo: Mfumo na mwongozo wa kushughulikia malalamiko umeanzishwa na kufanyiwa majaribio katika Taasisi saba za umma, Vitengo vya Habari Elimu na Mawasiliano vimeimarishwa kwa lengo la kuwaelimisha wananchi kuhusu viwango vya huduma zitolewazo na Serikali; na Madawati ya kupokea malalamiko katika Wizara na Idara Zinazojitegemea yameanzishwa.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kuendelea kuendesha Serikali kwa kufuata Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa kidemokrasia nchini kote kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji, mitaa, kata, Wilaya, Mikoa hadi Taifa. Katika kutekeleza maelekezo haya yafuatayo yamefanyika: Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma



ya mwaka 1999, Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002, Sheria ya Wakala wa Serikali Na.30 ya mwaka 1997 na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 1994 zimehuishwa ili kukidhi matakwa ya Utawala Bora. Aidha, Sera ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imeandaliwa na kupitishwa.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kuendelea kutoa mafunzo juu ya utawala bora kwa Watendaji katika ngazi zote na kuhakikisha kwamba matokeo ya mafunzo haya yanaiweka Serikali kwenye utendaji ulio wazi. Yafuatayo yamefanyika: Viongozi na maafisa waandamizi katika Utumishi wa Umma 402 wamepata mafunzo maalum ya Uongozi na Maadili, Usimamizi wa Maadili na Utawala Bora ili kuwawezesha kusimamia na kuimarisha maadili na uwajibikaji. Aidha, Mafunzo ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ambayo yalishirikisha viongozi wa Serikali, vyama vya siasa, dini, watumishi wa Serikali na Asasi zisizo za kiserikali yalitolewa katika Wilaya zote za mikoa ya Tabora, Shinyanga, Rukwa, Ruvuma, Mtwara, Singida, Kigoma, Lindi, Manyara, Iringa na Pwani.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa pamoja na Kuongeza nafasi na fursa katika ngazi za uteuzi kwenye utawala, uongozi na menejimenti ndani ya Serikali na Taasisi zake. Katika kutekeleza maelekezo haya yafuatayo yamefanyika:-

Watumishi wanawake wenye sifa wameteuliwa kushika nyadhifa za juu katika Utumishi wa Umma. kama ifuatavyo: Majaji wanawake kutoka 13 hadi 34; Mawaziri kutoka wanne hadi saba; Makatibu Wakuu kutoka saba hadi tisa; Naibu Makatibu Wakuu kutoka mmoja hadi watano; Makatibu Tawala wa Mikoa kutoka wanne hadi 10; Wakuu wa Wilaya kutoka 20 hadi 25; Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka 14 hadi 35; na Wakurugenzi katika Wizara na Idara Zinazojitegemea kutoka 29 hadi 133. Aidha, jumla ya watumishi wanawake 315 wamepatiwa ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili katika Vyuo Vikuu na mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwajengea uwezo katika utendaji kazi na kupata sifa za kuwawezesha kuteuliwa katika nyadhifa mbalimbali za maamuzi.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kupanua na kuimarisha fursa za ajira kwa walemavu. Katika kutekeleza maelekezo haya yafuatayo yamefanyika: Mwongozo wa kuwahudumia Watumishi wa Umma wenye ulemavu umeandaliwa na kusambazwa kwa waajiri mbalimbali wa Taasisi za Serikali; taarifa za watumishi wenye ulemavu katika Utumishi wa Umma na wahitimu watarajiwa zimekusanywa na kuhifadhiwa kwenye kanzidata kwa lengo la kuandaa mkakati wa kuwasaidia kupata ajira. Aidha, Watumishi wenye ulemavu 11 wamepata ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili katika Vyuo Vikuu vilivyopo nchini kuanzia mwaka 2008 – 2009 ili kuwawezesha kushindana katika soko la ajira.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi yote yanayofanywa na Serikali ambayo yanawagusa. Katika kutekeleza maelekezo haya yafuatayo yamefanyika: Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma sura ya 404 imeendelea kutekelezwa na Baraza la Majadiliano ya pamoja katika Utumishi

wa Umma limeundwa na kuzinduliwa mwaka 2006 kwa lengo la kuimarisha ustawi wa wafanyakazi mahali pa kazi;

Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja ya Kisekta yamezinduliwa mwaka 2008 kwa lengo la kujadili na kuishauri Serikali kuhusu masharti ya kazi na maslahi ya watumishi katika Sekta husika; jumla ya mabaraza ya wafanyakazi 130 yameundwa katika taasisi mbalimbali za umma (Wizara 25, Idara Zinazojitegemea 10, Wakala wa Serikali 18, Ofisi za Wakuu wa Mikoa 20, Mamlaka za Serikali za Mitaa 36 na Taasisi nyingine za Umma 21). Kutokana na ushauri uliotolewa na Mabaraza hayo kwa Serikali kuhusu kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma, Serikali imeweza kupunguza viwango vya kodi ya mapato inayokatwa katika mishahara ya Watumishi wa Umma kutoka asilimia 18 hadi 14. Sanjari na hatua hizi, mishahara ya Watumishi wa Umma imeendelea kuboreshwa ambapo kima cha chini cha mishahara kwa mwezi kimeongezeka kutoka Sh.65,000 mwaka 2005/2006 hadi Sh.104,000 mwaka 2009/2010. Aidha, Serikali imeendelea kulipa malimbikizo na mapunjo ya mishahara kwa Watumishi wa Umma yenye thamani ya Sh.227,276,573,725.48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kusimamia Sheria na taratibu zinazohusu ajira za wageni. Katika kutekeleza maelekezo haya, Kamati za Ushauri za Ajira za Wageni katika Wizara, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Idara Zinazojitegemea zimeundwa. Kamati hizi zimeelekezwa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria na taratibu za ajira za wageni zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Kuendelea kutoa mafunzo juu ya Utawala Bora kwa watendaji katika ngazi zote na kuhakikisha kwamba matokeo ya mafunzo hayo yanaiweka Serikali kwenye utendaji ulio wazi. Iliendelea kutoa elimu kwa umma ikiwa ni moja ya majukumu yake ili kuimarisha Utawala Bora kwa kuhakikisha kwamba nchi inaendeshwa kwa misingi ya Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa kidemokrasia. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliendesha Semina kwa Waheshimiwa Madiwani 529 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18.

Aidha, Sekretarieti imeshiriki kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Nane Nane na kusambaza machapisho mbalimbali yenye lengo la kuhamasisha na kukuza maadili kwa Viongozi wa Umma na wananchi kwa ujumla. Vile vile vipindi 10 vya Televisheni vyenye ujumbe mahsusi wa Maadili ya Viongozi wa Umma vimerushwa kupitia televisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatilia malalamiko ya baadhi ya wananchi kwamba kuna watu wengi wanaolimbikiza mali nyingi kama majumba, mashamba n.k. kuliko uwezo wa mapato halali wanayopata. Jumla ya Fomu 20,861 za Tamko la Mali na Madeni zilirejeshwa kutoka kwa Viongozi wa Umma.

Idadi hiyo ni sawa na asilimia 63.78 ya Fomu 32,704 zilizotarajiwa kuwasilishwa na Viongozi wahusika. Fomu 11,843 za Tamko la Mali na Madeni sawa na asilimia 36.22 hazikurejeshwa. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeendelea

kuwafuatilia Viongozi ambao wamekiuka Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na.13 ya Mwaka 2005 ili wachukuliwe hatua.

Mheshmiwa Mwenyekiti, jumla ya malalamiko 757 dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchunguzwa, malalamiko 197 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na malalamiko 560 hayakuhusiana na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Malalamiko yanayohusu ukiukaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yako katika hatua mbalimbali za uchunguzi na malalamiko mengine yalipelekwa kwenye Taasisi husika.

Mheshmiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine ambayo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza ni kuhakiki mali na madeni ya Viongozi wa Umma 1,678 wa kada mbalimbali wakiwemo Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Naibu Katibu Wakuu, Majaji, Wabunge, Madiwani, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wahasibu Wakuu, Wakaguzi wa Ndani, Wakuu wa Mashirika, Wenyeviti wa Bodi, Maafisa wa Polisi, Magereza na Jeshi la Ulinzi la Wananchi. Lengo la kufanya uhakiki huu ni kuthibitisha ukweli wa Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma. Uhakiki huo ulibaini dosari kadhaa katika Tamko la baadhi ya Viongozi wa Umma na hatua husika zimechukuliwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Sekretarieti imeandaa rasimu ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398 Toleo la 2002. Marekebisho haya yanalenga kuweka utaratibu wa kutenganisha shughuli za biashara na uongozi wa umma. Muswada wa Sheria wenye mapendekezo hayo utawasilishwa Bungeni baada ya Serikali kukamilisha uchambuzi. Sheria hii itasaidia ufuatiliaji wa maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Kuimarisha mifumo na Taasisi za uwajibikaji, uadilifu na uwazi wa viongozi wa Serikali, wasio wa Serikali na vyama vya siasa. Watumishi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma wameanza kutumia Mfumo wa Kanzidata ili kurahisisha hifadhi ya kumbukumbu na taarifa mbalimbali zikiwemo malalamiko, mali, rasilimali na madeni ya Viongozi wa Umma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi hadi sasa Sekretarieti imeidhinisha ruzuku ya jumla ya Sh.2,031,560,644 kwa Taasisi za Umma, Azise na Azaki 300 kutoka Mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mwanza, Mbeya, Iringa, Kagera, Tanga, Arusha, Dar es Salaam na Ruvuma. Ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa miradi iliyopewa ruzuku unaendelea ili kuhakikisha kwamba fedha iliyotolewa inatumika ipasavyo. Aidha, kuanzia awamu ya tatu Ruzuku itakayotolewa italenga kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Tume Ya Mipango. Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa na Taifa linalojitegemea; kwa kuleta mapinduzi ya kilimo na viwanda. Tume ya Mipango imeendelea kujiimarisha katika kuratibu utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume imekamilisha utafiti kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, matokeo ya mapitio hayo yataiwezesha Tume kuandaa mipango ya muda mrefu na muda wa kati ya maendeleo ambayo itatekelezwa kwa kurejea utaratibu wa kuwa na mipango ya miaka mitano-mitano kuanzia mwezi Julai, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Tume Ya Utumishi Wa Umma. Kuendelea kuendesha Serikali kwa kufuata Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa kidemokrasia nchini kote kuanzia ngazi ya Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata, Wilaya, Mikoa hadi Taifa. Katika kutekeleza maelekezo haya, Tume ya Utumishi wa Umma imefanya yafuatayo: Taasisi 161 za umma zilifanyiwa ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ajira na Nidhamu. Taasisi 27 ambazo hazikufanya vizuri katika kaguzi za awali zilifanyiwa ukaguzi wa marejeo. Taasisi 25 zilifanyiwa ukaguzi maalum kutokana na malalamiko ya watumishi na taarifa za utekelezaji zinazowasilishwa Tume. Aidha, Rufaa 464 na Malalamiko 14,081 kutoka kwa Watumishi wa Umma dhidi ya Waajiri/Mamlaka za Ajira na Nidhamu yalipokelewa na kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuendelea kutoa mafunzo juu ya Utawala Bora kwa watendaji katika ngazi zote na kuhakikisha kwamba matokeo ya mafunzo hayo yanaiweka Serikali kwenye utendaji ulio wazi. Katika kutekeleza maelekezo haya, yafuatayo yametekelezwa: Vipindi vya radio 126 vimerushwa hewani, makala 165 zimetolewa kwenye magazeti, vipeperushi na majarida; fulana na kofia zenye ujumbe kuhusu utawala bora zimetolewa; vikao vya kazi 33 vya wadau vimefanyika. Miongozo na maelekezo kuhusu masuala ya kiutumishi iliandaliwa na kusambazwa kwa Mamlaka za Ajira. Miongozo na maelekezo haya ni pamoja na Vitabu vya rejea nakala 3,274, Miongozo wa Ajira nakala 3,894, Miongozo wa Nidhamu na Rufaa nakala 3,894 Miongozo wa Kuwasilisha Taarifa Tume nakala 708 na Maelekezo Mahsusni kwa Mamlaka za Nidhamu na Kamati za Uchunguzi nakala 2,195. Aidha, ziara za kujitangaza na kuelimisha wadau kuhusu usimamizi na uendeshaji wa rasilimaliwatu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zimefanyika katika mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio Ya Utekelezaji Wa Mpango wa 2009/2010. Ofisi Ya Rais, Ikulu. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kuongoza, kufuatilia, kuratibu uendeshaji bora wa Serikali na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Rais na Baraza la Mawaziri. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo:-

Nyaraka 39 za Baraza la Mawaziri zilijadiliwa na kutolewa uamuzi katika vikao 14 vya Baraza. Kamati ya Katiba, Sheria na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanya vikao 10 ambapo miswada ya Sheria 17 ilichambuliwa. Kamati ya Makatibu Wakuu ilijadili Nyaraka 47 katika vikao 25. Kamati hiyo pia ilifanya vikao vya kazi vinne na kujadili

mada 18 zinazohusiana na utendaji kazi Serikalini. Aidha, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanya vikao 29 na kuchambua Nyaraka 44.

Rufaa 115 za watumishi zilichambuliwa na kati ya hizo 92 zimetolewa uamuzi na Rais. Malalamiko 82 yalichambuliwa na kutolewa maelekezo na Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, mkutano wa kazi kuhusu namna ya kushughulikia malalamiko ya wananchi na Watumishi wa Umma kwa Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Utumishi wa Halmashauri toka Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma ulifanyika kama ilivyopangwa.

Mafunzo ya Utawala Bora na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa yalitolewa kwa wajumbe 324 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Wilaya katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Iringa, Ruvuma, Mwanza, Shinyanga, Singida na Tabora.

Kazi ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili (*NACSAP II*) katika vikao vya *MKUKUTA* iliendelea kufanyika kama ilivyopangwa. Ukaguzi wa utendaji na uimarishaji wa Kamati za Uadilifu mahali pa kazi katika Taasisi za Umma umefanyika katika Wizara 18 na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 35. Uchambuzi wa vigezo kwa ajili ya kuandaa viashiria vya kupima utekelezaji wa malengo ya utawala bora yaliyowekwa na Serikali, Wadau na Washirika wa Maendeleo umekamilishwa. Taasisi zote za Serikali zimeelekezwa kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa mahali pa kazi.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*TAKUKURU*). Mafanikio yaliyopatikana katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa ni kama yafuatayo:-

Upelelezi wa malalamiko 895 ulikamilika na kufikisha kesi mpya 202 mahakamani, hivyo kufanya jumla ya kesi 532 kuendeshwa mahakamani zikiwemo kesi kubwa 18. Serikali ilishinda kesi 43 na washitakiwa kuhukumiwa vifungo mbalimbali. Aidha, kiasi cha Sh.9,805,884,072 kiliokolewa katika hatua mbalimbali za uchunguzi ambacho kingeweza kuchukuliwa na wala rushwa. Mijadala ya wazi 98 na midahalo 92 kuhusu mbinu za kuzuia na kupambana na rushwa ilifanyika sehemu mbalimbali nchini.

Utafiti kuhusu Rushwa na Utawala (*National Governance and Corruption Survey*) umefanyika na matokeo yamewasilishwa Serikalini. Aidha, tafiti tatu zilifanywa na Makao Makuu katika Sekta za Ardhi, Afya na Serikali za Mitaa; Tafiti nyingine 23 zilifanywa na Ofisi za Mikoa za *TAKUKURU* katika Sekta ya Nishati na Madini, Serikali za Mitaa, Afya, Fedha, Ushirika na Masoko, Uvuvi, Maliasili na Utalii, Maji na Umwagiliaji, Kilimo na Chakula, Sekta Binafsi, Asasi Zisizo za Kiserikali (*NGOs*) na Miundombinu. Warsha tano za kujadili matokeo ya kazi za utafiti na kuweka mkakati wa kuondoa matatizo yaliyobainishwa zilifanyika kwa kuhusisha Sekta za Elimu na Michezo, Ushirika, na Miundombinu.

Kazi za udhibiti na ufuatiliaji wa vitendo vya rushwa 116 zilifanywa katika maeneo mbalimbali.

Machapisho 8,500 kuhusu taarifa za tafiti zilizofanyika na yanayohusu ushauri wa njia bora za kuzuia na kudhibiti rushwa katika Idara na Taasisi za Serikali yalitolewa.

Ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Mkoa wa Temeke na Wilaya ya Maswa umekamilika na majengo yameanza kutumika. Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkoa wa Manyara na Lindi uko katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, ukarabati wa majengo ya Ofisi za Dar es Salaam, Mwanza, Iringa, Rest House (Dodoma), Makao Makuu, Kinondoni, Kibondo na Kishapu ulifanyika.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (*MKURABITA*). Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango huu ni kama ifuatavyo: Taratibu zitakazotumika katika kufanya mabadiliko ya Sheria na Kanuni za urasimishaji ardhi Vijijini na Mijini na utoaji wa Hati Miliki utakaoweza urasimishaji kwenda kwa kasi zaidi zimekamilika. Hadi mwezi Aprili, 2010 jumla ya mashamba 21,160 yamepimwa, kati ya hayo mashamba 17,526 yameingizwa katika mtandao wa kompyuta kwa ajili ya kutayarisha hati miliki za kimila. Hati 8,109 tayari zimeandaliwa. Wilaya zilizohusika katika awamu ya kwanza ni Musoma Vijijini, Serengeti, Makete, Manyoni, Mpwapwa, Mvomero, Njombe, Nachingwea na Rufiji. Aidha, urasimishaji wa ardhi vijijini unaendelea katika wilaya nyingine 12 (Kasulu, Muleba, Kahama, Sikonge, Geita, Meru, Mwanga, Moshi Vijijini, Mbarali, Sumbawanga, Mbinga, na Masasi).

Mpango Kazi kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi katika Jiji la Mbeya na Manispaa za Arusha na Morogoro umekamilika. Aidha, Jijini Dar es Salaam, urasimishaji unaendelea katika Kata ya Hananasif Manispaa ya Kinondoni ambapo jumla ya viwanja 1,423 vimepimwa na hati miliki 500 zimeandaliwa. Manispaa ya Temeke inaendelea na mchakato wa kuchagua eneo kwa ajili ya zoezi hili.

Urasimishaji wa ardhi Mjini umefanyika katika eneo la Idundilanga katika Halmashauri ya Mji wa Njombe ambapo jumla ya Viwanja 1,003 vimepimwa na kuandaliwa ramani za mipango miji na ramani za upimaji. Hadi mwezi Aprili 2010 jumla ya maombi ya hati 207 yamewasilishwa katika Ofisi za Kanda mjini Mbeya ambapo jumla ya hati 49 zimeandaliwa na kupokelewa na Halmashauri ya Mji wa Njombe tayari kwa kukabilidhiwa kwa wamiliki. Urasimishaji wa biashara unaendelea katika kata za Gerezani na Mchikichini Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam. Vituo vya mawasiliano ya biashara vitaanzishwa katika kata hizi ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu za biashara. Aidha, Kampeni za uhamasishaji nchi nzima kuhusu Urasimishaji biashara na rasilimali umefanyika kwa kuendesha Semina kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji Tanzania Bara; kurusha Vipindi maalum vya televisheni na kutoa machapisho mbalimbali.

*MKURABITA* imeshiriki katika mashindano ya Umoja wa Mataifa juu ya Utumishi wa Umma (United Nations Public Service Innovations Award) na imetunukiwa ushindi wa Pili katika eneo la Utoaji Huduma katika Utumishi wa Umma (Improving Public Service Delivery). Sherehe za kukabidhiwa tuzo kwa ushindi huu zitafanyika huko Barcelona Hispania tarehe 23 Juni, 2010.

Kikosi Kazi kilichoundwa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kutekeleza jukumu la maandalizi ya uanzishwaji wa mifumo mipya ya biashara kimekamilisha kazi na tayari Wizara iko katika mchakato wa kukamilisha taratibu zinazohusika ili kubadilisha sheria husika.

Mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa Mwongozo wa Ulipaji Kodi na Uandikaji vitabu vya hesabu kwa wafanyabiashara wadogo uko katika hatua za mwisho.

Mipango ya awali ya ujenzi wa Kituo cha Mawasiliano Dodoma imekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2010/2011. Aidha, shughuli za urasimishaji Biashara Kata ya Gerezani Jijini Dar es salaam zitawezesha kuanzisha Kituo cha Mawasiliano katika Manispaa ya Ilala.

Shughuli za kukuza na kusimamia mahusiano ya kibiashara kati ya Benki au Vyombo vya Fedha na wamiliki rasilimali na biashara zinaendelea. Mazungumzo ya awali yamefanyika na Ofisi ya Pembejeo za Kilimo na tayari walengwa wawili kutoka Kijiji cha Nkale katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni wamepata mkopo wa Matrekta ikiwa ni pamoja na kupewa mafunzo ya namna ya kumiliki na kutumia matrekta hayo kwa faida.

Timu ya Taifa ya Urasimishaji Biashara ikihusisha Mwakilishi wa Benki ya CRDB na wadau wengine imeundwa. Hatua hii ina lengo la kuwafanya walengwa kuelewa nafasi ya Vyombo vya Fedha katika kuleta maendeleo ya biashara na umiliki wa rasilimali ulio na tija. Timu ya Kiufundi (Technical Team) baina ya *MKURABITA* na Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa imeundwa. Timu hiyo itakahakikisha vitambulisho hivyo vinakuwa na mfumo utakaowezesha kuanzishwa kwa masjala unganishi ya Kitaifa ya milki hizo katika soko.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund – TASAF*). *TASAF* imeendelea kuisaidia jamii katika kuainisha, kuchambua mahitaji, kuweka vipaumbele, kuratibu na kukusanya rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Utekelezaji wa miradi hii unalenga kupambana na umasikini kupitia dhana ya ushirikishwaji wa jamii.

Mheshmiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana kutokana na Mfuko huu ni kama ifuatavyo:-

Miradi 966 yenye thamani ya Sh.13,865,471,364 imeibuliwa na wananchi na kupatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji.

Vikundi 1,000 vya makundi maalum (Wazee, Wajane, wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, n.k.), vimewezeshwa kupata mafunzo ya ujasiriamali katika uzalishaji na kujiongezea kipato na pia vimehamasishwa kushiriki katika mpango wa kuweka akiba na kuwekeza.

Walengwa 6,547 wa Mpango wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini wamepatiwa fedha Sh.127,000,000 tangu mpango huu ulipoanza mwezi Desemba, 2009 katika Wilaya za majaribio za Kibaha, Bagamoyo na Chamwino.

Taasisi za Jamii nne katika Manispaa za Kinondoni, Morogoro, Arusha na Jiji la Mwanza zimeanzishwa. Kiasi cha Shilingi 108.5 milioni zimekusanywa na Taasisi hizo.

Katika Mpango wa Kupunguza Hewa Chafu, andiko moja (*Project Idea Note*) limekamilika na kuwasilishwa *UNDP* kwa tathmini ya kupatiwa fedha. Maandiko mengine matano yanaandaliwa kwa madhumuni ya kuyawasilisha katika Taasisi mbalimbali za fedha kwa ajili ya kuombea fedha. Aidha, maandiko haya yote yamelenga katika kutumia nishati inayotokana na taka za vyooni.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*Presidential Trust Fund for Self Reliance - PTF*) ulianzishwa kwa lengo la kupambana na umaskini kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na Mfuko huu ni kama ifuatavyo:-

Mfuko umetoa mikopo ya nyumba kwa wateja 92 yenye thamani ya Sh. 272,356,250. Kati ya wateja hao, 87 ni wanawake sawa na asilimia 94.6 na wanaume ni watano sawa na asilimia 5.4%.

Mfuko umetoa mikopo kwa Wana-SACCOS 1,529 yenye thamani ya Sh. 394,565,592. Kati ya wateja hao, 814 ni wanawake sawa na asilimia 53.2% na 715 ni wanaume sawa na asilimia 46.8%.

Mfuko umetoa mikopo ya ada za shule kwa watoto 135 yenye thamani ya Sh. 83,850,200. Kati ya mikopo hiyo 108 ni wanawake sawa na asilimia 80% na 27 ni wanaume sawa na asilimia 20%. Mikopo ya ada za shule ilitolewa kwa shule za Sekondari, Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi. Mikopo hiyo ililipwa moja kwa moja katika akaunti ya benki ya Shule au Chuo husika.



Mfuko umetoa mikopo kwa Askari wa Jeshi la Polisi 454 yenye thamani ya Sh. 236,350,000. Kati ya hao, wanawake ni 429 sawa na asilimia 94.5% na wanaume 25 sawa na asilimia 5.5%. Aidha, kwa uchambuzi zaidi Mfuko umetoa mikopo 370 kwa wake za Polisi, Polisi wa kike 59 na Polisi wanaume 25.

Mfuko umeendelea kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kujiwekea akiba. Jumla ya Sh. 669,128,552 ziliwekwa kama akiba ya lazima ili fedha ziweze kuwasaidia wananchi kama mtaji kwa shughuli za maendeleo.

Mfuko umeendelea kutoa mafunzo ya biashara kwa wateja kwa lengo la kuwajengea ujasiri katika biashara zao. Aidha, wateja 11,353 walijengewa uwezo wa biashara wakati wa mafunzo ya awali ya mikopo ya mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, OFISI YA RAIS, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

Kuimarisha Miundo na Mifumo ya Utoaji Huduma:-

Miundo ya Taasisi mbili (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi) imeidhinishwa kwa utekelezaji.

Aidha, Miundo ya Taasisi tatu (Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Mahakama) inaendelea kuhuishwa.

Rasimu tatu za Miongozo kuhusu kushirikisha Asasi za Kiraia katika kuongeza uelewa wa wananchi kudai huduma; kufanya Tathmini Binafsi kwa Taasisi za Serikali na jinsi ya kufanya upembuzi yakinifu wa kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma zisizo za msingi zimekamilika.

Rasimu ya orodha ya viwango vya kimenejimenti kwa ajili ya Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali imekamilika.

Uanzishwaji wa Wakala tatu za Serikali (Serikali Mtandao, Misitu Tanzania na Maendeleo ya Uvuvi Tanzania) upo katika hatua za mwisho.

Wizara 16 zimepatiwa mafunzo ya tathmini, ufuatiliaji na uandaaji wa taarifa za utendaji kazi.

Tovuti Kuu ya Serikali (*eGovernment Portal*) imekamilika na inafanyiwa majaribio kabla ya kuanza kutumika.

Waraka wa Utumishi Na.5 wa Mwaka 2009 kuhusu Matumizi Bora na Salama ya Vifaa na Mifumo ya *TEKNOHAMA* Serikalini na Waraka wa Utumishi Na.6 wa Mwaka 2009 kuhusu Utunzaji na Utekezaji wa Taarifa zilizo kwenye mfumo wa elektroni ziliandaliwa na kusambazwa kwa Taasisi za Serikali.

Mkakati wa Serikali Mtandao umekamilika na umeanza kutekelezwa.

Taasisi saba za Serikali (Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Bunge na Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia, Tanzania - *TGDLC*) zimeunganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano ya Serikali (*eGovernment Network*) na zinafanyiwa majaribio.

Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu umewekwa katika ofisi 10 za Wakuu wa Wilaya kwenye mikoa minne (Lindi, Mbeya, Morogoro na Dar es Salaam).

Ujenzi wa kituo cha kuhifadhi kumbukumbu tuli cha Kanda ya Ziwa - Mwanza unaendelea.

Michoro na gharama za ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Tuli cha Dodoma imekamilika. Taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi ziko katika hatua za mwisho na ujenzi utanza mwaka wa fedha ujao (2010/2011 Tathmini ya kumbukumbu za wizara tatu (Afya na Ustawi wa Jamii, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, na *UTUMISHI*) imefanyika ili kubaini majalada yenye umuhimu wa kudumu na yasiyokuwa na umuhimu.

Eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kuwaenzi Waasisi wa Taifa limepatikana wilayani Bagamoyo. Taratibu za kuwatambua wamiliki wa eneo hilo zinafanyika ili tathmini ya kuwalipa fidia ifanyike. Aidha, Mpango wa utekezaji wa uanzishwaji wa Kituo umekamilika. Kuimarisha Uendelezaji wa Sera:- Mpango wa kujenga uwezo wa uendelezaji wa sera kwa kuziimarisha Idara za Sera na Mipango katika wizara tano (Miundombinu, *UTUMISHI*, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, na *TAMISEMI*) umekamilika. Aidha, mafunzo yametolewa kwa watumishi 42 kutoka wizara 24. Mwongozo wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri unahuishwa kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Ufuatiliaji wa utekezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Kiutumishi zilizopo umefanyika katika mikoa 11 (Dodoma, Manyara, Arusha, Mbeya, Rukwa, Kigoma, Singida, Mwanza, Mara, Lindi na Mtwara).

Sera ya Taifa ya Kumbukumbu na Nyaraka imeandaliwa na kuidhinishwa. Aidha, maandalizi ya Sera ya Mafunzo katika Utumishi wa Umma yapo katika hatua za mwisho.

Uhuishaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002, Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Na.19 ya mwaka 2003 na Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Na.6 ya mwaka 2004 unaendelea kwa kuainisha maeneo yenye migongano katika sheria hizi. Maslahi ya watumishi katika Utumishi wa Umma:- Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha kwa Watumishi wa Umma ipo katika hatua za mwisho za kukamilishwa. Uanzishwaji wa Bodi ya Maslahi na Tija katika Utumishi wa Umma upo katika hatua za mwisho.

Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma pamoja na Baraza Kuu la Wafanyakazi yameendelea kukutana kwa mujibu wa sheria.

Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa umebadilishwa na kuwa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa. Kuimarisha Uwajibikaji na Usikivu kwa umma:-

Uhamasishaji juu ya namna bora ya kushughulikia malalamiko umefanyika katika taasisi 18 za umma na mafunzo kwa maofisa wanaoshughulikia malalamiko katika taasisi hizo yamefanyika.

Rasimu ya Mfumo wa kufuatilia Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma imekamilika. Warsha iliyoshirikisha Asasi za Kiraia kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kuainisha maeneo na mikakati ya ushirikiano ilifanyika. Mikutano kuhusu ukuzaji wa maadili kwa watumishi wa umma ilifanyika katika wilaya na halmashauri za mikoa minne ya Mtwara, Ruvuma, Tabora na Singida. Mwongozo wa Uwajibikaji katika Taasisi za Umma umekamilika. Mikutano ya kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imefanyika katika wilaya 14 za Mikoa ya Tabora na Shinyanga.

Kuratibu Sherehe za Siku ya Utumishi wa Umma zinazofanyika Mkoani Mwanza ambapo Taasisi 150 za Serikali zinashiriki katika maonesho kuanzia tarehe 17 hadi 23 Juni, 2010 kwa lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali. Kuimarisha Usimamizi wa Watumishi wa Umma:-

Malalamiko 458 kati ya 497 yatokanayo na ukiukaji wa Kanuni na Taratibu yamepatiwa ufumbuzi na wahusika wamepeva mrejesho. Watumishi 25 kutoka Taasisi za Serikali 25 walipatiwa mafunzo ya namna ya kuandaa Mipango ya Mafunzo kwa ajili ya taasisi zao. Watumishi 45 waliokuwa nje ya Utumishi wa Umma kwa sababu mbalimbali wamerudishwa kazini, 380 wamehamishwa na 134 wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali. Mafunzo mbalimbali yametolewa kwa Watumishi wa Umma 574 ndani na nje ya nchi wakiwemo watumishi wenye ulemavu 11.

Watumishi wa Umma 50 wakiwemo wenye ulemavu 25 kutoka katika Wizara nne na Halmashauri za Wilaya za mikoa mitano wamepatiwa mafunzo ya jinsi ya kupambana na janga la *UKIMWI*.

Ukaguzi wa watumishi na orodha ya malipo ya mishahara umekamilika katika Idara ya Mahakama na unaendelea katika Wizara mbili (Kilimo, Chakula na Ushirika; na

Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi). Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeanzishwa na imeanza kutekeleza majukumu yake.

Mfumo wa kurahisisha uwasilishaji wa Taarifa za Kiutumishi umeanzishwa katika Halmashauri tatu za majaribio (Kisarawe, Kibaha na Bagamoyo) na unatarajiwa kusambazwa katika Halmashauri 26 za pembezoni mwa nchi.

Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Toleo la Mwaka 1994 zimehuishwa na zitaanza kutumika Julai Mosi 2010. Mwongozo wa Kusimamia Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma umekamilika. Uendelezaji wa Uongozi wa Utumishi wa Umma: - Taratibu za kuanzisha Chuo cha Kuendeleza Viongozi katika Utumishi wa Umma zimekamilika na Mkurugenzi wa Chuo hicho ameteuliwa.

Mafunzo ya Uongozi yametolewa kwa Viongozi 589 wa ngazi mbalimbali ndani na nje ya nchi. Tathmini ya Ubora wa Viongozi kwa kuzingatia Mwongozo wa Vigezo vya Uongozi Bora katika Utumishi wa Umma imekamilika. Uratibu wa Programu ya Mabadiliko ya Utendaji katika Utumishi wa Umma: - Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko ya Utendaji katika Utumishi wa Umma katika taasisi 65 ulifanyika. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliwezesha kuandaa Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma. Vikao vitatu vya Usimamizi wa Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma vimefanyika. Kitengo cha Uratibu wa Mabadiliko katika Utumishi wa Umma chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi kimeendelea kuwezesha ili kutekeleza majukumu yake. Kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa; Viongozi Wastaafu wa Kitaifa 13 wameendelea kuhudumiwa kwa mujibu wa Sheria Na.3 ya Mwaka 1999 na Marekebisha yake ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inasimamia taasisi mbili ambazo zinatoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi wa Umma na watumishi wa sekta nyingine. Taasisi hizi ni: Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania na Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia (*Tanzania Global Development Learning Centre*). Katika mwaka wa fedha 2009/2010 taasisi hizi zimetokeleza yafuatayo: -

Chuo cha Utumishi wa Umma: -

Kujenga uwezo kwa kuajiri watumishi 18 wa kada mbalimbali na kuwapatia Watumishi 28 mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Kutoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi wa Umma 6,180 na kutoka Sekta Binafsi 2,535.

Aidha, Chuo kimeendelea kutoa ushauri katika Utumishi wa Umma. Kuanzisha Tawi la Mtwara ambalo lilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 23/10/2009. Aidha, ukarabati wa majengo ya Chuo Makao Makuu na matawi ya Tabora na Mtwara unaendelea.

Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia, Tanzania (*Tanzania Global Development Learning Centre*): -

Ukarabati wa Ofisi za Kituo awamu ya kwanza umekamilika.

Mafunzo yametolewa kwa Watumishi watatu wa Kituo kwa njia ya Mtandao.

Kituo kimeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika utoaji wa mafunzo. Taasisi hizo ni pamoja na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Chuo cha Utumishi cha Ethiopia, Chuo cha Utumishi cha Singapore na Taasisi ya Utawala ya Kenya. Kituo kimetoa mafunzo katika maeneo mbalimbali kwa Watumishi wa Umma 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajira na Maslahi ya Watumishi wa Umma. Katika kushughulikia masuala ya ajira na maslahi ya Watumishi wa Umma, Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

(a) Ajira: Vibali vya ajira mpya 44,857 kati 45,568 sawa na asilimia 98.4 vilivyoidhinishwa kwa mwaka 2009/2010 vilivyotolewa kwa waajiri mbalimbali.

(b) Upandishwaji vyeo; Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa 45,269 walipandishwa vyeo. Idadi hii ni sawa na asilimia 80 ya watumishi 56,586 walioidhinishwa kupandishwa vyeo kwa mwaka 2009/2010.

(c) Mishahara; Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mishahara katika Utumishi wa Umma (1999) imehuishwa. Aidha, rasimu ya Sera mpya ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma (2010) imeandaliwa kwa lengo la kuwianisha malipo ya mishahara kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuhakiki na kuidhinisha madai ya mapunjo na malimbikizo ya mishahara ya Watumishi wa Umma. Hadi mwezi Mei, 2010 jumla ya watumishi 45,846 wamelipwa malimbikizo na mapunjo ya mishahara yenye thamani ya shilingi 58,084,735,629. Kati ya hawa, 20,760 ni walimu na 25,086 ni watumishi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, OFISI YA RAIS, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

Jumla ya Viongozi wa Umma 7,819 wa kada mbalimbali walitumiwa Fomu za Tamko la Mali na Madeni kwa kipindi kilichoishia 31 Desemba, 2009. Hadi mwezi Aprili, 2010 Viongozi wa Umma 6,737 sawa na asilimia 86.16 ya Viongozi wa Umma waliwasilisha Tamko la Mali na Madeni. Aidha, Viongozi wa Umma 1,082 sawa na asilimia 13.84 wa kada mbalimbali hawajawasilisha Tamko lao. Sekretarieti inaandaa taratibu za kuwafikisha viongozi husika kwenye Baraza la Maadili.

Jumla ya malalamiko 171 dhidi ya Viongozi wa Umma yamepokelewa, kuchambuliwa na kufanyiwa uchunguzi wa awali ili kubaini ukweli wa malalamiko hayo.

Kati ya hayo, malalamiko 89 yanahusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Malalamiko yanayobaki hayaihusu Sheria hii hivyo yamewasilishwa kwa vyombo husika kwa ajili ya kuchukua hatua. Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma 809 wa Kada mbalimbali nchini kote ilihakikiwa kwa lengo la kuthibitisha ukweli wa taarifa walizotoa kwenye Tamko. Viongozi waliohakikiwa mali zao ni pamoja na Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wabunge, Madiwani, Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma, Mahakimu Wakazi, Makamishna wa Tume na Wakurugenzi katika Wizara na Idara za Serikali.

Kutoa elimu ya Maadili kwa Viongozi wa Umma kwa njia mbalimbali ikiwemo radio, semina na machapisho. Semina kuhusu Utawala Bora na Maadili zilitolewa kwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala tarehe 27 na 28 Aprili, 2010. Aidha, Mada kuhusu Utawala Bora na Maadili zilitolewa kwa Waheshimiwa Madiwani 529 wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa 18.

Elimu ilitolewa pia kwa wananchi kwa njia ya machapisho ikiwa ni pamoja na kusambaza nakala 2,000 za Jarida la Maadili, nakala 8,000 za Kalenda za ukutani, nakala 2,000 za Kalenda za mezani na nakala 4,000 za vipeperushi vyenye ujumbe kuhusu Maadili. Sekretarieti ilishiriki katika Maonesho ya Nane Nane mwaka 2009 Mjini Dodoma. Jumla ya wananchi 1,817 wakiwemo Viongozi wa Umma walitembelea Banda la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kupatiwa maelezo kuhusu kazi na majukumu ya Sekretarieti na misingi ya Maadili inayopaswa kuzingatiwa na Viongozi wa Umma.

Kuandaa taratibu za kutenganisha Uongozi wa Umma na shughuli za Biashara ili kuondoa mgongano wa maslahi katika Uongozi wa Umma.

Baraza la Maadili limeundwa na Wajumbe wameteuliwa na kuapishwa.

Kusimamia Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi chini ya Mpango wa Taifa wa Uwajibikaji, Uwazi na Uadilifu (*Accountability, Transparency and Integrity Programme (ATIP)*). Kamati ya Uendeshaji wa Mfuko iliidhinisha na kutoa ruzuku yenye jumla ya Sh.1,575,396,200 kwa Taasisi 28 zikiwemo za Serikali, Vyama vya Kiraia na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. (Taasisi za Serikali mbili, Asasi za Kiraia 23 na Vyama vya Kitaaluma tatu). Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyopewa ruzuku unaendelea kufanyika.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Sekretarieti inakamilisha taratibu za ujenzi wa Makao Makuu (Maadili House) Jijini Dar es Salaam na Ofisi ya Kanda Mtwara. Aidha, ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti Kanda ya Kusini Mtwara umeanza. Taratibu za kupata kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki eneo la Chalinze zinaendelea.

Mheshmiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizokamilishwa ni pamoja na kuhuisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja, kukamilisha Mpango Mkakati wa Sekretarieti. Aidha, katika kuimarisha uwezo wa Sekretarieti watumishi 39 wamepewa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, elimu kuhusu athari za maambukizi na kuenea kwa Virusi vya *UKIMWI* na *UKIMWI*; na mafunzo ya Huduma kwa Mteja yametolewa kwa watumishi wote.

Mheshmiwa Mwenyekiti, OFISI YA RAIS, Tume ya Mipango. Tume ya Mipango imeendelea kutekeleza majukumu yake makuu ya msingi ambayo ni pamoja na kuishauri Serikali kuhusu Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na kutoa Mwongozo wa Uchumi wa Taifa pamoja na kubuni sera za uchumi, kuishauri Serikali kuhusu menejimenti ya uchumi na kufanya tafiti ambazo zitawezesha kubuni mikakati ya maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Mheshmiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

Mapendekezo ya kisera yanayotokana na matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2008/2009 yameandaliwa na yamewasilishwa katika mamlaka husika kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Kuibua maeneo ya kiuchumi na kijamii ya kufanyiwa utafiti ambayo yameanza kufanyiwa kazi katika mwaka huu wa fedha 2009/2010.

Mpango wa mafunzo kwa watumishi wa Tume umeanza kutekelezwa. Hadi Aprili 2010, watumishi 61 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Aidha, watumishi 18 walioajiriwa katika mwaka 2009/2010 walipatiwa mafunzo elekezi.

Kuandaa Mpango Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano. Kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Mheshmiwa Mwenyekiti, OFISI YA RAIS, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni chombo kipya kilichoanzishwa kwa mujibu wa kifungu 29 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebisha na Sheria Na.18 ya mwaka 2007. Majukumu ya Sekretarieti ya Ajira ni:-

Kutafuta wataalam wenye ujuzi na kuandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa (database) za wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira.

Kuandaa orodha ya wahitimu wa vyuo vikuu na wataalam wenye weledi (professionals) kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma. Kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika Utumishi wa Umma na kufanya usaili.



Kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na mchakato wa ajira.

Mheshmiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Sekretarieti ya Ajira ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

Kuwajengea uwezo Watendaji wa Sekretarieti ya Ajira kwa kuwapa mafunzo elekezi.

Kutangaza nafasi wazi za kazi 2,924 kutoka kwa waajiri na kufanya usaili. Kuwatembelea waajiri 24 kuelezea majukumu ya Sekretarieti ya Ajira na kupata uzoefu.

Mheshmiwa Mwenyekiti, OfiA RAIS, Tume ya Utumishi wa Umma. Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika Mwaka wa fedha 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

Kufanya vikao vya kisheria vitatu na vikao viwili vya dharura vilivyotolea maamuzi mbalimbali kuhusu Rufaa 73 na malalamiko 109.

Kufanya ukaguzi katika Mamlaka za Ajira na Nidhamu 27 ambazo katika kaguzi za awali zilipata kiwango cha chini na hafifu katika uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Kufanya ukaguzi katika Mamlaka kuhusu mchakato wa ajira mpya na upandishwaji vyeo katika Taasisi 18. Makala 26 zinazohusu kuwaelimisha wadau kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kama ilivyo rekebisha kwa Sheria Na.18 ya mwaka 2007; na majukumu ya Tume ziliandaliwa na kuchapishwa katika Magazeti.

Kutembelea na kufanya mazungumzo na Wadau wake katika Ofisi za Sekretarieti za Mikoa 18, Mamlaka za Serikali za Mitaa 83 pamoja na kutembelea Watumishi wa Taasisi za Muungano Tanzania Zanzibar.

Mikutano ya kazi na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 127, Wenyeviti wa Kamati za Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) wa Mikoa na Wilaya 121, Maafisa Tawala na Maafisa Rasilimaliwatu wakuu wa Wakala wa Serikali 20 na Maafisa wa Sekretarieti za Mikoa 18 imefanyika.

Kufuatilia Taratibu za Uendeshaji katika Utumishi wa Serikali za Mitaa, Afya na Walimu. Taratibu hizo zimekamilika na kuanza kutumika. Watumishi wa Tume 196 kati ya watumishi 630 sawa na asilimia 31.1 walipimwa VVU na kupewa ushauri nasaha. Kuratibu vikao vitatu vya Kamati za Ajira za Idara za Utumishi wa Walimu katika Mamlaka za Ajira na Nidhamu 132 na Mikoa 21 ambapo Walimu 6,011 wamesajiliwa; 7,758 wamethibitishwa kazini; 16,408 wamepandishwa vyeo; 4,103 wamebadilishwa vyeo.

Aidha, mashauri ya nidhamu 226 yameshughulikiwa, vibali 162 vya maombi ya kustaafu walimu vimeshughulikiwa na mafao 337 ya kazi mikataba kwa walimu na mafao ya vifo (death gratuity) yalikokotolewa kwa ajili ya malipo. Kufanya tafiti tatu kuhusu utendaji katika Utumishi wa Umma ambapo mchakato wa kufanya utafiti huu umekamilika na kazi hii ya utafiti inaendelea na inatarajia kukamilika mwezi Juni, 2010.

Miongozo mitatu kuhusu masuala ya ajira na nidhamu (Mwongozo wa masuala ya ajira katika Utumishi wa Umma; Toleo Na.2 la 2009, Mwongozo wa Ukaguzi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma; Toleo Na.1 la 2009 na Mwongozo wa Masuala ya Nidhamu; Toleo Na.2 la 2009) imehuishwa na kusambazwa katika Mamlaka za Ajira na Nidhamu pamoja na kuelimisha wadau kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Rejea inayounganisha pamoja Taratibu za uendeshaji za makundi manne ya Utumishi Serikalini, Ualimu, Afya na Serikali za Mitaa imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshmiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha uwezo wa Tume, kazi zifuatazo zilifanyika: watumishi wapya 79 wameajiriwa, watumishi 30 wamepandishwa vyeo na watumishi 44 walithibitishwa kazini. Aidha, watumishi 386 walipata mafunzo kuhusu Mfumo wa Wazi wa Kupima Utendaji Kazi, watumishi 138 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi ya rasilimaliwatu na mafunzo elekezi; na watumishi 104 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuwajengea uwezo kiutendaji.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Mapendekezo Ya Mpango Wa Utekelezaji Kwa Mwaka Wa Fedha 2010/2011. Baada ya maelezo ya kina kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 na Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2009/2010 kwa Mafungu 20, 30, 32, 33, 66, 67 na 94 sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Shughuli kwa mwaka 2010/2011 kwa mafungu haya kama ifuatavyo:-

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Ikulu. Katika mwaka 2010/2011, Ofisi ya Rais imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-(a)Ikulu:-Kutoa huduma kwa Mheshimiwa Rais. Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo mbalimbali kama vile, uchumi, siasa, jamii, sheria, uhusiano wa kimataifa na kadhalika.

Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Pili wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, kufuatilia mapitio ya mpango huu na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora. Kuanzisha Tovuti ya Rais na kutoa mafunzo kwa watumishi watakaohudumia Tovuti hii.

Kuandaa na Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na *UKIMWI* mahali pa kazi. Kutoa huduma za ushauri nasaha na kupima kwa hiari kujua hali ya maambukizi ya Virusi vya *UKIMWI* na kuwahudumia watumishi waishio na Virusi vya *UKIMWI* na *UKIMWI*.

Kutoa mafunzo kwa watumishi kulingana na mpango wa mafunzo ili kuwaongezea ujuzi na ubora wa kiutendaji. Kufanya uchambuzi wa Nyaraka na kutoa ushauri kwa Wizara juu ya uandishi wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na kuendelea kuhudumia Baraza la Mawaziri na Kamati zake, Kamati ya Makatibu Wakuu (*IMTC*) na Kamati zake.

Kushughulikia rufaa za watumishi wa umma zinazoletwa kwa Rais na Katibu Mkuu Kiongozi.Kupitia upya Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kufuatilia utekelezaji wake.Kupitia upya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, Ikulu.Kuratibu Programu za

Mabadiliko katika Sekta za Umma. Taasisi yauia na Kupambana na Rushwa (*TAKUKURU*).

Kuchunguza tuhuma 2,258 zilizopo na tuhuma mpya zitakazopokelewa.

Kuendesha kesi 399 zilizopo mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na chunguzi mbalimbali zinazoendelea. Kuchunguza vitendo vyote vya rushwa kabla na baada ya kura za maoni kwa vyama vyote vitakavyoshiriki uchaguzi mkuu 2010, wakati wa kampeni, upigaji kura, baada ya uchaguzi na kuchukua hatua zinazostahili kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 2007 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sanjari na Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na.6 ya mwaka 2010.

Kufanya tafiti nne katika Jeshi la Polisi, Mahakama, Kilimo na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kushauri namna bora ya kuziba mianya hiyo pamoja na kuendesha warsha tatu za kujadili matokeo ya tafiti hizo.

Kuwaelimisha na kuwajengea uwezo na ujasiri Watumishi wa Serikali, Mashirika ya Umma na Binafsi wa kushiriki katika kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa katika maeneo yao ya kazi.

Kuelimisha wananchi kwa kutumia vyombo vya habari, kalenda, vipeperushi, “stickers”, “wheelcovers” na “posters” ili wajiepushe na vitendo vya rushwa na kutoa taarifa za wote wanaojihusisha na vitendo vya kupokea na kutoa rushwa katika Ofisi za *TAKUKURU* za Wilaya, Mikoa na Makao Makuu.

Kubuni njia za kisasa na kitaalam za kuelimisha na kuhamasisha wananchi ili washiriki na kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa. ufuatilia na kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zinafanya kazi iliyokusudiwa sanjari na kuendelea kuwaelimisha wananchi kusaidia kufuatilia matumizi ya fedha hizo katika Mamlaka zao. Kuajiri watumishi wapya 26 na kuwapatia mafunzo elekezi; kutoa mafunzo kwa watendaji wa ngazi ya kati kwa watumishi 150 na mafunzo ya uongozi kwa watumishi 40. Kamilisha ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Manyara na Lindi, Ofisi za Wilaya za Mpanda na Iramba; na kuanza ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Pwani na ofisi mbili za Wilaya za Misenyi na Newala. Kuvijengea uwezo vitengo vya mipango na mifumo ya taarifa na upashanaji habari ili kuongeza ufanisi wa taasisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (*MKURABITA*). uendelea na marekebisho ya sheria na taratibu za kurasimisha ardhi na biashara Tanzania Bara na katika Visiwa vya Unguja na Pemba. Kuendelea na urasimishaji wa ardhi vijijini katika Wilaya nyingine 20 za Tanzania Bara na wilaya tano Zanzibar. Hii ni pamoja na ujenzi wa Masijala za Ardhi za vijiji katika wilaya hizo. Kuendelea na urasimishaji wa ardhi ya mijini katika miji ifuatayo: Dar es Salaam, Arusha, Morogoro na Mbeya kwa Tanzania Bara na maeneo mawili ya Mji wa Zanzibar.

Kuendelea na urasimishaji wa Biashara katika Majiji ya Mwanza na Tanga; Manispaa za Ilala na Arusha, na wilaya moja moja katika Mikoa ya Kilimanjaro na Pwani kwa Tanzania Bara na maeneo mawili ya Zanzibar. Kuunda Kitengo maalum cha

kuwezesha wamiliki wa rasilimali na biashara zilizorasimishwa ili zitumike kama dhamana za kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha.

Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano ili kutoa elimu kwa kuanzisha Vituo vya Mawasiliano katika kanda 5 nchini na kuweka miundombinu ya kompyuta na “internet” kwa ajili ya kurahisha upatikanaji wa taarifa. (d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa 132 na Visiwa vya Unguja na Pemba kutekeleza miradi 1,200 itakayoibuliwa na wananchi.

Kutoa huduma za kitaalam na ushauri wa namna ya kutekeleza miradi ya jamii kwa ufanisi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote na vikundi vya jamii (walengwa). Kujenga uwezo kwa wataalam wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote kuhusu uundaji wa Vikundi vya Uwekaji Akiba, Usimamizi, Uwekaji Kumbukumbu na Ujasiriamali. Aidha, kuendelea kutoa vifaa kwa walengwa pamoja na kuwaunganisha na huduma za kibenki ili waweze kupata mikopo. Kutekeleza Mpango wa kijamii wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini sana katika Wilaya za majaribio za Kibaha, Bagamoyo na Chamwino.

Aidha, kutafanyika tathmini ya ufikiaji malengo ya mpango na kuongeza idadi ya kaya za kupatiwa msaada kwa kaya 16,000 ambazo hazijafikiwa ndani ya Wilaya tatu za majaribio. Kuendelea kuimarisha Mifumo ya Taarifa na Kumbukumbu za miradi, ufuatiliaji na tathmini.

Kusimamia umaliziaji wa miradi iliyopita ambayo ina mahitaji ya ziada ili ikamilike na kutoa huduma zilizokusudiwa. Kufanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa fedha zote za miradi zinatumika kama ilivyokusudiwa, ubora na thamani ya fedha vinakuwepo pamoja na viwango vya ubora vinavyozingatia miongozo ya sekta husika.

Kutekeleza miradi 400 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 40, Unguja na Pemba ili kupunguza makali ya upungufu wa chakula kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi duniani.

Kukuza uelewa wa walengwa kuhusu kanuni na taratibu za utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na jamii kwa kutumia vyombo vya habari kama vile radio, televisheni na magazeti juu ya taratibu mbalimbali za kupata fedha, usimamizi na kukabidhi miradi. Kuendelea kukamilisha mchakato wa kuwezesha TASAF kuwa Taasisi ya kudumu ili iweze kufanya kazi zake za kufikisha huduma kwa wananchi kwa uhakika zaidi.

Mfuko wa Rais wa Kujitegemea Kutoa huduma ya mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati mijini na vijijini katika matawi 19 ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea yaliyopo; Kutoa huduma ya ushauri na mafunzo ya kibiashara kwa wateja kwa kushirikiana na Taasisi mbali mbali zinazotoa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika biashara zao katika matawi 19 ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea yaliyopo. Kujenga uwezo kwa wadau/watendaji na wafanyakazi ili kuweza kutoa huduma za viwango vya juu na kuongeza tija katika utoaji wa mikopo katika matawi 19 ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea yaliyopo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa Fedha 2010/2011 kwa ufanisi, kwa Fungu 20 na 30 zinaombwa fedha kama ifuatavyo:-

Fungu 20 Sh. 8,810,623,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fungu 30 Sh. 238,557,726,000. Kati ya fedha hizi Sh. 171,265,647,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 67,292,079,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Menejimenti Ya Utumishi Wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa.

Haya yatafikiwa kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-Kuhuisha na kuwianisha Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazosimamia utendaji katika Utumishi wa Umma. Kuhuisha miundo, mifumo ya utendaji na viwango vya Ki-menejimenti vinavyolenga katika kuboresha utoaji wa huduma katika Utumishi wa Umma. Kuhakikisha kwamba Serikali inajishughulisha na majukumu mahsusi ambayo yanaendeshwa kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Kusimamia matumizi sahihi ya rasilimaliwatu pamoja na kuratibu ajira katika Utumishi wa Umma.

Kukuza na kusimamia uzingatiaji wa maadili katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utendaji na hivyo kupunguza malalamiko na kero mbalimbali. Kuelimisha umma kuhusu mabadiliko yanayoendelea katika Utumishi wa Umma kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano.

Kusimamia uendelezaji wa stadi za uongozi na kuwaendeleza Watumishi wa Umma kitaaluma kwa kuzingatia makundi maalum. Kuimarisha mifumo ya taarifa, mawasiliano ya habari na matumizi ya *TEKNOHAMA* Serikalini. Kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuendeleza mabadiliko katika Utumishi wa Umma Tanzania Zanziba Kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa kwa mujibu wa Sheria. Kuendelea na mchakato wa kuanzisha Kituo cha kuwaenzi Waasisi wa Taifa. Kujenga Kituo cha Taifa cha kuhifadhi kumbukumbu tuli Dodoma na cha Kanda Mwanza. Kuweka mfumo bora wa masijala katika ofisi 15 za Wakuu wa Wilaya. Kusimamia utekelezaji wa masuala ya anuai za jamii katika Utumishi wa Umma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ajira Na Maslahi Ya Watumishi Wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali inatarajia kutumia shilingi trilioni 2.332 kugharamia malipo ya mishahara, ajira mpya, upandishwaji vyeo na kulipia madai ya malimbikizo na mapunjo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Kiasi hiki ni asilimia 38.84 ya Mapato ya Ndani. Aidha, kiasi hiki kimeongezeka kwa shilingi bilioni 558 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 31.5 ya fedha zilizotengwa kugharamia malipo hayo katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshmiwa Mwenyekiti, mishahara ya Watumishi wa Umma itaongezwa kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa katika Baraza la Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma, Serikali imeandaa Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha Katika Utumishi wa Umma. Baada ya Sera hiyo kupitishwa, Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo utaandaliwa. Aidha, Serikali itakamilisha uanzishaji wa Bodi ya Maslahi na Tija katika Utumishi wa Umma.

Mheshmiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 49,593 ambapo kipaumbele kitakuwa katika sekta za Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo. Aidha, Serikali inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 64,404 wa kada mbalimbali.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Taasisi za Mafunzo. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inasimamia taasisi mbili zinazotoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi wa Umma na watumishi wa sekta nyingine. Taasisi hizi ni Chuo cha Utumishi wa Umma na Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia Tanzania (*Tanzania Global Development Learning Centre*). Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Taasisi hizi zinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Chuo cha Utumishi wa Umma (*TPSC*).

Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma 8,500 na Sekta Binafsi 5,500.

Kutoa shauri 10 za kuboresha utendaji na usimamizi wa Utumishi wa Umma.

Kufanya tafiti tano za kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa umma. Kuwajengea uwezo watumishi 40 wa Chuo katika mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Kuimarisha jarida la Makala Maalum za Menejimenti ya Utumishi wa Umma (*Public Sector Management Journal*). Kuendelea na ukarabati wa majengo ya ofisi Makao Makuu na Matawi ya Chuo ya Mtwara na Tabora.

(b) Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia Tanzania (*TGDLC*).

Kuandaa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya mafunzo kwa njia ya mtandao. Kuendesha mikutano ya kikanda kwa njia ya mtandao. Kuendelea na ukarabati wa majengo ya kituo na kujiimarisha kitaaluma ili kukidhi mahitaji yanayotokana na maendeleo ya kiteknolojia.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa Fedha 2010/2011 kwa ufanisi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia Sh.39,127,948,000. Kati ya fedha hizi Sh. 16,557,348,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 22,570,600,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Sekretarieti Ya Maadili Ya Viongozi Wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itaendelea na jukumu lake la kukuza na kuimarisha maadili katika Uongozi wa Umma kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

Kutoa mafunzo ya Utawala Bora hususan Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Viongozi wapya baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Kuandaa na kuendesha mjadala utakaochangia maandalizi ya maadili ya kitaifa.

Kushirikiana na taasisi husika kuandaa Mitaala ya Maadili kwa ajili ya kufundisha somo la Maadili katika Shule za awali, Sekondari na Vyu.

Kukamilisha utaratibu wa kutenganisha Uongozi wa Umma na shughuli za Biashara.

Kufanya Uhakiki wa Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma 1,000 wa Kada mbalimbali.

Kushughulikia masuala ya ukiukaji wa maadili kuhusu Viongozi wa Umma kwa kadri yatakavyowasilishwa kwa njia ya malalamiko au kubainishwa na Sekretarieti.

Kusimamia Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi na kuidhinisha maombi mapya ya kupatiwa ruzuku, kufuatilia utekelezaji na kufanya tathmini ya miradi iliyopatiwa ruzuku kutoka katika mfuko huu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Mfuko unatarajia kutoa ruzuku ya kiasi cha Sh.1,500,000,000. Kutoa elimu ya maadili kwa viongozi na wananchi kwa njia ya semina, vipindi vya radio, machapisho, maonesho na maadhimisho mbalimbali.

Kujenga uwezo wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kuajiri watumishi wapya 17; kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Maadili na watumishi 60; pamoja na kununua vitendea kazi.

Kujenga Ofisi ya Makao Makuu na Kanda ya Kusini (Mtwara) pamoja na kuanzisha Ofisi ya Kanda ya Mashariki (Chalinze mkoani Pwani).

Mheshmiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa Fedha 2010/2011 kwa ufanisi, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inatarajia kutumia Sh.3,482,169,000. Kati ya fedha hizi Sh.2,292,169,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.1,190,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Tume Ya Mipango. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Tume ya Mipango itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

Kupitia Malengo na Viashiria vya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kubaini kama bado vinaendana na matakwa ya mstakabali wa maendeleo ya Taifa. Kuandaa mfumo mpya wa utayarishaji mipango kutoka mfumo wa mpango wa miaka mitatu hadi miaka mitano. Kuandaa mpango wa maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2011-2016. Kutoa mwongozo wa sera za kitaifa kumwezesha mwananchi kushiriki katika ukuaji na mageuzi ya kiuchumi.

Kutafiti na kutathmini rasilimali zilizopo na kuelekeza matumizi sahihi kwa maendeleo ya Taifa na kupunguza umasikini. Kuibua na kufanya tafiti za kina kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii. Kujenga uwezo wa Tume kitaaluma ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kuratibu na kuchambua mwelekeo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika ngazi za kisékta, kitaifa, kikanda, kimataifa na kubainisha changamoto zitakazojitokeza. Kutekeleza masuala mtambuka kama vile mazingira, masuala ya UKIMWI, Jinsia na Utawala Bora.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa Fedha 2010/2011 kwa ufanisi, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inatarajia kutumia Sh.5,936,827,000. Kati ya fedha hizi Sh.5,759,827,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 177,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Sekretarieti Ya Ajira Katika Utumishi Wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Sekretarieti ya Ajira itaendelea kutekeleza majukumu yafuatayo:-

Kuandaa Kanzidata za Wataalam ili kurahisisha mchakato wa ajira. Kuandaa orodha ya wahitimu wa Vyuo Vikuu na Wataalam Weledi (*Professionals*) kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma.

Kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na mchakato wa ajira. Kuendesha mchakato wa ajira kwa nafasi 49,593 mara baada ya kupata vibali vya ajira kutoka kwa Waajiri mbalimbali. Kufungua Ofisi za Kanda saba ili kusogeza huduma karibu na wadau wa mikoani na kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji Watumishi wa Sekretarieti.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa Fedha 2010/2011 kwa ufanisi, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inatarajia kutumia Sh. 4,005,380,000. Kati ya fedha hizi Sh. 3,005,380,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 1,000,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ofisi Ya Rais, Tume Ya Utumishi Wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Tume ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Kupokea na kushughulikia rufaa za watumishi dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka za Ajira na Nidhamu.

Kuhuisha Miongozo mbalimbali na kuisambaza kwa mamlaka za Ajira na Nidhamu. Kukagua uzingatiaji wa mifumo mbalimbali ya kimenejimenti katika Utumishi wa Umma. Kufanya ukaguzi wa kawaida wa Rasilimali watu katika Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuhusu uzingatiaji wa Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma.



Kufanya kaguzi Maalum kufuatia malalamiko ya watumishi kuhusu ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma. Kuendesha mikutano ya Tume kwa mujibu wa Sheria. Kuelimisha wadau kuhusu shughuli za Tume kupitia vyombo vya habari na kufanya mikutano ya wadau. Kutoa elimu kuhusu maadili ya kazi na kujiepusha na mazingira hatarishi kwa maambukizi ya *VVU/UKIMWI*.

Idara ya Utumishi wa Walimu ndani ya Tume itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria kama Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu.

Aidha, mikutano ya robo mwaka katika Mikoa 21 na Wilaya 113 itafanyika. Kufanya tafiti kuhusu masuala ya rasilimaliwatu kulingana na mahitaji ya Tume na wadau wake. Kutoa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Kupima Utendaji Kazi kwa watumishi wapya wa Tume na kuendelea kugharamia mafunzo ya watumishi 104 wanaoendelea na masomo.

Kuhuisha Mpango Mkakati wa Tume uliopo na kuandaa Mpango Mpya. Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wake katika ngazi za wilaya, mikoa na Makao Makuu kwa kuwajengea uwezo wa kiutendaji na kuongeza vitendea kazi.

Mheshmiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa Fedha 2010/2011 kwa ufanisi, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia Sh.8,063,940,000. Kati ya fedha hizi Sh. 7,970,865,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 93,075,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Majumuisho. Ili tuwe na uchumi imara na endelevu tunahitaji Utawala bora ambapo Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinatumika katika kusimamia uchumi na uendeshaji wa shughuli za Umma. Taasisi zenye jukumu la kuhakikisha mazingira haya yanakuwepo ni Ofisi za Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Mipango, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma.

Hivyo Mipango ya Utekelezaji ya 2010/2011 ya Taasisi hizi inalenga kufanikisha majukumu haya. Mheshmiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina majukumu yetu na mipango ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2010/2011, naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka 2010/2011 kama ifuatavyo:-

(a) **Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu**

Matumizi ya Kawaida Sh. 8,810,623,000

**Jumla Sh. 8,810,623,000**

(b) **Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 171,265,647,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 67,292,079,00

**Jumla** Sh. 238,557,726,000

**(c) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 16,557,348,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 22,570,600,000

**Jumla** Sh. 39,127,948,000

**(d) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi**

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 2,292,169,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 1,190,000,000

**Jumla** Sh. 3,482,169,000

**(e) Fungu 66: Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango**

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 5,759,827,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 177,000,000

**Jumla** Sh. 5,936,827,000

**(f) Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 3,005,380,000

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 1,000,000,000

**Jumla** Sh. 4,005,380,000

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

(i) Matumizi ya Kawaida Tsh. 7,970,865,000

(ii) Miradi ya Maendeleo Tsh. 93,075,000

**Jumla** Tsh. 8,63,940,000

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa hotuba uliyoitoa. Ninaamini kabisa, Waheshimiwa Wabunge tumeisikiliza kwa makini. Sasa nimwite Msemaji wa Kamati. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kupokea majina ya ambao wangenda kuchangia

asubuhi ya leo ili tuweze kupanga muda wetu sawa sawa kama unavyojua leo ni Jumamosi.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma), kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais (Ikulu), inahusisha Mafungu Mawili: Fungu 20 - Ofisi ya Rais (Ikulu); na Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuna mafungu matano. Mafungu hayo ni Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; na Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, tarehe 31 Mei, 2010, Kamati ilikutana katika Ukumbi wa Karimjee, kushughulikia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, kama nilivyoeleza hapo juu. Katika kikao chake, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2010/2011, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, (MB), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, akishirikiana na Mheshimiwa Sophia M. Simba, (MB), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo tuliyoelezwa katika Kikao cha tarehe 31 Mei, 2010 ni kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Ikulu) na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais. Katika maelezo hayo, mtoa hoja alieleza pia kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu), pamoja na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa Mwaka 2009/2010, Kamati ilikuwa na maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji na utendaji kazi ya Ofisi ya Rais (Ikulu), pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa sehemu kubwa, ushauri wa Kamati ulizingatiwa, hususan ushauri uliohusu TAKUKURU, TASAF, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mheshimiwa Waziri ilionesha, kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Ofisi ya Rais (Ikulu) na Taasisi zake na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake, zilitekeleza mpango na makadirio ya mapato na matumizi. Katika kikao hicho, Wajumbe walihoji masuala ya msingi kuhusu utekelezaji na kupatiwa majibu ya kina yaliyoridhisha. Naomba pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati iliridhika na utekelezaji wa majukumu na malengo yaliyokuwa yamepangwa kwa fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Kamati, mtoa hoja alieleza kuhusu mipango iliyopo kwa mwaka 2010/2011. Maelezo hayo yalihusu Ofisi ya Rais (Ikulu), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii. Mipango mingine iliyoelezwa ilihusu Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Chuo cha Utumishi wa Umma na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Vilevile, Kamati ilielezwa malengo ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na malengo ya Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, maelezo tuliopewa kuhusu malengo yaliyowekwa kwa Mwaka 2010/2011 kwa mafungu yote, kwa sehemu kubwa yameelezwa na mtoa hoja kabla yangu. Naomba kutoa taarifa kuwa, baada ya kufanya uchambuzi wa kina na majadiliano kuhusu maelezo yaliyotolewa, Kamati iliridhika kuwa malengo hayo ni mazuri na ni vyema yakapatiwa fedha katika kipindi cha mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuhusu fedha zinazoombwa ili kutekeleza Mpango kwa Mwaka 2010/2011 kwa ufanisi. Maelezo hayo yalihusu Mafungu yote chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu) na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Ili kujiridhisha kuhusu makadirio hayo, Wajumbe walipata fursa ya kuhoji masuala mbalimbali kwa kila Fungu na kupatiwa majibu ya ufafanuzi kwa namna ilivyowaridhisha. Napenda kutoa taarifa kuwa, baada ya kupitia kifungu kwa kifungu, Kamati iliridhishwa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia dhima ya Ofisi ya Rais (Ikulu), Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma akishirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo ya Ofisi ya Rais (Ikulu), Fungu 20 na Fungu 30 na kwa kuzingatia kuwa huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu, Kamati inashauri kuwa, umakini uongezwe katika utekelezaji wa majukumu ya TAKUKURU na vyombo vingine muhimu vilivyo chini ya Ofisi ya Rais. Sambamba na ushauri huo ni maoni ya Kamati kuwa, vitendea kazi vya Taasisi muhimu katika mafungu haya, vinapaswa kupewa umuhimu mkubwa ili kuziwezesha taasisi na vyombo husika kufanya kazi yake muhimu wakati huu ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa malengo yaliyoanishwa katika Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, yanazingatia pia majukumu na dhima ya Ofisi hii. Kwa msingi huo, Kamati inashauri kuwa, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Serikali iwezeshe zaidi kifedha, teknolojia na eneo ili iendelee na kazi yake nzuri na muhimu kwa ajili ya Taifa letu. Aidha, Kamati inapendekeza kuwa, uangaliwe uwezekano wa kuifanya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kuwa Mamlaka au Idara inayojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Watumishi katika Utumishi wa Umma, kuna umuhimu mkubwa wa kuwaendeleza Watumishi wa Umma. Tunashauri kuwa ni vyema Serikali ikapanga upya mikakati maalumu kwa ajili ya kuendeleza kujenga uwezo wa Watumishi wa Umma pamoja na kupanga mikakati ya kudumu na watu wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, Vyuvo vya Utumishi wa Umma vilivyopo Mtwara, Tabora na Dar es Salaam, vina mchango mkubwa katika kuwaendeleza Watumishi wa Umma na kuongeza ufanisi wao. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inashauri kuwa, majengo ya vyuo hivyo hususan mabweni yaongezwe, sambamba na kuongeza uwezo wa kudahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumbukumbu za mtumishi ni jambo la msingi na muhimu, serikali iongeze umakini katika kusimamia utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za utumishi wa waajiriwa katika Utumishi wa Umma ili kupunguza kero za upotevu wa kumbukumbu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika kukuza na kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma nchini, pamoja na kuipongeza kwa kazi nzuri inayofanya, tunashauri kuwa, mchakato wa kurekebisha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lengo la kutenganisha biashara na uongozi wa umma, uwahusishe wadau katika eneo hilo kwa namna itakayofaa.

Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ni chombo muhimu kwa ajili ya mwelekeo wa Taifa na kutoa picha halisi ya hali ya maendeleo ya Taifa. Ni vyema Serikali ikasimamia mawasiliano mazuri baina ya Tume ya Mipango na Hazina ili kujiimarisha ipasavyo na kuwa na mikakati madhubuti kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira na Tume ya Utumishi wa Umma, bado wigo wa ajira katika Utumishi wa Umma unahitaji kuongezwa. Kwa upande wa Tume ya Utumishi wa Umma, Kamati inashauri kuwa, mazingira ya kazi kwa Watumishi wa Tume hii waliopo Mikoani na Makao Makuu, yanahitaji kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, kwanza, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Pili, napenda kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Hawa Abdulrahmani Ghasia, (Mb), Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Sophia Simba, (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa wakati wote Kamati tulipochambua Makadirio ya Ofisi hii.

Ninaomba pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma). Jambo kubwa lililofanikisha utoaji wa maoni yao katika mjadala ni pamoja na ujuzi, uzoefu, umahiri na uhodari walionao katika nyanja mbalimbali kwenye Sekta ya Utumishi wa Umma pamoja na masuala ya uendeshaji nchi na Utawala Bora. Kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yusuf R. Makamba, Mjumbe, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mjumbe, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mjumbe, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mjumbe, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mjumbe, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mjumbe, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mjumbe, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mjumbe, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mjumbe, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mjumbe, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mjumbe, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mjumbe, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mjumbe na Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Dkt. Thomas D. Kasililah, Katibu wa Bunge, kwa kusimamia vyema uratibu wa shughuli za Kamati. Kipekee kabisa, nawashukuru pia Makatibu wa Kamati hii Ndugu Athuman Hussein na Elihaika Mtui, chini ya uongozi wa Ndugu Charles Mloka, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, kwa kuratibu vizuri shughuli zote za Kamati na kuhakikisha kuwa, Taarifa hii ya Kamati inakamilika kwa wakati uliopangwa. Nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kujituma katika shughuli za uratibu wa Vikao vya Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likuballi kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na Taasisi zote chini ya Ofisi ya Rais, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, jumla ya shilingi 307,984,613,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mafungu yote kama alivyowasilisha mtoa hoja.

Kipekee, naomba kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Chalinze, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kipindi chote hiki cha miaka mitano kwa kuwatumikia; na mimi nawaahidi sitowaangusha katika kipindi kilichobaki. Ninaishukuru pia familia yangu kwa moyo wa upendo wanaonipa katika kipindi chote katika mazingira magumu ya kuwahudumia Wananchi wa Jimbo la Chalinze katika milima na mabonde. Ninawasihi na kuwaomba Wananchi wa Jimbo la Chalinze, waombe dua kumwombea mpiga kura mwenzetu, Mbunge wetu wa Zamani wa Jimbo la Chalinze, Mwana Chalinze,

Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ili dua hilo liwe dhamira yake ya kuchukua fomu tarehe 21 ibaki palepale bila kuwa na kikwazo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala na hasa kwa maneno yako ya mwisho. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zangu za dhati kwa kunipa fursa hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi pamoja na Tume ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa nimekosa fadhila iwapo sitatoa shukrani kwa Chama changu cha CHADEMA, kwa sababu ndiyo walioniwezesha kuwa hapa. Ninawapongeza Viongozi wote Wakuu na wengine wote, chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mwenyekiti (T), kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni. Pia nalishukuru Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), kwa kuendelea kuonesha imani kwangu. Aidha, nichukue nafasi ya kipekee kabisa, kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Shoka Khamis Juma (MB), Msemaji Mkuu wa Upinzani (Utawala Bora), kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha uandaaji wa Hotuba hii, kwani ni Msemaji Mkuu katika Wizara zinazojumuishwa katika Hotuba hii. Vile vile, natoa pongezi za dhati kwa Viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (MB) na Naibu Kiongozi, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa (MB), kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha hotuba zetu zinaandaliwa vizuri. *(Makofi)*

Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni pamoja na kusimamia na kuweka miongozo ambayo itasaidia kuinua kiwango cha utendaji katika Taasisi za Utumishi wa Umma na hivyo kuifanya Sekta ya Utoaji wa Huduma kwa Umma kutoa huduma bora zaidi ambapo anayepata huduma aipate kwa muda stahili bila ya usumbufu wowote. Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, Utumishi wa Umma ndiyo nyenzo muhimu katika kuendeleza au kuharibu uchumi wa nchi. Imani hii inatokana na ukweli kwamba, Sekta Binafsi au Sekta ya Umma, haiwezi kusonga mbele bila kushirikisha Sekta ya Utumishi wa Umma katika utendaji wake kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhana hii basi, kila shughuli itakayofanywa na taasisi ya kutoa huduma kwa umma, ambayo haitamlenga moja kwa moja mteja ambaye ni mwananchi, basi ihesabike kama ni upotevu wa rasilimali ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendeshwa kwa mzunguko wa mafaili; kukwama kwa mzunguko huo maana yake maamuzi hayafanyiki na hivyo Serikali imesimama kwani watu hawawezi kuendelea kufanya lolote maana maamuzi yote yako kwenye mafaili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa, urasimu unaweza kusababishwa na mambo mengi mojawapo ni kama vile kutokuwepo na watumishi wenye uwezo wa kukabiliana na majukumu ya kazi zao kutokana na taaluma ya kazi husika au kutokana na kutokuwa na *morale* wa kazi, kwa sababu ya maslahi kidogo wanayoyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo hayo yote yanaweza kumalizwa kwa Serikali kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la kuwa na takwimu sahihi za Rasilimali Watu ambao watatoa huduma katika Sekta zote za Uchumi wetu. Kwa mfano, Sekta ya Afya na Elimu zina upungufu mkubwa wa watumishi na ukiangalia mipango yetu hasa katika nyanja za sayansi, mahitaji ni makubwa kuliko uzalishaji wa wataalamu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uchumi endelevu hatuna budi kuwa na takwimu sahihi ya rasilimali watu katika sekta zote, kwa njia hiyo ni rahisi kufanya uwekezaji sahihi bila kuacha ombwe la wajanja kufanya ufasidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa mipango madhubuti iwekwe ya kujua idadi ya wataalam wetu katika kila fani, upungufu na mipango ya kujaza upungufu huo kwa kutumia watu au teknolojia ya mawasiliano hasa katika elimu na huduma za afya. Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa Serikali, katika karne ya teknolojia, kushindwa kuelewa idadi kamili ya Watumishi wake. Uzembe wa kutokuwa na kumbukumbu sahihi huligharimu sana Taifa fedha nyingi ambazo zingeweza kuelekezwa katika kuajiri wataalam ambao wanahitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anawasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2009/2010 hapa Bungeni alisema nanukuu: “Zoezi la uhakiki wa rasilimali watu lililofanyika katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwenye Vyuo vya Ualimu na shule zote za Sekondari za Serikali, Tanzania Bara lilibaini kuwa, watumishi 1,413 hawakuwa katika vituo vyao vya kazi na walilipwa kiasi cha shilingi 3,043,609,699/= kinyume cha Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Taarifa za uhakiki zimekabidhiwa kwa vyombo husika ili hatua za kisheria na kinidhamu ziweze kuchukuliwa dhidi ya waliohusika”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua mpaka sasa ni hatua gani ambazo zimechukuliwa kwa watumishi waliohusika na udanganyifu huo na kuliingizia Taifa hasara kubwa kiasi hicho tena kwenye Wizara moja na ni kiasi gani cha



fedha kilichorejeshwa Serikalini mpaka sasa au bado vyombo vya dola vinachunguza? Maelezo haya ya Waziri, yanahuishwa vipi na jibu la Waziri katika Mkutano huo wa Bunge ambapo Waziri alieleza kuwa kazi ya utambuzi bado inaendelea?

Inakuwaje Waziri huyo huyo, akatoa majibu tofauti kwa jambo hilo hilo, tena kwa jambo kubwa kama hili ambalo linaingizia Taifa hasara kubwa sana. Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa, ni eneo lingine ambako Serikali ya Awamu ya Nne imeshindwa kusimamia majukumu yake kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatumia fedha nyingi kufundisha walimu katika ngazi ya shahada, lakini wanapohitimu karibu nusu yao wanakwenda kwenye shule binafsi, hivyo kuendelea kuwepo kwa upungufu katika shule za Serikali. Hili Mkaguzi Mkuu wa Serikali ameliona pia, je, Serikali imekwishaandaa utaratibu kwa shule binafsi kuchangia gharama za kufundisha walimu katika ngazi mbalimbali ili kufidia gharama amgazo Serikali inatumia kwa kusomesha kisha shule za binafsi zinawachukua pasipo gharama yoyote na kuacha shule nyingi za umma bila walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo kwa Watumishi wa Umma. Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa watumishi wake wanapata mafunzo yanayokidhi matakwa na hali halisi ya ushindani katika dunia ya sasa. Lakini matumizi yoyote kwa ajili ya shughuli hiyo yanatakiwa kuangalia na hali halisi ya nchi yetu ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mkaguzi inaonyesha kuwa shilingi 16,785,000/= zililipwa kwa makosa kwa mtumishi kama posho ya kujikimu kwa Afisa kuhudhuria kozi fupi ya siku 21 huko Swaziland. Kambi ya Upinzani inasema malipo hayo ni sehemu tu ya mchezo unaoendelea kwa Wizara au Idara na taasisi zote za Serikali kupeleka watumishi nchini Swaziland kwa baraka za Idara Kuu ya Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama gharama kwa mtumishi mmoja kulingana na cheo chake na kozi anayoisoma ni kati ya *USD 5000-8000* kama *tuition fees*, posho ni kati ya *USD 350-500* kwa siku, usafiri wa kwenda na kurudi ni kati ya *USD 3000-4000*. Jumla ni takriban *USD 22,500* kwa kozi ya wiki tatu (siku 21). Hizi ni sawa na shilingi 29,250,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtumishi mmoja wa Serikali anaweza kulipiwa milioni hizo kwa muda wa siku 21, je, ni watumishi wangapi wa Serikali wamekwisha kwenda Swaziland? Je, fedha hizo zingeweza kuwalipia wanafunzi wangapi katika Vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaamini kabisa kuwa kama utaratibu mzuri ungefanywa kwa kushirikisha vyuo vyetu hapa nchini, kozi hizo za muda mfupi zingeweza kutolewa hapa nchini na watumishi wengi zaidi wangufaika na fedha nyingi zingeliweza kuokolewa kwa kazi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tathmini ya matumizi ya fedha ambazo zimekwishatumika katika kadhia hiyo ya kupeleka watumishi Swaziland na nje ya nchi katika kipindi cha mwaka 2008/2009 hadi Machi, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira na mishahara. Hali halisi ya uchumi wa nchi inaonyesha kupanda sana (mfumuko wa bei umekuwa mkubwa sana) na hivyo matumizi ya kawaida kwa mtumishi wa Serikali kuongezeka. Kupanda huko kwa gharama za maisha kunatakiwa kuongezeke na kipato cha mtumishi wa umma ili aweze kuondokana na kishawishi chochote cha kuharibu utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume cha hapo tunashuhudia watumishi wa umma wanapoteza muda mwingi kwenye shughuli za pembeni, kama kufuga kuku, ng'ombe au biashara ya *grocery* kwa lengo la kuwaongezea kipato ili kumudu hali halisi ya upandaji wa maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa mapato ya ndani, Kambi ya Upinzani imekuwa inashauri katika hotuba zake kuwa kiwango cha chini cha mishahara wa wafanyakazi wa umma kiwe kinaongezeka kutokana na hali halisi ya uchumi. Tumetoa hata mfano kama ule wa nchi za Ulaya zinazotumia mfumo wa *scala mobile*. Mwaka 2009 tulishauri kima cha chini kiwe Tshs 315,000/- kwa mwezi, kwa ngazi nyingine mishahara upande kwa asilimia ambayo italeta uwiano baina ya kipato cha chini na cha juu. Hii ni kwa mujibu wa bajeti mbadala ya fedha ya mwaka 2009/2010 kama ilivyowasilishwa na Waziri Kivuli wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali halisi ya sasa ni dhahiri kuwa kima cha chini kinatakiwa kipande hadi shilingi 350,000/-. Kiwango hiki hakitanzwa kodi ili kuweza kumfanya mtumishi wa ngazi ya chini aweze kumudu gharama za maisha, japo hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani mara zote mapendekezo yetu yanatokana na kuangalia hali halisi ya bidhaa na huduma zinazotumika kila siku katika maisha ya kawaida. Mfano, mchele kilo moja ni shilingi 1600; unga kilo moja shilingi 600; sukari kilo moja shilingi 2000; nyama kilo moja shilingi 4000; mafuta ya taa lita moja shilingi 1400; mkaa pishi moja shilingi 500; mchicha fungu moja shilingi 200; nazi moja shilingi 500 na mafuta ya kula chupa moja shilingi 1300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo bado nauli kwa usafiri wetu wa kila siku kwenda na kurudi, ikiwa una watoto wanaosoma shule inakubidi utumie zaidi ya shilingi 5000 kwa siku kwa usafiri wa mtumishi wa umma na watoto wake wawili au watatu wanaosoma shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kupima mishahara kwa kuangalia upandaji wa maisha ni vyema nikarejea ushauri uliotolewa katika hotuba yetu ya bajeti mbadala juu ya *Time Management* kwamba, Serikali ifanye utafiti ili kugundua muda ambao mtumishi anatumia kwa kufanya kazi na ule anaotumia kwa kutafuta huduma za kibenki, usafiri, hospitali na kadhalika, ni vyema Serikali ikaanzisha mfumo wa *two clock in and out*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi huu ni mojawapo ya kigezo cha Kambi ya Upinzani kuitaka Serikali kupandisha kima cha chini cha mishahara ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesema kuwa watumishi au wafanyakazi watapunguziwa asilimia moja katika kodi ya *PAYE* wanayolipa kila mwezi. Kwenye Vyombo vya Habari, Wafanyakazi wamedai kuwa makubaliano yalikuwa kupunguza asilimai mbili na siyo asilimia moja ambayo Serikali imepunguza. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu hivi makubaliano yalikuwa asilimia ngapi na kama ni kweli asilimia mbili ni kwa nini Serikali imefanya kinyume na makubaliano? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema kuwa mishahara ni maisha ya mtumishi huyo na familia yake. Hivyo basi, kucheza na mishahara wake ni kucheza na maisha yake. Hivyo basi, kwa kupunguza asilimia moja wakati wawekezaji katika sekta mbalimbali wanapata misamaha ya kodi na kupewa motisha za kila aina, hii ni sawa na kucheza na maisha ya wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni chanzo cha matatizo makubwa ya kuwafanya watumishi kugoma. Hii inatokana na ukweli kwamba watumishi wanapopandishwa madaraja ya kazi hawabadilishiwi viwango vya mishahara na marupurupu yao yanayoendana na kupandishwa madaraja, hili limekuwa ni tatizo sugu katika sekta ya utumishi wa umma. Watumishi katika idara kama Kilimo, Misitu na afya inawachukua muda mrefu kurekebishiwa mishahara yao mpaka wanakata tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mrundikano wa stahiki hizo za watumishi kwa sekta zote inafikia kiasi kwamba Serikali inashindwa kuwalipa kutokana na bajeti za kawaida za Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa mtumishi yeyote anapopewa nafasi ya kukaimu hawezi kutoa maamuzi mazito ya kiutendaji kwa asasi aliyomo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze watumishi wa umma ni muda au kipindi gani ambacho mtendaji anatakiwa kukaimu nafasi ya uongozi kabla ya kuthibishwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri na ukweli kwamba kuna wakala kadhaa na taasisi za umma ambazo watendaji wake wakuu kwa muda wa zaidi ya miaka minne wanakaimu tu bila ya kuthibitishwa(*confirmed*) kwa nafasi zao, il-hali utendaji wa taasisi au wakala zao ni mzuri sana kwa mujibu wa Kamati za Kudumu za Bunge wanaopata taarifa za utendaji kwa taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, aligundua udanganyifu mkubwa wa shilingi 13,299,400/= alizolipwa mtumishi wa ofisi yako anayeishi katika nyumba ya Serikali kama posho ya nyumba. Aidha, shilingi 282,453,350/= zilitumika kama gharama za hoteli wakati walikwishapewa posho za kujikimu. Kambi ya Upinzani inauliza kama hili linatokea katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ofisi tunayoamini kuwa ndio kiwe kioo au mfano kwa Wizara nyingine. Je, katika maeneo mengine si hali ni mbaya zaidi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya Mfumo wa Utumishi wa Umma. Serikali imetoa Baraka zake kwa taasisi ya umma kutoa nafasi kwa watumishi wake kuingia katika ajira ya mikataba, ambapo mtumishi anakuwa na hiari ya kuendelea kuwa na *pension* au kupata kiinua mgongo chake baada ya Mkataba wake kama ilivyo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi hilo kumetokea ubadhirifu mkubwa ambao si rahisi kwa hali ya kawaida kuamini kuwa unafanyika. Katika zoezi hilo linaloendelea kwa asasi na taasisi za Serikali, viongozi wa asasi hizo (ngazi ya Umeneja na Ukurugenzi) wamekuwa wakijilipa kiinua mgongo kila baada ya miaka mitatu na kujilipa mishahara ya miezi sita na kuingia tena mkataba kwa miaka mingine na wakati huo huo mashirika husika yanawalipia michango ya pensheni katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu unaendelea kutumika licha ya kuwepo kwa Waraka wa Serikali wa tarehe 1 Desemba 2009 uliosainiwa na Katibu Mkuu wa Utumishi, Bwana George D. Yambesi ambao unatamka bayana kwamba watumishi watakoajiriwa na Wakala wa Serikali na taasisi nyingine za Umma kuchagua kimojawapo kati ya Masharti na Mkataba na Masharti ya Kudumu. Serikali inatoa kauli gani kwa Taasisi zinazofanya utaratibu huo ambao ni kinyume na Sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa hilo ni kwa watumishi 12 wa Mamlaka ya Bandari, ambapo mtu mmoja kwa miaka mitatu analipwa shilingi 76,789,544.40/= kama kiinua mgongo na mishahara wa miezi sita shilingi 42,660,858.0/=. Hii sijui tunaweza kuifanisha na nini katika hali ya kawaida, Jumla fedha kwa watumishi 12 walijipa Shilingi 1,224,308,836.80/=. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina. Hili linafanyika wakati Serikali inakataa katakata kupandisha kima cha mishahara na hasa ya watumishi wa ngazi ya kati na chini.

Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa fedha hizi kama kweli Ofisi ya Utumishi wa Umma ingekuwa makini na kazi zake kusingetokea matumizi ya aina hiyo. Vinginevyo inatufanya tuamini kuwa matumizi hayo yanakuwa na baraka zote toka Ofisi

hii ya Rais. Huu ni mfano mmoja tu, je ni fedha kiasi gani zimepotea kwa njia hii kwa taasisi zingine za Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tathmini ya watumishi wangapi kwa taasisi zote wako kwenye mpango huo wa kubadilisha mikataba yao ya kazi? Pia ni kiasi gani cha fedha kimelipwa mwisho wa mikataba ya utumishi wao katika miaka minne iliyopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais - Utawala Bora. Taarifa zinaeleza kuwa moja ya mafanikio ni kwamba Serikali imeendelea kutoa huduma kwa Mheshimiwa Rais na familia yake. Kambi ya Upinzani haina pingamizi na hilo, lakini inaomba kupatiwa ufafanuzi kuhusu hizi taasisi ambazo zinaanzishwa na wake wa Marais zina uhusiano gani na Ikulu kama Taasisi ya Umma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imeona ipate ufafanuzi huo kwa kuwa akinamama hao kabla ya kuingia Ikulu wanakuwa hawana hizo *NGOs*, tukumbuke kuwa misaada yote ya hali na mali kwa *NGOs* hizo inapatikana kwa kutumia nafasi za waume zao (Marais). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu ni kwamba katika utendaji kazi wa *NGOs* hizo vitendea kazi vya Serikali ndivyo vinavyotumika, hivyo basi, suala hili linatofauti gani na Rais kufanya biashara akiwa Ikulu? Kwani *NGOs* hizo zinatoa ajira kwa watu, lakini ni nani anakagua mahesabu yake? Hii ni sawa na Kampuni binafsi ya mtu. Huu si ni uvunjifu wa maadili ya Viongozi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ingependa kuelewa nafasi ya Mke wa Rais kikatiba, kwani umetokea mtindo pindi Mke wa Rais anapofanya ziara zake mikoani anasomewa taarifa za utendaji kazi katika Wilaya husika. Hii maana yake ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hiyo inapata nguvu kutokana na ongezeko la shilingi 14,354,549,000/= mwaka 2010/2011 kwenye ofisi ya Rais, Idara ya Utawala kwa kulinganisha na mwaka 2009/2010 ambapo mwaka 2009/2010 bajeti ya utawala kwenye matumizi mengine ilikuwa ni shilingi 153,597,461,100/=, mwaka huu wa bajeti fungu hilo limekuwa ni shilingi 166,952,010,100/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kama hali halisi iko hivyo na Watanzania wameridhika, ni bora nafasi ya Mke wa Rais itamkwe katika Katiba na majukumu yake yaainishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Mfuko huu dhana yake kubwa ni kuwasaidia wananchi kuondokana na umaskini, lakini kwa hali halisi unawazidishia umaskini kwa kuwa unatoza riba ya 2.5% kwa mwezi, kwa mwaka ni 30%. Riba hii ni zaidi ya karibu mara mbili ya 15.2% inayotozwa na mabanki ya biashara, huu ni wizi wa mchana kutwa (*day light robbery*). Kambi ya Upinzani inauliza

kweli Serikali na Rais wana dhamira ya kweli kuwasaidia wananchi kuondokana na umaskini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU. Wakati Waziri akiwasilisha hotuba yake ya bajeti kwenye Bunge hili mwaka jana alisema, nanukuu: “Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2008/2009 na kazi zitakazotekelezwa katika mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

(i) Upelelezi wa tuhuma 706 za malalamiko ya vitendo vya rushwa ulikamilika na kiasi cha Shilingi 13,312,865,997 kiliokolewa kutokana na chunguzi hizo. Aidha, jumla ya kesi 305 zinaendelea kusikilizwa Mahakamani.

(ii) Katika mwaka 2009/2010, TAKUKURU itaendelea na uchunguzi wa tuhuma 2,288 zilizopo na zitakazowasilishwa. Kipaumbele kitawekwa katika tuhuma kubwa za rushwa kama vile mikataba mikubwa, ununuzi Serikalini, matumizi ya fedha za Serikali katika miradi mikubwa pamoja na tuhuma nyingine zitakazoonekana kuisababishia Serikali hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inahoji ni kwa nini mpaka sasa zile kesi kubwa alizoahidi Waziri kuwa zingefikishwa Mahakamani na ambazo ziliingizia Taifa hasara kama Radi ambayo uchunguzi wa nje umekamilika, eti wa ndani hadi leo haujakamilika, tueleweje wakati Serikali imetuma hata ujumbe kudai *change* ya shilingi 29 bilioni Uingereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu na taasisi hii inapaswa kufanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kuwa hakuna rushwa kwenye zoezi zima la uchaguzi na pia wanasisia wanazingatia sheria na kanuni na haswa sheria ya gharama za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inatenga kiasi cha fedha cha kutosha kwa ajili ya kuhakikisha kuwa majukumu ya taasisi hii na haswa katika kipindi cha uchaguzi mkuu yanafanyika na kuwezesha kufanyika kwa uchaguzi mkuu ambao hautakuwa na rushwa wala ufidadi, ila na wao wajue sio malaika, hivyo wasijingize katika upendeleo wa aina yeyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Grace S. Kiwelu kwa maoni hayo ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa wabunge, sasa tunaendelea na taratibu za leo lakini kabla ya matangazo kuna maoni nilipata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambayo Ofisi ya Katibu ni vizuri ikayafanyia kazi.

Moja ni kuhakikisha kwamba *CRDB* katika maeneo yetu ya Bunge inafanya kazi siku za Jumamosi ili kuwapunguzia Wabunge adha ya kwenda mjini na kama tunavyojua katika Mkutano huu wa Ishirini Jumamosi ni siku ya kazi kama kawaida. Tunawapongeza *NMB* kwa kuendelea kufanya kazi Jumamosi bila matatizo. (*Makofi*)

La pili ni kwamba kuna malalamiko kidogo kuhusiana na kuwepo kwa Mbu kwenye jengo na hasa Waheshimiwa akinamama wamenipa *option* mbili tu kwamba ama jengo lifanyiwe *fumigation* haraka au la sivyo basi viletwe vyandarua vya miguu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao hapa ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora Mheshimiwa Sophia Simba ambao ni Ndugu Adrian Kitwana Kondo mtoto wake, na wa pili ni Mwinjuma Abdulaziz ni mtoto wake pia. Karibuni sana vijana wetu kwani Mama anafanya kazi nzuri hapa Bungeni. Wako pia wageni wake ambao ni viongozi wa *TANU* kutoka Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zilizo chini yake ambao ni pamoja na Ndugu Michael Mwanda, Katibu Mkuu Ikulu. Karibu sana Ndugu Mwanda.

Mheshimiwa Jaji Mstaafu Stephen Ihema Kamishna wa Maadili; yuko pia Eng. T. Salema ambaye ni Mratibu wa *MKURABITA*, yuko na Ndugu M. Likwelile, Mtendaji Mkuu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Lakini pia yuko mgeni maarufu Mheshimiwa Dr. Edward Hossea, Mkurugenzi Mkuu wa *TAKUKURU*. Waheshimiwa Wabunge, hatumpigii makofi hata Mheshimiwa Hossea? Karibu sana Ndugu Hossea, mtani wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Hossea hajaja hivi hivi tu, bali amekuja na kitabu ambacho kitagawiwa kwa kila Mheshimiwa Mbunge kinachozungumzia habari za Sheria zinazozuia na kupambana na rushwa wakati wa uchaguzi. Inahimizwa kila Mheshimiwa Mbunge ahakikishe anapata nakala ambazo zimeletwa na Mheshimiwa Waziri Sophia Simba ndani ya ukumbi huu. (*Makofi*)

Vilevile kuna wageni wafuatao ambao pia nao wanatoka Ikulu nao ni Bwana Shaaban Gulumo, Bwana Mangira ambaye ni Mratibu Ikulu; Ndugu Mayaya ambaye ni Mratibu wa Utawala Bora Ikulu; Brig. Gen. Nicholous Mitti Mratibu Mkuu wa Baraza la Usalama wa Taifa; Bwana Mandara ambaye ni Katibu wa Sekretarieti ya Maadili na pia Bwana Ladislous Mwananga, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *TASAF*. Karibuni sana. (*Makofi*)

Kuna pia wageni wa Mheshimiwa Hawa Ghasia Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambao ni Ndugu Bibie Ghasia mdogo wake; pia ndugu Hussein Mhata ambaye ni mtoto wake wa kwanza, lakini pia Mheshimiwa Ghasia amefuata maelekezo ya Mheshimiwa Spika kwa kumleta Amina Diwani Msangi, wifii yake, maana Mheshimiwa Spika wiki hii aliuliza Mawifi vipi? Karibuni sana wageni. (*Makofi*)

Pia tuna Viongozi nane ambao ni Wakuu wa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango wamekuja kusikiliza hotuba ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Rais, Utawala Bora ambao ni pamoja na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma Ndugu George Yambesi, karibu sana Katibu Mkuu. (Makofi)

Pia Katibu Mkuu wa Sekretariaeti ya Ajira Ndugu Xavier Daud, Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Rais Tume ya Mipango; Dr. Phillip Isidor Mpango, Naibu Katibu Mtendaji anayeshughulikia Klasta ya Sekta za Uzalishaji Ndugu Maduka Paul Kessy, Naibu Katibu Mtendaji anayeshughulikia *cluster* ya Miundombinu na Huduma; Eng. Happines Ngoti Mgalula, Naibu Katibu Mtendaji anayeshughulikia *cluster* ya Huduma za Jamii na Maendeleo ya Raslimali watu; Ndugu Florence Mwanri, sasa haya majina yamefanana na Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri lakini tukipata ufafanuzi tutafafanua baadaye. (Makofi)

Pia yuko Naibu Katibu Mtendaji anayeshughulikia *cluster* ya Kimataifa na Mahusiano ya Kiuchumi, Ndugu Cliphod Katondo Tandari na mwisho ni Kaimu Naibu Mtendaji anayeshughulikia *cluster* ya Uchumi Jumla, Ndugu Grace Mosha. Karibuni na ahsanteni sana. (Makofi)

Vilevile wako wageni wa Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni wanafunzi wa *UDOM* kutoka Nachingwea, nao ni Ndugu Fikirini Hamis, Ndugu Shaibu Sudi, Ndugu Oigen Mruneni na Ndugu Salum Nyambi. Karibuni sana wanafunzi wa *UDOM*.

Yupo pia Ndugu Salvatory Mabada ambaye ni Mratibu Kata ya Makulu amekuja kwa ajili ya kusikiliza hotuba inayoendelea ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Pia kuna wageni wa Kanisa la Moravian ambao sidhani kama wapo labda kama watakuwa *basement* tunawakaribisha nao, wanaongozwa na Mchungaji Essau Kalinga. Tunawakaribisha sana.

Baada ya matangazo hayo, liko tangazo moja tu la kazi ambapo Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Nishati na Madini, kwamba leo baada ya Mkutano huu kumalizika kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachoanza baada tu ya Mkutano huu katika ukumbi namba 231, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na uchangiaji na orodha niliyonayo ni wachangiaji wawili na orodha imekwishafungwa. Kwa hiyo, mchangiaji wa kwanza ni Mheshimiwa Halima J. Mdee na mchangiaji wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya. Mheshimiwa Mdee karibu!



**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini je itakuwa ni dakika kumi na tano au thelathini?

**MWENYEKITI:** Dakika ni kumi zile zile!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa hiyo mimi nitachangia kwa uchache hasa nikisisitiza.....

**MWENYEKITI:** Kwa kuwa mko wawili basi mmepewa dakika kumi na tano kila mmoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Lakini nitazungumza kwa uchache hasa kusisitiza yale ambayo yamezungumzwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niseme kwamba katika suala la kwanza ambalo nitalizungumza nina *interest* kwa namna moja au nyingine kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *POAC* ambayo inashughulika na kusimamia Hesabu za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya matatizo makubwa ambayo tumeyaona kwenye Kamati hasa kuhusiana na suala zima la ajira za kudumu *versus* ajira za mkataba. Naomba suala hili pia na Waziri Mkuu akiwa kama ndiye msimamizi wa kazi za Serikali alifuatilie kwa umakini sana kwa sababu tumejikuta kwamba mashirika na taasisi mbalimbali za Serikali mengi ambayo yanatengeneza fedha yanatumia hiyo *advantage* ya kutengeneza fedha nyingi kujinufaisha wao zaidi kuliko kuangalia ni kwa namna gani watanufaisha nchi kwa ujumla. Wakati Msemaji wa Kambi ya Upinzani akizungumza, amezungumzia kwa kina sana kuhusiana na hizi ajira za aina mbili yaani ajira za kudumu na ajira za mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika miaka ya karibuni ilianzisha mfumo mpya wa ajira za mikataba na lengo kubwa ambalo naliona dhamira ilikuwa ni nzuri, ilikuwa ni kuhakikisha kwamba watu wanakuwa na makubaliano na Serikali ama Mashirika ya Umma kufanya kazi kwa kipindi cha muda fulani ili baadaye sasa waweze kufanyiwa tathmini kutokana na utendaji wao wa kazi ili mwisho wa siku mwajiri aamue kama aendelee na mkataba.....

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba unilinde wananisumbua.

**MWENYEKITI:** Endelea mimi nakulinda.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwenyekiti wanani-*distort*, naomba wakae kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huo ulikuwa ni mzuri kwa sababu utakuwa unapima utendaji wa watumishi wetu. Sasa kinachojitokeza ni kwamba mashirika yetu

ambayo yameamua kutumia huu mfumo wa mkataba wanaamua kuutumia vibaya kwa maslahi ya mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Serikali uko wazi kabisa na nichukue fursa hii kupongeza juhudi za kutengeneza waraka kwa madhumuni ya kupeleka kwenye haya mashirika, lakini kibaya umekuwa hauzingatiwi na haya mashirika. Nalizungumza hili kwa sababu kabla Bunge halijaanza tumekutana na mashirika mbalimbali, mkiwaambia huu utaratibu hawaufahamu na matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba watu wanapata faida mara mbili kwa sababu mtu anaingia kwenye mkataba lakini vilevile anaendelea kuchangiwa kwenye Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii kitu ambacho ni kinyume na Sheria na utaratibu. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake ni kwamba fedha nyingi sana zinapotea kwa kwenda kwenye mifuko ya watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzaji amezungumzia hapa na kwamba CAG anazungumza sana haya mambo na ndiyo maana tunawashauri ndugu zetu Serikalini kwamba tuwe tunasoma hizi taarifa za Mkaguzi Mkuu, kuna vitu vingine tunavizungumza hapa vinaweza vikaonekana ni vipya lakini siyo vipya vipo kwenye taarifa zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mkaguzi amefanya utafiti Bandari peke yake, Bandari wamewaingiza hawa watu ambao wako kwenye *Managerial position 45* kwenye huu utaratibu wa mkataba. CAG amefanyia utafiti wafanyakazi ama watumishi wenye *Managerial position* kumi na mbili tu kutoka kwenye *port* ya Dar es Salaam. Katika hawa wafanyakazi kumi na mbili katika kipindi cha miaka mitatu mitatu waliyojitengea wamevuna kiasi cha shilingi bilioni 1.2, wafanyakazi kumi na mbili ndani ya kipindi cha miaka mitatu unakuta mfanyakazi mmoja, maana sisi Wabunge na kale kakiinua mgongo ketu ilipigwa kelele kweli ndani ya miaka mitano. Lakini huyu mfanyakazi wa Bandari ndani ya miaka mitatu amelipwa shilingi milioni 76, mtu mmoja, kila baada ya miaka mitatu ana-renew na anakuwa amepata milioni 76 kwa kila mwaka, sasa hadi astaafu sijui atakuwa ameshavuna shilingi ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza unakuta pia eti kwa kuwa hana mkataba wa kudumu kuna kitu kinaitwa fidia ya mshahara wa miezi sita yaani milioni 42. Kwa hiyo, unakuta mtu mmoja kafanya kazi miaka mitatu lakini analipwa milioni zaidi ya 100, haya ni matumizi mabovu ya fedha. Lakini kibaya zaidi baada ya kuchukua hili fungu lote bado analipiwa *pension*, mwajiri anamchangia na yeye anachangia kitu ambacho ni kinyume na taratibu. Sasa ukiangalia hesabu za wafanyakazi 45 tu hawa wa Bandari ambao wako kwenye *Managerial position* unakuta ndani ya vipindi vya miaka mitatu karibia bilioni tano inafika kulipa wafanyakazi 45, lakini bajeti ya kilimo bilioni tatu ndani, hakuna uhusiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri viongozi tujaribu kutumia raslimali zetu za ndani, mashirika yetu yanatengeneza fedha sana, tujaribu kuyasimamia. Mashirika yetu ya Umma yanaendeshwa kama taasisi za watu binafsi wakati sisi tunaendelea kuwa omba omba kumbe tungeweza tukatengeneza fedha za kutosha ndani

na kuacha kuwa watumwa wa nchi za nje. Kwa hiyo, naomba Waziri haya masuala myafuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kine ni kwamba kama tumeamua kuingia kwenye mkataba lazima kuwe na mfumo mmoja unaoeleweka, lazima kuwe na *harmonisation* ya hii mifumo ya kimikataba, haiwezekani leo *PPF* inajiamulia kivyake, *TPA* inajiamulia kivyake na *PSPF* inajiamulia kivyake. Kama tumeamua mikataba inakuwa *renewed* baada ya miaka mitano basi iwe miaka mitano kwa watu wote na kama ni 25% ya mishahara baada ya miaka mitano iwe 25% ya mishahara kwa wote na kama ni 10% basi iwe kwa wote lakini siyo kila shirika linajiamulia kivyake, matokeo yake mashirika yetu yanakuwa hayawanufaishi Watanzania. Kwa hiyo, tupanue wigo wa mapato kama ambavyo tumekuwa tukiwashauri kila siku, wigo wa mapato uko ndani ya uwezo wetu, tutekeleze wajibu wetu tuache kungea siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nitazungumzia suala la TAKUKURU *versus* migogoro ya ardhi. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuweza kufanya kile ambacho Waziri mwenye dhamana husika alishindwa kukifaya miaka miwili iliyopita, Waziri ambaye pia ni Katibu Mwenezi wa CCM. Suala la migogoro ya ardhi, Dar es Salaam nililizungumzia kwa uchungu sana miaka mitatu iliyopita, nikatoa ushahidi kuonyesha ni wanasiasa wa aina gani na kwa majina wanaoshiriki kuuza maeneo ya wazi Dar es Salaam, Mheshimiwa akaweka *report* yake pale akaunda *team* yake ambayo iliwajumuisha walewale wezi waka-clear. Lakini nashukuru Bunge lilifanya kazi yake vizuri na kutoa taarifa ambayo iliendana na yale niliyoyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha baadhi ya watu ambao niliwatuhumu miaka mitatu na Bunge likathibitisha, majalada yao yako TAKUKURU, yako TAKUKURU kwa muda wote huo, wanasiasa ambao ndiyo viongozi, tutakamata Watendaji hawa lakini msingi wa wizi wa uuzaji wa viwanja vya Umma Dar es Salaam ni wanasiasa. Kwa hiyo, tusipowakamata wale wanasiasa watendaji hawa tutakuwa tunawaonea bure. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kama Londa!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Londa umemsema wewe mimi sijamsema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri TAKUKURU kama hii dhamira wanayo kweli na naamini wataitekeleza kama wakiamua kufanya kama ambavyo walivalia njuga lile suala la vile viposho vya Wabunge. Kwa hiyo, wakikomalie hili ili wananchi maskini kule ambao ardhi zao zimechukuliwa ambao wameshindwa kujenga shule na Zahanati kwa sababu tu ya wanasiasa wachache ambao miaka kumi iliyopita walikuwa maskini hata shilingi 5000 walikuwa hawana lakini leo ukienda ni mabilionea kwa sababu ya kuuza viwanja vya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Wiliam V. Lukuvi na nilimpigia simu nikamuahidi kwamba, nitakupa *support* na ukitaka majina kwa ushahidi

nitakupa, sasa isije ikawa ni nguvu ya soda kwa sababu huu ni mwaka wa uchaguzi.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Watumishi wa Umma ambao Serikali inagharamia kuwasomesha lakini wanachukuliwa na shule binafsi. Msemaji wa Kambi ya Upinzani amelizungumza. Hili ni tatizo kubwa sana na ni tatizo ambalo CAG amekuwa akilizungumza miaka nenda rudi. Kumekuwa na tatizo Serikali inatumia gharama kubwa kuwasomesha watumishi na Watanzania kwa ujumla lakini kutokana na kwamba malipo yetu ni madogo na sijamsikia leo Mheshimiwa Ghasia akizungumzia mishahara kwa mapana labda ni siri. Kwa kuwa, malipo yetu kwa watumishi ni madogo, matokeo yake ni kwamba hawa watoto ama vijana tunaowasomesha wanakwenda kwenye shule binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani kuna haja ya Serikali kuwa wakali kidogo, tusibakie kuwa *loose* tu, lazima yaingiwe makubaliano mahsusi baina ya Serikali na hizi shule binafsi ambazo wao hawasomeshi watumishi wanasubiri Serikali inawasomesha halafu wao wanakuja kuwadaka na kuwatumia, matokeo yake ndiyo kama taarifa zenu zinavyoonesha hapa Mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 355, wakati kiutaratibu inatakiwa iwe Mwalimu mmoja afundishe wanafunzi 55. Kwangu nadhani Serikali kuna haja ya kuwa wakali katika hili, uwezo mnao na meno mnayo au labda mtuambie hizi shule pia na ninyi ambao ni watu wa maamuzi mna hisa nazo, kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu watoto wetu ambao ni maskini ambao wanatakiwa wafaidike kutokana na walimu ama wataalam mbalimbali ambao wanasomesha na fedha zao za kodi wanashindwa kufaidi matokeo yake ni kile kikundi cha watu wachache kwenye shule binafsi wenye fedha ndiyo wanajikuta wanafaidi matunda hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali tufanye hivyo, tuingie makubaliano na hizi shule binafsi tena kwa lazima siyo hiari kwa sababu wanatumia walimu au wataalam mbalimbali ambao wamesomesha kwa madhumuni ya kuwafaidisha Watanzania wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Wataalam wake kwa kuweza kuandaa hotuba hii na kuileta hapa ili tuweze kuijadili. Pia niipongeze sana hotuba ya Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambayo kwa kina imeeleza mambo mengi ya msingi, ikiwa Serikali itayachukulia maanani na kuyafanyia kazi itaweza kuboresha huduma kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Lipo tatizo kubwa ambalo linatia mashaka kwamba kila mwaka kwenye taarifa ya CAG tunaona Serikali inatoa mishahara kwa watumishi hewa, ni jambo la kusikitisha. Ukiangalia taarifa ya CAG ya mwaka uliopita 2008/2009, karibu Halmashauri nyingi kuna fedha nyingi sana ambazo zimetengwa, zimetoka Hazina zimekwenda kwenye Halmashauri kwa watumishi hewa.

Kwanza hii ni aibu kwa Taifa kwa sababu inamaanisha nini, inamaanisha Serikali haina takwimu sahihi za watumishi gani walioko kazini, watumishi gani waliohamishwa, watumishi gani waliostaafu na watumishi gani waliokufa. Hii pia inatupa wasiwasi kwamba kuna *linkage*, kuna kitu kinachofanyika kwa watumishi wa Halmashauri na Serikali Kuu kwamba hizi fedha zikija zinaingia kwenye mifuko ya watu binafsi. Kwa hiyo, hii ni aibu, kwanza, ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi na pia hizo fedha ambazo zinakwenda zinakaa *pending*, hazina kazi zingejajiri watumishi sehemu ambapo tuna matatizo makubwa ya watumishi. Kwenye Halmashauri, tuna matatizo makubwa ya Watumishi wa Ugani, Watumishi wa Afya, Watumishi wa Kilimo na watumishi wengine. Lakini kusikia kwamba kuna mishahara hewa, inasikitisha, tunaomba Serikali isome taarifa za CAG na izifanyie kazi, hii ni aibu sana kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ni Serikali kuhamisha watumishi wanaonekana wamekiuka maadili ya kazi zao, pale anapoonekana mtumishi amekiuka maadili anahamishwa kwenye kituo kimoja kwenda kwenye kituo kingine cha kazi. Suala hili limekuwepo, tunalizungumza hapa Bungeni kila siku lakini bado kwa sababu sisi tuko vijijini, tuko na wananchi, tunashuhudia bado yanafanyika. Inakuwaje Mtumishi wa Umma anayelipwa fedha za walipa kodi, anafanya ubadhirifu tena mkubwa kabisa. Uchunguzi unafanyika na inaonekana kabisa kweli amehusika kwa asilimia mia moja kwamba amefanya ubadhirifu, lakini Serikali inamhamisha kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Kwa hiyo, utaratibu huu unalea uzembe makazini, unalea viongozi wabovu, unalea watendaji wasiokuwa waadilifu. Tunaomba sana Serikali ifanye kazi yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo, kwanza nishukuru sana kwamba Hospitali ya Mwananyamala ambavyo ilikuwa imekithiri watumishi wasiokuwa waadilifu, wanaotukana kinamama wajawazito, wanaofanya mambo yasiyokubalika, Serikali imewahamisha. Lakini kitendo cha kuwahamisha kutoka Mwananyamala kuwapeleka hospitali nyingine, kwa kweli naona sio hekima, kwa sababu waliyokuwa wanayafanya Hospitali ya Mwananyamala wanayapeleka hospitali nyingine. Ina maana tunahamisha tatizo *from one area* kwenda kwenye eneo lingine. Tunamsaidiaje Mtanzania kwa kufanya hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Serikali ituambie kwamba uhamisho ni adhabu. Mimi sidhani kama uhamisho ni adhabu. Uhamisho ni utaratibu unaotumiwa na Serikali kumtoa mtumishi kwenye kituo kimoja kwenda kituo kingine. Pale inapokuwa aidha ameiba, amefanya ubadhirifu, ameshindwa kufanya kazi, tumweke chini, tuweke watumishi wengine waadilifu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la watumishi ambao wanajiendeleza kimasomo wakiwa makazini. Wapo wanaojiendeleza kwa fedha zao wenyewe taratibu na wapo ambao wanaojiendeleza kwa kutumia fedha za Serikali kwa maana kwamba Serikali inawalipia masomo yao. Lakini yapo malalamiko mengi sana ya watumishi ambao baada ya kujiendeleza, kwa mfano, Mwalimu wa Shule ya Msingi, mtu anajiendeleza kidogo kidogo mpaka anapata Digrii ya Kwanza na wengine wanakwenda mpaka Digrii ya Pili, cha kusikitisha, wakirudi kwenye vituo vyao vya kazi wanabaki pale pale walipo, hawatambuliki kwa maana ya kuwa *recognised* wala hawapandishwi vyeo kwa maana hiyo hata mishahara yao haipandi. Kwa kweli, suala hili linakatisha tamaa sana. Tunaomba Wizara ijaribu kuangalia na kuwa na takwimu sahihi, watumishi wanavyokwenda kujiendeleza kwanza ni kwa ajili ya kuongeza ujuzi, pili ni kwa ajili ya kuongeza tija kwenye kazi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Pale unapomuacha kwenye kituo kimoja bila ya mishahara kupanda, bila kuwa *recognised*, bila chochote inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wapo watumishi ambao wanakaa miaka mitano na wengine miaka saba pale pale akiwa Mwalimu wa Msingi, matokeo yake anaona hana haja kwa sababu inaonekana elimu yake haijasaidia anaamua kuhama kwenye fani kabisa, anaondoka pale anakwenda kufanya kazi kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, tunapoteza watumishi kwenye sekta muhimu kama sekta za afya, elimu kwa sababu ya kutokuwatambua tu. Naomba hili lifanyiwe kazi na Serikali kwa sababu ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine mishahara kwa watumishi wa Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali. Ni lazima Serikali ikubali kwamba Watanzania wengi sana wameajiriwa kwenye sekta binafsi. Serikali haina uwezo wa kuwa-*accommodate* na kuwachukua watumishi wote wa Tanzania ambao wana elimu kwa sekta mbalimbali na kuwaajiri kwa sababu uwezo wa Serikali wa kuwaajiri ni mdogo, wengi wako kwenye sekta binafsi na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali. Inasikitisha pale ambapo Serikali inatamka kima cha chini cha mishahara kwa Serikali, kingekwenda moja kwa moja kwa sekta binafsi na pia kwenye Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali kwa sababu ni wengi walioajiriwa huko. Lakini cha kusikitisha, Serikali inatamka kima cha chini cha mishahara, sekta binafsi na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali wanaendelea kulipa mishahara wanayoipenda wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hapa, Serikali imetamka kima cha chini, mwaka huu hatujakisikia, tuna imani kwamba tutakijua, imetamka ni shilingi 104,000/= lakini mpaka ninapoongea sasa hivi wapo watumishi wa viwanda wanaopewa shilingi 65,000/= kwa mwezi. Shilingi 65,000/= kwa mwezi, jamani kila mmoja ajifikirie kwa siku 30, mtu huyu ana watoto, anahitaji waende shule, anahitaji awahudumie kiafya, amepanga nyumba, analipa kodi ya nyumba, analipa maji, umeme, ataishi vipi? Kweli hapa tunaweza kuondoa umaskini kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali, inapotoa maamuzi, iwe inatoa kwa Watanzania wote sio kundi moja la watu fulani. Tunaomba ihakikishe kwamba sekta binafsi inalipa mishahara ambao Serikali inasema vinginevyo Watanzania wengi

wataendelea kuwa maskini kwa sababu kipato wanachokipata kutoka kwenye sekta binafsi kwa baadhi yao hakiwasaidii chochote. Mtu anafanya *shuttling*, fedha yote inaishia kwenye nauli ya basi tu, hawezi kujenga milele, ataendelea kubaki kwenye nyumba za kupanga na waliokuwepo vijijini wataendelea kubaki kwenye nyumba ambazo sio nyumba bora milele na hapo hapo wanashindwa kusomesha watoto wao, huduma za afya wanashindwa kuzigharamia na mambo ya msingi yote yanakuwa ni magumu kwa sababu tu Serikali haijaweza kutupa jicho lake kikamilifu kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wanalipwa mshahara ambao Serikali imetamka hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kuniokolea muda. Nilipata ushauri hapa kwamba ni vizuri na Kambi ya Chama Tawala ikapata angalau kidogo mchangiaji. Lakini tutarudi kwenye dakika 10, 10 kwa sababu ya muda, kwa hiyo, Mheshimiwa Mchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Shibuda, Mheshimiwa Mchemba endelea kujiandaa kwanza.

Niwakumbushe tu Waheshimiwa kwamba wakati wa mchango jana na juzi kulikuwa na vibwagizo vikubwa vilitoka katika Wilaya ya Kilwa kuliko mahali popote pengine. Cha kwanza kilitoka kwa Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum Kilwa (CUF). Yeye anasema, “Ukiona paka analia ujue amekanyagwa mkia”. Akafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kusini, yeye akasema hao “Mavuvuzela”. Akafuatia Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, akasema hao “wapumbavu”. (*Makofi/Kicheko*)

Nashukuru, tunaendelea na mjadala.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi angalau na mimi leo nichangie kidogo kwenye hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Rais Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, dada yangu, mdogo wangu, Mama Hawa Ghasia, Mheshimiwa Mwenyekiti wangu, Mama Sophia Simba, wataalamu wote wa Idara hizi na Ofisi hizi, kwa kazi nzuri waliyoifanya na hotuba nzuri waliyoiwasilisha. Kwa kweli, hotuba hii imegusa maeneo mengi lakini pia pamoja na hotuba hizi ni kwamba kazi nzuri wamefanya na inaonekana. Ukienda upande wa rushwa, kazi wamefanya, ukienda upande wa Utumishi, wamejitahidi, niwape hongera na pongezi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchangia kwangu ni kudogo sana, ni kuhusu Chuo cha Uhazili Tabora. Chuo hiki sasa hivi kinachukua idadi ya watumishi wengi sana ambapo kimeunganishwa pamoja na kile Chuo cha Magogoni ambako walikuwa wanachukua wanafunzi wa aina mbili. Lakini sasa hivi ongezeko la wale watumishi waliopo pale na mabweni yaliyopo hayatoshi. Kwanza niipongeze Serikali kwa ukarabati

inaoufanya sasa hivi, lakini kumekuwa na tatizo kubwa la hawa wafanyakazi kukosa mahali pa kuishi, wanapanga mitaani kiasi kwamba hawawezi kabisa kumudu masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie ukarabati wa ukumbi. Tabora nzima inatumia ukumbi wa Uhazili, ndio mkubwa sana. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri katika ukarabati huo auangalie na aupe kipaumbele ukumbi wa Uhazili, tuna matatizo makubwa sana. Fedha zitengwe za kutosha ili wananchi wote waweze kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukarabati wa mabweni ambao unafanyika sasa hivi, unasuasua. Fedha inayotengwa, ni kidogo sana ingawaje ni sungura mdogo lakini kwa kweli ningeomba waangaliwe upya kwa sababu hali ya pale sio nzuri, ukarabati wake hauridhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ongezeko la madarasa. Sasa hivi wanasoma kwa zamu muda mrefu mno kiasi ambacho masomo mengine au wanafunzi mahali pengine pa kujisomea wanakuwa hawana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika bajeti yake pia auangalie jinsi gani ya kuweza kuongeza angalau madarasa kwa sababu yale madarasa ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba usafiri uwepo wa uhakika, kwa sababu usafiri uliopo sasa hivi hautoshi. Kuna matatizo mengi ambayo yanaweza kujitokeza, lakini pia waongezewe *matron* wa kutosha, *matron* waliopo sasa hivi hawatoshi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie taaluma ya Makatibu Muhtasi, hawa Masektretari ambao tunao sasa hivi maofisini wamesahaulika, wanafanya kazi ngumu sana, wanafanya kazi ambazo ni siri kubwa sana za Serikali, wanafanya mambo ambayo kwa kweli hawa wakitaka kupindua nchi au kuisaliti nchi, wanaweza na ndio maana uvujaji wa siri unatokea sana kwa sababu hiyo. Ninaomba wapewe motisha kwa masaa wanayofanya lakini pia waangaliwe upya jinsi gani watakavyoweza kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Sheria ya Kuajiri Watumishi, hawa Makatibu Muhtasi. Sheria hiyo imepitwa na wakati. Sasa hivi Mheshimiwa Waziri, tuna tatizo kubwa, kumshaingia utandawazi, hasa kama utandawazi wa sayansi na teknolojia sasa hivi ajira ya zamani walikuwa wanaajiriwa watumishi hawa kwamba lazima ajue hatimkato (*shorthands*) lakini sasa hivi inabidi wajue kompyuta. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ilete Sheria mpya au kubadilisha Sheria ya Ajira wanapoingia kwenye usaili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ningeomba Sheria ya Utumishi ibadilishwe kwa ajira ya watumishi mfano Mkuu wa Idara, anatakiwa akaimu kwa muda wa miaka sita. Anapokaimu kwa muda wa miaka sita inamvunja moyo wa kufanya kazi. Kwa hiyo, ninaomba sheria hiyo kwa sababu TAMISEMI, Mkuu wa Idara ni lazima



amalize miaka sita ndipo aajiriwe, naomba sheria hii pia aangalie upya ili iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mradi wa *TASAF*, *TASAF I* imefanya kazi vizuri sana lakini *TASAF II* inapoanza, ni vizuri sasa ijielekeze kwenye miradi ambayo haijakamilika. Nilichangia pia kwenye Ofisi ya TAMISEMI kwamba miradi ambayo haijakamilika ya *TASAF I* mfano elimu, afya kwa sasa hivi *TASAF II* ingeangaliwa upya ili kuondoa kero na matatizo ambayo yapo kwenye mradi huu. Lakini pia kuna miradi mingine ambayo ni ya wafugaji ambayo inafadhiliwa na *TASAF*, hiyo nayo ingekamilishwa kama vile majosho kwa upande wa mifugo. Halafu kuna miradi mingine ya visima pia nayo vingeweza kufanyiwa kazi nzuri kwa *TASAF II* ili miradi hii iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu wastaafu ambapo sasa hivi kuna matatizo mengi, *documents* zao zinapotea, halafu kuna wajane ambao wanafuatilia. Tatizo kubwa ambalo nimeliona ni ufuatiliaji wa hawa wastaafu na hususan wanapokuwa wamefariki wake zao au waume zao, wanapata taabu sana kupata mirathi. Ukienda Wizarani, wanasema kwamba nenda Utumishi, ukienda Utumishi ni kusumbuka na wanasumbuka, bado Kitengo hiki cha wastaafu hakijawa na utaratibu na usimamizi mzuri. Pamoja na utaratibu tuliokuwa nao ambao tumejiwekea kuhakikisha kwamba tunamaliza kazi zetu kwa wakati na kwa muda muafaka lakini Kitengo hiki cha Utumishi kwa wale wastaafu, kwa kweli kuna usumbufu mkubwa sana. Kwa sababu kuna sehemu nimepeleka malalamiko ya wastaafu mpaka sasa hivi lakini naambiwa lete hiki alete hiki mpaka hivi leo bado namaliza mwaka na namaliza Bunge bado kabisa hawa wastaafu hawajaingizwa kwenye *payroll* na bado hawajafanyiwa kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yako na ridhaa yako, niombe nimepeleke kumbukumbu hizi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili alifuatilie. Dada yangu huyu ni mahiri sana, kazi anafanya nzuri sana na juzi juzi ametoka Tabora, amefanya kazi nzuri na amekaribishwa vizuri, amepokea matatizo makubwa sana ambayo walikuwa wamemlalamikia wananchi, ni tumaini langu na yale malalamiko ya watumishi ambao wamempelekea dada yangu, atayasikiliza na atayafanyia kazi. Hao wastaafu wawili ambao bado wanasumbuka ni vizuri sasa nimepeleke ili angalau aweze kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nishukuru sana kwa sababu nilikuwa nimeshakata tamaa ya kuchangia. Kwa hiyo, nimshukuru sana na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nishukuru sana kwa wale waliosema tuongeze muda kwa ajili ya Chama Tawala. Ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia 200. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchemba. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge ambao tuko ndani tuendeleo kuvumiliana kuwepo kwa ajili ya jukumu lililo mbele yetu lakini vile vile Wabunge ambao wako nje ya ukumbi huu, niwaombe sana warudi haraka kadri iwezekanavyo. Najua kuna vikao kadhaa vinaendelea lakini ni vizuri tuwe na idadi inayotutosheleza vizuri kupitisha mambo yetu.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Magalle Shibuda, dakika 10, kwa kawaida Mzee Magalle Shibuda dakika 10 hazimtoshi, lakini ebu jaribu mzee.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, napenda nichukue fursa hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja ya maombi ya bajeti kwa Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza juhudi zote zinazofanywa na Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora). Napongeza vilevile juhudi zote zinazofanywa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwa ustawi na maendeleo ya Utumishi wa wananchi wa Tanzania kupitia Idara yake. Utekelezaji wenu, kwa kweli, ni nuru ya matumaini na faraja kubwa kwa msako wa matarajio ya kupata huduma bora kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamaji wa mpira ni rahisi sana kumkosoa mtu kwa sababu ya hisia za kufikirika kwamba angekuwa fulani angeweza kufunga goli. Kwa hiyo na mimi sina ugomvi na sina choyo ya ulemavu wa fikra za hisia kwa mtu ambaye ana dhana za kufikirika. Napenda kusema hayo kwa sababu sura ya ubinafsi wa kushutumiana na kusutana hasa katika kipindi cha kuelekea katika uchaguzi, huwa ni jambo la kawaida. Napenda kubainisha kwamba tuko katika mwaka wa tano hivi sasa na kiinua mgongo kwa Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala pamoja na Serikali yake na kiinua mgongo kwa Wabunge, Madiwani ni kusutwa, kusengenywa kwa sababu watu wenye uchu wa madaraka ndio hulka na silka yao kuja na maneno ya fedhuli mbalimbali. Kwa hiyo, sishangai hata Chama cha Mapinduzi kikisemwa, hata sisi tukisutwa kwa sababu “dua la kuku halimpati mwewe” na “asiyejua maana haambiwi maana”. Lakini napenda kuwakumbusha wale wanaotusuta na kusema maneno ambayo ni ya utashi wa hisia binafsi kuwaambia kwamba jamani “kelele za mpangaji hazimnyimi usingizi mwenye nyumba”, kwa hiyo, mna haki ya kusema, semeni hayo mnayoyasema lakini sisi tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Maswa, sasa naomba nitumie fursa hii, kuishukuru sana Serikali kwa mambo yote iliyowatendea wananchi ya kuchochea ustawi na maendeleo ya jamii. Vile vile napenda nitumie fursa hii, kumpongeza mwana mtoto wa Maswa, Dr. Edward Hosea wa PCCB, kwa juhudi zake na kukumbuka kwao kwa sababu hata katika Kitabu cha Hotuba iliyotolewa mnaona jengo la PCCB Maswa, hongera kijana, Mwenyezi Mungu akuepushe na akunusuru na watu wote wenye hila na dhuluma ya usafi wako ambao unaoonyesha dhahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutumia fursa hii, nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa sababu utendaji wake wa kazi, ni wa kuaminisha dhamira binafsi, hulka yake, malezi yake, mavuno yake yaliyoundwa ndani ya Mfumo wa Chama cha Mapinduzi kuhusu kusimamia haki, utawala bora, ambao kwa kweli kauthibitisha kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 15 ya mwezi huu, juzi tu, nilitangaza kuahirisha dhamira yangu kuwania uteuzi wa Kiti cha Urais katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda nibainishe ya kwamba tamko langu hilo lilikuwa ni huru, la ridhaa yangu binafsi na mtu yeyote asianze kuumba maneno ya hisia za utashi wa mapepo ya hila na dhahiki. Nasema hayo kwa sababu, la kwanza kabisa, napenda kuwaambia Watanzania na ulimwengu mzima, sikuweza kubughudhiwa kwa jambo lolote na fedhuli ya aina yoyote kutoka chombo chochote, si usalama wa Taifa na si Chama cha Mapinduzi. Nilikuwa salama salmini, nimelala salama nimeamka salama na ndiyo maana nilikuwa na jeuri ya Chama cha Mapinduzi na Katiba ya Nchi kusema ndiyo nawania uteuzi wa Kiti cha Rais. Napenda kuthibitisha kwamba sikupata bugudha yoyote kutoka Chama cha Mapinduzi, Kamati ya Maadili ya Chama cha Mapinduzi, Kamati ya Maadili ya Serikali, kwa kweli napenda kusema Watanzania tujivune kwamba tuna Rais na tuna Chama komavu ambacho kina heshimu maana ya demokrasia na maana ya utawala bora. Uthibitisho umetolewa jana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na nawaomba ndugu zangu wa Mpanda Mashariki turejesheeni huyu mtoto katika hili Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Pinda hana hila, hana choyo na kama kuna jambo la kukosoa atakosoa, kama kuna jambo la kusifia atasifia. Nakushukuru sana kwa pongezi ulizonipa na sio zangu ni pongezi kwa wananchi wa Maswa, wazazi walionizaa Jimbo la Maswa. Nakushukuru ahsante sana. Sikubughudhiwa na vikao kama nilivyosema, sikununiwa na Mheshimiwa Rais wakati wowote ule, sikununiwa hata na Mama Salma, alifika mpaka Maswa akawasaidia wanawake wa Maswa kwa zawadi ambazo wanahitaji zivasaidie katika kuimarisha huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu zangu, Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe, naomba nimpongeze Mama Salma Kikwete, kwa dhati kabisa kwa juhudi zake za kujituma kukagua mfumo dume. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Hivi yale anayoyafanya kuhimiza wanawake mpate haki, kuhimiza kuhusu masuala ya watoto mbona hatumpongezi, tunaona nongwa kwa nini anakwenda? Huo ni moyo wa kijitolea. Namwomba Mama Salma asivunjike moyo kwani hata Manabii na Mitume waliokuja kwa kheri walisutwa, aendeleo kwani malipo yako mbinguni. Pongezi hizi ni kutoka kwa waungana kama Shibuda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema hayo kwa sababu, Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kaonsha uamifu wake wa dhati kwa kujua kwamba mume wake anazungumzia ajenda ya ustawi na maendeleo kwa wanawake. Lakini tukumbuke Waafrika hatujapevuka kuondokana na mfumo dume. Hata juzi Mama Abdallah kasema na akina mama humu mmekuwa mkisemea usawa. Mimi nilitegemea leo hata ndugu zangu wa Upinzani mngesimama mkasema tunampongeza Mama Salma kwa kuhakikisha anapekua pasiwe na dhuruma za mfumo dume. Lakini ipo siku moja mtasema kwa sababu kila jambo kupevuka likafahamika huchukua muda. Kwa hiyo basi, tunakupeni subira siku moja mtapevuka mtampa hongera zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kanuni za Utumishi, tuzimarishe ili zilinde haki za watumikiwa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, imarisheni kanuni zisiwe za kulinda watumishi tu. Mnasema haki za binadamu, hata watumikiwa

wana haki za binadamu ya kupata utumishi uliotukuka kutoka kwa hao watumishi. Mtumishi kakosea, mnasema Kanuni zinazuia asisimamishwe kazi, jama kuna wengine mnawapa madaraka mnawaonea. Uzito wa mzigo wa dhamana za madaraka mnazowapa, hata kwa kweli mkiwalazimisha walindwe na kanuni, mnawaonea wananchi watarajiwa kupata utumishi huo. Kwa hiyo, tujipekue upya na kama mtu kapewa dhamana tunahisi haambiliki na haelekei akasogezwa kwa maelekezo, hili kuachiwa ni hatari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba Waziri wa Utumishi uimarishe, semina zimekuwa nyingi na makongamano hasa kwa Ma-DC. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivi kwa nini kabla ya kuwateua msiwape semina na makongamano ili wakija watembelee vijiji kwa asilimia 90, kumi iwe ni kupigwa *brush* za *workshop*? Hivi sasa, muda mwingi sana ni semina, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ma-DED wanakwenda kila siku kwenye semina, sasa kama hawa hawajaiwa wakawa watumishi wa kusimamia na kuratibu, mnawaonea kuwapa madaraka. Kwa sababu mkulima akienda shamba si aanze kupekua ardhi kuangalia, je, nikipanda mbegu hapa itaota, kazi ni jembe kulima. Kwa hiyo, nawaombeni na Idara ya Utumishi mpekue na muangalie na mchambue kwamba hayo yanakwenda vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda niwashauri, imarisheni kuchunguza fedhuli na hulka na silka za ubinadamu hasa kwa wale wanaotumikia wananchi kama Idara ya PCCB. Idara ya PCCB inapoajiri mtu haimjui hulka na silka yake. Kila binadamu ana maumbile yake na udhaifu wake. Sasa panapojulikana kwamba uaminifu na utiifu wake haufai kutekeleza majukumu yake ya PCCB hata kama alikuwa ni Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, wa Idara basi apunguziwe madaraka au apewe *marktime* kidogo, si kumwonea bali ni kumwimarisha. Naomba mpekue kwa sababu hayo yapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakieni kila la kheri Waheshimiwa Mawaziri pamoja na viongozi wote wa Idara ya Usalama wa Taifa na PCCB na Idara za Wizara zote. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunakushukuru sana Mheshimiwa Shibuda.  
**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Makatibu Wakuu wote wa Ikulu na wasaidizi wao, kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nina maoni katika maeneo machache ambayo yakiangaliwa, yataboresha utekelezaji na huduma kwa jamii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kuwa Sera nzuri za Chama cha Mapinduzi za MEMEM, MMES na Afya, zimepokelewa vizuri na wananchi, shule

zinaongezeka na hospitali (zahati/vituo vya afya) zinajengwa kwa wingi, upungufu wa Walimu na Waganga, hauendi sambamba na ukuaji wa miundombinu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, baadhi ya Walimu, Waganga na Wanasheria ambao wengi wao wanasomeshwa na Serikali, wanapomaliza wanakimbilia sekta binafsi. Nashauri yafuatayo:-

(a) Serikali ifunge mikataba na wahitimu ili wanapomaliza wautumikie umma kwa miaka kati ya mitano hadi kumi (5-10); na

(b) Mishahara Serikalini iwe karibu sawa na ile ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Taarifa za Mkuguzi wa Serikali zinaonesha kuwa tatizo la malimbikizo ya masurufu limekuwa sugu sana. Nashauri yafuatayo:-

(a) Wanaolimbikiza masurufu siyo tu waagizwe kurudisha bali wapewe adhabu zaidi ili wengine waogope; na

(b) Wahasibu na Maofisa wanaoruhusu masurufu kwa wote wasiorudisha ya awali nao waadhibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, *TASAF* inafanya kazi nzuri sana lakini siku hizi baadhi ya Maafisa wanakula njama na Wakandarasi na watumishi wa Halmashauri kuhujumu fedha za umma kwa utekelezaji mabaya wa miradi. Naomba wachunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund – TASAF*), Miradi iliyoidhinishwa – Babati Mjini. Takwimu zinaonesha kuwa Babati Mjini – *Town Council* ilipewa Shs.373,270,729.99 kwa miradi ishirini na moja tu (21). Takwima hizi zinaonyesha kuwa Halmashauri ya Mji wa Babati ndiyo iliyopewa fedha kidogo kuliko miji mingine yote nchini ukiacha Halmashauri ya mji wa Korogwe. Kwa kuwa lengo la *TASAF* ni kuibua miradi muhimu ya jamii kama vile afya, elimu, maji na kadhalika Halmashauri ya Mji wa Babati, ni kati ya Halmashauri ya mji ambayo ni changa sana. Naomba kufahamu ni sababu zipi zimepelekea Halmashauri ya mji wa Babati kupewa fedha kidogo sana na ushauri ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*). Mfuko huu ambao lengo lake ni kupambana na umaskini kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu, bado haufahamiki vizuri kwa wananchi hasa walioko vijijini. Ni muhimu zitolewe takwimu Kimkoa na Wilaya ili tuone jinsi mikopo ya mfuko huu ilivyosaidia wananchi kwa usawa. Kwa mfano, mikopo ya nyumba, *SACCOS* na ada za shule, zipo Mkoa na Wilaya zipi? Uwazi ni muhimu sana kwa mfuko huu. Naomba nipate takwimu hizi kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, napongeza sana uanzishwaji wa chombo hiki kipya ambacho sasa kitaweka kumbukumbu za wataalam, orodha ya wahitimu na kutangaza nafasi zilizowazi. Hili ni jukumu muhimu sana na naomba nishauri kuwa ajira zote za Serikali sasa zitangazwe na Kitengo hiki tu badala ya utaratibu unaoendelea wa kila Idara, Mkoa na Halmashauri kutangaza nafasi. Utaratibu huu utaondoa upendeleo kwenye Utumishi wa Umma na pia utalinda aina ya wataalam wanaojiriwa nchini. Pia utaratibu huu utasaidia kuwa na takwimu sahihi ya wanaomba kazi baada ya masomo yao hasa wa Vyuo Vikuu ambao kwa sasa wanatangatanga kutafuta ajira baada ya masomo yao. Hivyo, nashauri Kitengo hiki kiimarishwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la heri Waheshimiwa Mawaziri wote wa Ofisi ya Rais na watendaji wao wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Umma na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), kwa hotuba nzuri na yenye kutayarishwa kwa umahiri mkubwa. Naomba kuwapongeza Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Ofisi ya Rais, kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo ndiyo msingi wa mazingira mazuri na ufanisi katika utendaji kazi wa umma wa Tanzania na amani iliyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kipekee kabisa, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi (Wilaya mpya ya Momba), kwa busara zake kwa kuweza kusikia kilio chao cha siku nyingi. Kwanza, kuwatembelea Jimboni katika Tarafa na kijiji cha Kamsamba tarehe 31/10/2009. Pili, kuwapa matumaini ya kukamilikishiwa ujenzi wa barabara ya Mlowo – Kamsamba kipande kati ya Ikumbula na Kamsamba (Kilomita 25) na daraja la Mto Momba pale Kamsamba kijijini. Tatu, Kutupatia gari ya kubebea wagonjwa Kituo cha Afya Kamsamba na nne, kututunuku Wilaya na Halmashuri mpya ya Wilaya ya Momba na Tarafa mpya ya Tunduma, Mwenyezi Mungu azidi kumpa wingi wa hekima.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitoe shukrani za dhati kwa taasisi zote zilizopo chini ya Ofisi ya Rais, kwa utendaji bora hususan katika maeneo ya utawala bora na maadili ya viongozi na watumishi vinadumishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mengi mazuri yanayofanywa na Wizara na taasisi zilizoko chini ya Ofisi ya Rais, naomba nitoe machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni *TASAF*. Pamoja na umahiri wake katika kushirikisha wananchi katika kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali, kuna matatizo

yanayojitokeza ambayo hayachukuliwi hatua stahili kwa mfano, miradi mingi ya maji vijijini, hususan uchimbaji visima na uwekaji pampu zisizokidhi viwango. Hapa Wakandarasi wamekuwa wakitumia hila na udanganyifu. Visima vingi havitoi maji. Pamoja na taarifa kutolewa, *TASAF* haionekani kuchukua hatua kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa madarasa na mejengo mengine, *TASAF* imekuwa haikamilishi kwa wakati kutokana na urasimu/ukiritimba mkubwa katika hatua mbalimbali za kufikisha fedha kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, TAKUKURU. Pamoja na madai kuwa ni katika kutekeleza dhana ya utawala bora na haki za binadamu, taasisi hii inachelewa mno au kupuuza kuchukua hatua stahili kwa wakati muafaka kwa matukio mbalimbali yanayohusu rushwa. Ni vema hatua za haraka na kwa wakati muafaka zichukuliwe katika kutenda haki kwa watu wanaodhulumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Utumishi wa Umma. Ofisi inapongezwa sana kwa hatua za kuhakikisha mazingira ya Utumishi wa Umma yanaboreshwa. Hata hivyo, kuna wakati ambapo watumishi wamekuwa na wakati mgumu kwa kutotekelezewa haki zao. Kumekuwa na urasimu mkubwa hasa katika kuwaingiza kwenye orodha ya watumishi na kuwapatia cheki namba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezea hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inasomesha wataalamu mbalimbali, ndani na nje ya nchi. Nia na madhumuni ni kwa Serikali kujitosheleza kwa wataalamu na kuleta ufanisi katika kazi. Lakini kwa kadri siku zinavyokwenda, wataalamu wengi wanahama kutoka Serikalini ama kabla ya kuajiriwa na Serikali. Aidha, inaonekana kwamba Serikali haina takwimu sahihi ya wataalamu iliyowaajiri na ina upungufu kiasi gani au ziada kiasi gani. Kutokuwa na takwimu sahihi ya rasilimali watu, kunaathiri sana maendeleo ya kiuchumi katika nchi. Serikali haina budi kuweka na kutunza takwimu sahihi za rasilimali watu katika sekta zote za kiuchumi na zile za utoaji huduma kwa wananchi. Hatua hii haitasaidia tu kupanga mikakati mizuri ya kiuchumi lakini pia tutakuwa na mipango sahihi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba taasisi ya TAKUKURU imepata mafanikio makubwa katika mwaka 2008/2009 kwa kazi ambazo zimetekelezwa na katika kipindi hiki cha Uchaguzi Mkuu ambapo michakato na kutangaza nia kunaendelea, TAKUKURU imepania vya kutosha kuona kwamba hakuna mchezo mchafu unaochezwa. Ni jambo la busara sana TAKUKURU kusimamia jambo hilo ipasavyo. Lakini nipende kuishauri Serikali kuwatupia macho sana Watendaji wa Halmashauri ambao wamepewa mamlaka na Tume ya Uchaguzi (*NEC*) kusimamia mchakato wa Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunalalamika kwa muda mrefu sasa kwamba Watendaji wa Halmashauri wamekuwa wanatumia vibaya madaraka wanayopewa na *NEC*. Mara nyingi wamekuwa wanavikandamiza Vyama vya Upinzani wakati wa mchakato wa uchaguzi na kupendelea Chama Tawala kwa sababu tu wameajiriwa na

Serikali ya Chama Tawala. Tunaiomba TAKUKURU iwe macho sana juu ya Watendaji wa aina hii kwani hatma yake wanaweza kutuletea vurugu katika nchi.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kutoa mchango wangu katika suala zima la Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Dhana ya suala hili ni nzuri sana hasa ukizingatia kwamba walengwa wakuu wa mfuko huu ni wajasiriamali wadogo wadogo. Nia na madhumuni ni kuwaimarisha wananchi wa kawaida kiuchumi ili kuweza kumudu maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, kwa kiasi fulani mfuko huu haukutimiza lengo kwa sababu zifuatazo:-

a) Kutowaandaa ipasavyo kibiashara wajasiriamali husika. Kama tunavyofahamu, wajasiriamali wengi na hasa wanaoishi vijijini, hawana elimu ya kutosha ya ujasiriamali hali inayopelekea kutosimamia vema biashara zao na hatimaye kuambulia hasara. Napenda kuishauri Serikali ichukue juhudi za makusudi kutoa elimu ya kutosha juu ya ujasiriamali kabla ya kupewa fedha za Mfuko wa Kujitegemea ili waweze kusimamia vyema miradi yao kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla.

b) Utaratibu mzima wa uteuzi wa wajasiriamali ambao wangepaswa kupatiwa fedha za mfuko huo. Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kwamba kumekuwa na upendeleo wa dhahiri katika utoaji wa fedha hizo. Mfano huu pia nimeuona kule Zanzibar kwa sababu masheha wamehusishwa sana katika utaratibu huu, lakini wao hawatendi haki katika kupitisha majina ya wale ambao wanapendekezwa kupatiwa mkopo huo. Ninaishauri Serikali iuangalie utaratibu mzima wa utoaji wa fedha hizo kutoka ngazi ya juu hadi kule vijiji ili kuona haki inatendeka kwa wananchi wanaoomba mkopo huo.

c) Mfumo mbaya wa utozaji riba juu ya mkopo huo. Hili ni tatizo baya zaidi. Imedhihirika kwamba mfuko huu unatoza riba ya asilimia 2.5% kwa mwezi. Ukiikokotoa asilimia hii kwa mwaka inakuwa asilimia 30%. Ni dhahiri kwamba riba hii ni kubwa na mzigo mzito kwa mwananchi wa kawaida. Kwa maneno mengine ni kwamba badala ya kumsaidia mwananchi wa kawaida kuondokana na umasikini, viwango hivi vya riba vinamuongezea umasikini na kwa hivyo lengo lililokusudiwa halitoweza kupatikana. Ninapenda kuishauri Serikali kuviangalia upya viwango vya riba vilivyowekwa juu ya mkopo huo ili viteremshwe vilete nafuu kwa wajasiriamali wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tutaweza kumkomboa Mtanzania kiuchumi.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Maafisa wanaoshughulika na rushwa mara nyingi hukaa ndani ya Ofisi na kushindwa kugundua rushwa zinazozagaa, nashauri pindi Wanasisia wanapogundua rushwa na kuinadi katika majukwaa, wasipuuze bali wafuatilie ili kujua ukweli wa Wanasisia hao.



Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni jinsi gani Watumishi ambao walijajiwa Serikali Kuu na wakahamia Halmashauri au waliohamia Serikali Kuu baada ya kuajiriwa na Halmashauri, wamewekewa utaratibu upi wakati wa kulipwa maslahi yao ya kustaafu? Hasa pale anapofanya kazi eneo moja kwa miaka kadhaa na eneo lingine miaka kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itafutwe jinsi ya kuzuia rushwa kwa Waratibu wa *TASAF* katika Mikoa na Wilaya zake. Kwani vikundi vinapoibua miradi na kupata fedha za miradi hiyo, baadhi ya Waratibu hudai kiasi fulani apatiwe yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watumishi ambao walipunguziwa mishahara yao kwa madai kwamba hawakupata vyeo kihalali na Afisa Utumishi lakini baadaye ikaonekana kwamba si sahihi na warudishwa kazini lakini hadi leo hawajarudishwa katika mishahara yao ya awali. Watumishi hao wapo Halmashauri ya Kilwa. Naomba wale Maafisa wanaohusika na Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Kilwa walifuatilie suala hili ili Watumishi hao waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayestahili kupata mikopo ya magari awe bado ni mfanyakazi anayeendelea kufanya kazi na siyo ambaye anakaribia kustaafu kabla ya miezi saba, hata kama watakatwa katika *pension* yao. Hii ni sheria. Mambo hayo yametokea Bandarini. Ahsante.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri TAKUKURU wapewe vitendea kazi kama magari ya kutosha hasa wakati huu wa uchaguzi ili waweze kufika maeneo ya matukio mara moja wanapopata taarifa. Vilevile, watendaji hawa wajulikane ili wapewe taarifa za matukio na wananchi kirahisi, wasiwe Watumishi wa SIRI, wajulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke muda maalum wa Mtumishi hasa kwenye Serikali za Mitaa, kukaa kwenye eneo moja. Watumishi wasihamishwe ovyoovyoya bila utaratibu au vigezo vinavyoeleweka. Hali ya sasa ni fujo, viongozi wanachagua watumishi wanaowataka na hii inapunguza ufanisi wa kazi. Hali hii inakuwa mbaya zaidi maeneo ya mazingira magumu ambako watumishi wanakwepa kwenda huko ili mradi wanakuwa na viongozi wa kuwasemea.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia uzima na afya na kuweza kuchangia bajeti hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana uongozi wako, Spika, Naibu Spika pamoja na viongozi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu ni kuwa, Serikali ijitahidi sana kuboresha mishahara ya wafanyakazi ili iepushe migogoro isiyokuwa ya lazima ambayo hupunguza ari ya wafanyakazi kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuisisitiza Serikali iongeze kasi ya kuhakiki watumishi hewa ili kupunguza gharama kubwa za Serikali zisizokuwa na lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala bora, naomba Serikali ichukue jukumu lake la kusimamia vyema suala la rushwa ili wasiendelee kulitia Taifa letu aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwapongeza wote waliotoa hotuba zao vizuri, nashukuru.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora na timu zao za Utumishi zinazoongozwa na Makatibu Wakuu, kwa kuandaa Hotuba ya kina na yenye mwelekeo kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2010/2011. Natamka kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Utumishi vilivyopo ni vitatu tu yaani Dar es Salaam, Tabora na Mtwara. Ni wakati muafaka kuanzisha Vyuo Kikanda ili Watumishi wengi waweze kupata mafunzo ya kina ambayo yatawawezesha kutekeleza, kusimamia na kuratibu kazi zao kikamilifu. Naomba Mheshimiwa Waziri azingatie ushauri wa kuanzisha Vyuo Kikanda.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, kwa hotuba yake nzuri, yenye takwimu muhimu na aliyoisoma kwa ufanisi mkubwa. Tumeielewa vizuri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Bwana P. Luhanyo, Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana G. Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na wasaidizi wao wote, kwa kushirikiana vizuri na hivyo kumwezesha Waziri mtoa hoja kuwasilisha hotuba yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo suala moja ambalo nashauri liangaliwe kwa undani, nalo ni kuhusu Kitengo cha Utumishi na Utawala cha Halmashauri za Wilaya ambacho ni hafifu sana. Hakina Maafisa wenye taaluma na uzoefu hasa cha Halmsahuri ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia M. Simba pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma), kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo yanayosimamiwa na Wizara, ni pamoja na Chuo cha Utumishi wa Umma cha Tabora. Chuo hiki kinahitaji upanuzi wa haraka ili kukidhi mahitaji ya nchi ya Watendaji wa Maofisini katika ngazi mbalimbali. Kwa kuwa eneo la Chuo pale Tabora ni kubwa, ninashauri Serikali iweke mkakati wa makusudi kwanza wa kuyahamisha Makao Makuu ya Chuo toka Dar es Salaam na kuyapeleka Tabora. Pili Serikali itoe dhamana kwa Chuo ili kukiwezesha kupata mkopo toka Mashirika ya Hifadhi ya Jamii ili kukiwezesha kujenga majengo mapya kwa ajili ya madarasa, mabweni, Ofisi za Walimu, nyumba za Walimu n.k. Kwa kuzingatia kwamba Chuo kinaingiza mapato mazuri kutokana na karo za wanafunzi, nina hakika kwamba kitaweza kupata ziada ya kulipa mikopo itakayoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa uchaguzi, ili uchaguzi wetu uweze kufanyika kwa amani na utulivu pamoja na kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, ni vema TAKUKURU ikajipanga vizuri kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kazi nzuri, mafanikio yanaonekana, msijali maneno ya wafamaji, wamezidiwa na mafanikio ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni sana.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshuksuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uzima na kuniwezesha kufanya kazi zangu kwa ufanisi. Pia niwashukuru wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Fuoni, kwa kuniamini na kunipa kazi hii ya Ubunge nami naamini kwa ushirikiano tulionao, naamini watanirejesha tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mawaziri wote wanaoshughulikia Ofisi ya Rais pamoja na watendaji wote waliofanikisha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU ni chombo kinachosimamia kupambana na rushwa, rushwa ni adui wa haki. Hivi sasa tumekabiliwa na Uchaguzi Mkuu nchini na Serikali imetunga Sheria Na.6 ya Gharama za Uchaguzi ili uchaguzi wetu uende kwa haki na kupata viongozi bora. Hivi sasa katika Majimbo ya Uchaguzi, vitendo vya rushwa vimetawala kwa watarajiwa tena bila kificho, lakini hadi leo hatujasikia watarajiwa au wapambe kukamatwa. Hali hii inatia wasiwasi kana kwamba chombo hicho hakipo. Je, ile kazi ya kuchunguza vitendo hivi kabla na baada ya kura za maoni

iko wapi au tunasubiri Uchaguzi Mkuu? Naiomba Serikali masuala haya yafanyiwe kazi bila kujali nani amefanya kosa bila hivyo viongozi wengi watakaoingia ndani ya Bunge hili watakuwa watoa rushwa na dhana ya viongozi bora itakosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA ni ukombozi wa wanyonge na tunaishukuru Serikali kwa hili. Katika hotuba ya Waziri, ametaja vijiji vingi, Tanzania Bara vilivyobahatika na kupimiwa mashamba yao lakini kwa Tanzania Visiwani kataja vijiji viwili lakini hakuvitaja vyote, ni vema Mheshimiwa Waziri angevitaja vijiji na mitaa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Waziri Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa kuandaa hotuba ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwenye hotuba hii ni watumishi walioajiriwa na Serikali hususan Halmashauri na wanalipwa na Halmashauri zenyewe kwa muda mrefu, kwa nini Serikali Kuu isiwalipe kwenye *payroll* yake? Mfano, Bukombe wapo watumishi wameajiriwa tangu 1997 hadi leo bado wanalipwa na vyanzo vya Halmashauri kiasi kwamba hata mikopo benki hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa watumishi wa Idara ya Afya, wapo waliosoma na kufuzu kozi ya afya lakini elimu yao ni Darasa la Saba. Kwa nini Serikali isiwaajiri ili kupunguza upungufu huu na baadaye wajiendeleze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa nafasi za *VEO's*, nashauri Serikali iruhusu *VEO's* waajiriwe toka kwenye Wilaya husika. Inavyoonekana kwa taarifa za Wilaya ni kwamba ajira hizo zitaajiriwa na Sekretarieti ya Ajira. Nadhani tuziachie Halmashauri husika ili vijana waliomaliza Elimu ya Sekondari toka Wilaya hizo wapate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kwa kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mheshimiwa Hawa Ghasia, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Mheshimiwa Sophia Simba - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Bora, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo imesheheni mikakati mbalimbali katika kuboresha utendaji na ufanisi wa Wizara zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kabla sijaanza kutoa mchango wangu, niunge mkono hoja hii kwa moyo mkunjufu na ninawatakia utekelezaji mwema na wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitashukuru juhudi za Serikali katika kusikiliza na kupokea maombi ya watumishi kutoka Halmashauri zetu

na Taasisi mbalimbali za Serikali mkoani Singida. Hata hivyo, bado tunakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu Shule za Msingi na Sekondari, wauguzi na madaktari. Kwa maombi hayo yako ofisini kwa Mheshimiwa Waziri ninaomba kwa niaba ya Mkoa wangu, tupatiwe vibali hivyo ili tuweze kupangiwa watumishi hao na Wizara husika kwani upungufu wa kada hizi ni mkubwa sana kiasi cha kusababisha kushuka kwa taaluma Mkoani Singida katika shule zetu za msingi na sekondari, pia upungufu wa wauguzi na madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kupandisha mishahara ya wafanyakazi, kuongezewa mishahara. Ni wazi kuwa tija ya utendaji wa kazi itaongezeka kwa wafanyakazi na migogoro kazi kwa mwajiri na waajiriwa itapungua kama sio kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri wa Fedha hakutaja kima cha chini, ni vyema kitamkwe ni kiasi gani hata kwa asilimia kama sio kiwango halisi cha mishahara. Hii italeta faraja kwa wafanyakazi, pia tutakuwa tumekinadi Chama cha Mapinduzi kuchukua dola Uchaguzi Mkuu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la wafanyakazi kuomba rushwa kwa wananchi ili waweze kuwahudumia, mfano Mahakama, Hospital na vitengo vinavyotoa ajira katika Taasisi mbalimbali za Serikali. Ninaomba Serikali kukomesha tabia hiyo kwani inapaka matope Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tabia ya baadhi ya watumishi kufanya biashara saa za kazi na kuacha kufanya kazi. Ninaomba Serikali kukomesha tabia hii kwa adhabu kali kwa watumishi wenye tabia hii, kwani wanaiibia Serikali na kutokutoa huduma ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tabia ya watumishi kutopanga namna ya kuongeza vipato vyao nje ya mishahara, kitendo ambacho kinawafanya kuwa na maisha duni siku zote. Hivyo ni vema Serikali itoe elimu ya namna ya kuwa na vyanzo vingine vya kipato mfano kilimo, biashara ndogo ndogo bila kuingilia saa za kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia tena kuwa ninaunga mkono hoja hii na ninarudia kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa utendaji na uongozi wao makini na kuendelea kuwadhihirishia Watanzania kuwa wanawake tunao uwezo mkubwa sana. Nawaomba tu kuwa makini kwa watumishi wanaokimbilia mashirika binafsi wakati wamesomeshwa na Serikali, kuwepo na sheria ya kuwabana.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam wote waliohusika na maandishi ya bajeti hii, kimsingi bajeti ni nzuri. Hata hivyo, napenda kumchangia katika maeneo machache kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la rushwa, wapo viongozi ambao hawawezi kufanya kazi zao hadi wapewe kitu chochote. Kwa

ujumla rushwa imekuwa kama ugonjwa. Idara zinazoongoza kwa vitendo vya rushwa ni pamoja na Mahakamani, Polisi Hospital za Umma na kadhalika. Aidha, nakiri kwamba TAKUKURU inajitahidi kufanya kazi, lakini kwa mtazamo wangu, Idara hiyo inalemewa, watumishi wachache na vifaa vya kufanyia kazi kama vile gari ni chache pia. Ninaomba Serikali irekebishe hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia baadhi ya wafanyakazi wa Wizara hii ambao siyo waaminifu. Hawa wanaipaka Idara matope, wanapobainika waondolewe mara moja. Aidha, wakati huu tunapokwenda kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, vitendo vya rushwa vinaelekea kushamiri. Naomba TAKUKURU ifanye kazi zake vizuri bila kumwonea mtu haya. Lakini pia bila uonevu usio na sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema miaka ya 1990, Serikali ilianza kufanya mabadiliko mbalimbali hasa yaliyokusudia kuboresha utendaji kazi Serikalini. Sasa ni zaidi ya miaka 15 tangu mpango huo uanze, hata hivyo naona bado kuna matatizo mengi Serikalini kwa mfano, bado upandishwaji vyeo (madaraja ) na urekebishaji mishahara haijapatiwa ufumbuzi mzuri bado waalimu wanaendelea kuathirika na tatizo hilo watumishi wa kilimo hasa maafisa ugavi, watumishi wa Afya n.k.wanaendelea kucheleweshewa haki zao, napenda kujua tatizo ni nini hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ilihoji na mpango upimaji utendaji kazi wa wazi, yaani *Open Performance Review and Appraisal system (OPRAS)*. Mpango ulikuwa na lengo la kupima wafanyakazi, namna wanavyofanya kazi kwa uwazi zaidi, lengo pia lilikuwa ni kupeana malengo yanayotekelezeka na mwisho wa kipindi kilichokubalika upimaji uweze kufanyika. Hata hivyo, pamoja na nia nzuri ya Serikali, bado kwa maoni yangu kuna utendaji kazi usioridhisha kwa wafanyakazi wengi Serikalini. Nataka kujua, tangu utaratibu huu uanze, ni nini mafanikio na matatizo yake? Jitihada gani zinachukuliwa kuondoa matatizo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna urasimu mkubwa sana Serikalini hasa katika suala zima la kujibu barua za wananchi wanaoandika barua katika Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Najuliza, mabadiliko haya Serikalini yamewasaidia namna gani viongozi hao ambao hawawezi kujibu barua za wananchi? Je, hii ndio utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado suala la ucheleweshaji wa malipo hasa malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma ni tatizo kubwa katika eneo hilo, naomba kujua tatizo ni nini na litaisha lini? Nilitegemea kwamba katika kipindi hiki cha *reform*, wafanyakazi wetu wasingeweza kucheleweshewa haki zao. Tukumbuke kwamba haki inayocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009 kima cha chini kwa wafanyakazi wastaafu kilipandishwa kutoka karibu Sh. 21,000/= hadi Sh. 51,000/=. Bado kiwango hiki ni kidogo. Je! Si ingekuwa kwa watumishi wake ikapandishwa pia kiwango cha chini cha pensheni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa la mishahara kwa watumishi wa sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Wakati Serikali imeshaweka kima cha chini cha mishahara kwamba ni Sh. 104,000/=, bado watumishi wengi wa sekta binafsi wanalipwa Sh. 65,000/= hadi Sh. 87,000/= kwa mwezi. Ni kwa kiasi gani Serikali kwa kupitia Wizara hii inafuatilia sekta hizi na kuhakikisha kwamba maagizo/maamuzi ya Serikali yanafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watumishi wanajiendeleza kimasomo katika fani mbalimbali, wengine kwa gharama zao, wengine kwa kugharamiwa na Serikali. Hii ni kuongeza ujuzi na hivyo kuleta tija zaidi katika kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha, wanapomaliza masomo yao na kurudi kwenye vituo vya kazi wanabaki pale pale kwenye vyeo vyao bila kutambulika kupandishwa vyeo wala kuongezwa mishahara. Mfano, mwalimu wa *primary* anajiendeleza hali anapata *degree* na wengine *degree* ya pili (*Master Degree*) bado anaendelea kufundisha *primary school* wakati tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu wa Sekondari. Hili linawakatisha tamaa na wengine wanaamua kuondoka kutafuta kazi kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumiwa na Serikali wa kumhamisha mtumishi pale anapokiuka maadili ya kazi ikiwepo ubadhilifu wa fedha za walipakodi, kushindwa kuwajibika na makosa mengine, ni utaratibu mbovu sana na hili linatusababishia matatizo makubwa kama nchi na linazalisha watumishi wasio waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida sasa pale mtumishi anaposhutumiwa kwenye kituo chake na kuthibitika kwamba kukiuka taratibu za kazi, Serikali inamhamishia eneo lingine. Huku ni kulea watendaji wabovu, ni kuendeleza vitendo vya ubadhirifu, kuliingizia Taifa hasara na matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mishahara kwa watumishi hawa ni aibu kwa Taifa. Ina maana hakuna utaratibu makini wa Serikali wa kutambua watumishi wake wote waliyopo kazini, waliokufa, waliostaafu na waliohamishwa? Fedha nyingi zinapelekwa kwenye Halmashauri zetu wakati watumishi hao walishakufa na wengine walishastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana hakuna taarifa/takwimu sahihi za watumishi wa Serikali waliopo kazini? Hii ni aibu.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dr. Jakaya

Mrisho Kikwete, Waziri wa Nchi ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora; Katibu Mkuu, Utumishi wa Umma na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa kazi nzuri sana waliyofanya ya kutekeleza ilani ya CCM ya mwaka 2005 na pia kuweza kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba uwekwe utaratibu wa uwiano kati ya muda wa kufanya kazi, malengo na matokeo ambayo yataonyesha kiasi kilichoanzishwa kwa kila mwezi. Ungaliwe uwezekano wa kufanya kazi kwa masaa 24 kwa maeneo ya uzalishaji ili kufidia pengo kubwa la kutotimiza malengo yaliyokusudiwa na kuongeza tija kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tofauti kubwa kiutendaji kati ya watumishi wa umma na wafanyakazi walio katika sekta binafsi kwa upande wa watumishi wa umma wanafanya kazi kwa mazoea, lakini wanafanya kazi kwa kutimiza malengo yao ya kila mwezi: Je, ni sababu gani kwa watumishi wa umma kutokufanya kazi kwa bidii kama wenzao wa sekta binafsi. Serikali ingeangalia sana eneo hili.

Katika Halmashauri, baadhi ya Watendaji Wakuu wa Idara mbalimbali hawawajali ipasavyo, hawajui wajibu wao, hawakagui miradi, hali ambayo husababisha miradi mingi katika Halmashauri kutokuwa na ubora na kutomalizika kwa wakati.

Maoni yangu ni kwamba, kiundwe chombo kitakachoweza kuratibu na kukagua miradi mbalimbali katika halmashauri zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* imeshindwa kusimamia suala la kodi ya majengo (*Property Tax*) Mkoani Dar es Salaam na kusababisha Halmashauri kutotimiza matarajio ya Halmashauri na wananchi. Tunaomba Serikali iangalie eneo hili nyeti la chanzo kikubwa cha kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa TAKUKURU. Mwisho, naipongeza TAKUKURU kwa elimu wanayoendesha kutupatia na mafanikio makubwa waliyopata katika kipindi kifupi cha utendaji wa Dr. Hosea.

Naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, Mawaziri wenye dhamana na Wizara ya Utumishi na Wizara ya Utawala Bora pamoja na hayo niwapongeze pia watendaji wote wa Wizara hizi.

Kuhusu utumishi, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo juu ya urahisishaji wa mawasiliano Serikalini kwa kutumia mfumo mpya wa Serikali mtandao (*E-Government*) ambao mfumo huu unatoa fursa ya kurahisisha mawasiliano kwa watendaji wote wa Serikali na wa umma ni fedha kiasi gani zitafanya utekelezaji wa mfumo huu, naomba Waziri wakati wa majumuisho atoe ufafanuzi ili kuiongezea



uboreshaji kiutendaji Serikali yetu. Kukamilika kwa mfumo huu kutaondoa uzembe, wizi, urasimu na kadhalika na hivyo kujenga heshima kwa Serikali.

Kuhusu wastaafu kwa nini bado kuna urasimu mkubwa wa kuwapatia mafao wastaafu? Malipo yanacheleweshwa na kuleta usumbufu mkubwa zikiwemo gharama za kufuatilia madai yao hazina. Kwa nini hadi leo Serikali haijawa na utaratibu wa kuandaa malipo ya moja kwa moja kwa kufanya sensa ya kila mwaka kufahamu ni idadi gani ya wastaafu kutoka Idara za Serikali kwa kila mwaka wanaostaafu ili waandaliwe malipo yao na siku wastaafu wanapoagwa ili kupewa mkono wa kwa heri bila usumbufu .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya elimu, walimu wanateseka sana wanapostaafu kwa kuwa kada hii wengi wao wanatoka vijijini.

Suala la mishahara, ni kweli kabisa kiwango cha mishahara kima cha chini bado hakitoshelezi, hali ya maisha ya Mtanzania jambo lililo muhimu pamoja na mzigo kuwa mkubwa kwa Serikali naomba Serikali kukubaliana na maombi ya Vyama vya Wafanyakazi (*TUCTA*) katika mapendekezo yao ya kupunguza kodi inayotolewa na mishahara lakini pia nasisitiza juu ya Serikali kuangalia kwa kina sekta binafsi kwani huko ndiko kwenye dhuluma kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo za utawala bora ziendelee kudumishwa na kuimarishwa zaidi kwa ufuatiliaji wa vitendo hasa kwa kuangalia utendaji wa watumishi wanaotoa huduma kwa wateja kama wanazingatia nguzo za utawala bora ambazo ni uwajibikaji, ushirikishwaji na uwazi. Nguzo hizi zikisimamiwa kwa ufasaha mazingira ya upendeleo, wizi, rushwa, uzembe kazini, maamuzi bila kuzingatia utaratibu na kadhalika yatatoweka na hivyo kuzidisha ufanisi na kuongeza tija kwa Taifa.

Suala la maadili kwa watumishi wa umma, naiomba Serikali ili kujenga misingi ya utaiifa ni muhimu sana Tume ya maadili kufanya kazi kwa karibu na viongozi wote wa taasisi za umma ili kufuatilia mwenendo katika kutoa huduma kwa wateja hali ya namna hiyo itafanya viongozi kufanya kazi kwa kuzingatia maadili. Viongozi wenye kukiuka maadili wafuatiliwe kwa ukaribu na hatua za kinidhamu zichukuliwe, Tume iongezwe uwezo kwa kubaini viongozi wakorofi, wasiozingatia utawala bora, Tume iwatolee taarifa kwenye vyombo husika kama TAKUKURU, mahakama, polisi na kadhalika ili kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TAKUKURU baada ya kuongeza meno (Sheria ya Rushwa ) naomba Serikali kuongeza idadi ya watumishi wa taasisi hii ili waweze kukabiliana na hali hiyo kwani idadi ndogo bado haiweze kuhimili kuzuia wimbi kama vile magari madhubuti na kadhalika, navyo pia vipewe kipaumbele ili kuboresha taasisi hii katika mapambano ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASAF*, mfuko huu umetumika na unaendelea kutoa huduma ya miradi mbalimbali kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika jimbo langu la Mkoani katika eneo la Wambaa *TASAF* iliweka kifusi kwenye barabara, lakini jambo la kusikitisha ujenzi huu wa barabara kwa kutumia kifusi kwenye eneo hilo haukuwa makini matokeo yake sehemu kubwa ya barabara hiyo kifusi kimechukuliwa na maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema ujenzi huu wa barabara kwa kutumia mfuko wa *TASAF* uwahusishe wataalamu wa barabara na ujenzi usiwe wa kulipua vinginevyo fedha inayatumia katika ujenzi huo hazitaleta maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Rais kujitegemea, kuna malalamiko makubwa juu ya fedha zinazotolewa katika Mfuko wa Rais kwa walengwa, ipo haja yafanyike marekebisho makubwa katika kuzigawa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusiana na nani wa kupewa fedha hizi ni wale ambao tayari wameshaanza kujiendeleza katika miradi yao sio watafutwe watu watakiwe waanzishe miradi ili wapewe au wakopeshwe fedha ya Rais ya kujitegemea. Katika hali hiyo ni dhahiri fedha itapotea na haitaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Utawala Bora, Tume ya Haki za Binadamu katika kuhakikisha kuwepo kwa utawala bora imeundwa Tume ya Haki za Binadamu, kazi kubwa ya Tume hiyo ni kuwasikiliza wananchi mambo yaliyowafika katika uvunjaji wa haki za binadamu. Je, wananchi wanaielewa Tume hii inafanya kazi kwa utaratibu gani? Je, ipo ratiba inayoeleweka kwa mfano kwa Zanzibar inafanya kazi vipi ipo haja kwa kupitia vyombo vya habari hususani *TV* na redio itoe elimu ya vipi inavyofanya kazi ili wananchi waweze kufika kwenye Tume hiyo kueleza malalamiko yao. Ahsante.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa *TASAF* imefanikiwa mambo mbalimbali katika kupambana na umaskini na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika baadhi ya watendaji wenye mamlaka ya kutumia fedha za *TASAF*, wanazitumia isivyo halali na kupelekea kutofikia lengo lililokusudiwa kama ilivyobainika katika Halmashuri ya Muheza, Mkoani Tanga. Serikali iwe karibu na matumizi ya fedha za *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupanda kwa gharama za maisha huku ikionekana mishahara ya watumishi wa umma ni midogo hivyo nashauri Serikali kupandisha mishahara angalau kima cha chini kiwe shilingi 350,000/= kuelekea watumishi wa umma kutumia muda wakati mwingine wa kujitafutia kipato kufidia tofauti ya hali halisi na wanachopata watumishi hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje kuhusu matumizi mabaya ya fedha kiasi cha shilingi 282,453,350/= ambacho kililipwa kwa watumishi kwa ajili ya gharama hoteli wakati walishalipwa posho za kujikimu katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya

Utumishi wa Umma, kwa mujibu wa ripoti ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawaambia nini Watanzania kuhusu kulipwa kwa mishahara ya jumla ya shilingi 2,028,200/= kwa watu waliokwishaondoka katika Utumishi wa Umma kama CAG report iliyoishia Juni 30, 2008, hivyo hatua gani zilichukuliwa?

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Hawa Ghasia pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Simba, pamoja na Makatibu Wakuu wao na viongozi wote wa Idara na Taasisi wanazosisimamia kwa hotuba nzuri na kazi yao nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo lawama nyingi kuhusu urasimu hasa uzembe na ubadhilifu sehemu nyingi nchini, kuna haja kubwa ya kupiga vita kwa dhati kero hizi ili nchi yetu ipate maendeleo yanayokusudiwa. Ni muhimu OPRAS na Clients Service Charter zikatumika kwa dhati katika dhamira ya kuongeza tija na ufanisi dhidi ya urasimu hasi, uzembe na ubadhilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutambua na kuthamini jitihada kubwa inayofanywa na Serikali kupambana na rushwa na ufisadi bado kuna haja kubwa sana ya kuongeza nguvu na hasa katika kupambana na rushwa kubwa na rushwa katika chaguzi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya kuwaendeleza wananchi chini ya miradi ya TASAF, kuna ufisadi mkubwa sana chini ya mradi huu yaliyotokea katika Wilaya ya Mkinga na ya Muheza ni uthibitisho dhahiri kuhusu kero hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kero nyingi kuhusu mapungufu ya wastaafu, malipo yao yanakabiliwa na vikwazo vingi sana na marupurupu yao hayapandishwi kulingana na mfumuko wa bei inavyokua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Utawala Bora kwa hotuba nzuri ya Bajeti na ufanisi wao wa kazi nzuri usiokuwa na kifani.

Napenda nichangie kwanza ni kwenye Manispaa zetu. Wapo watumishi ambao hawaendi na wakati, naomba Wizara iwatupie macho ili iweze kuona namna ya kuwarekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuona uwezekanao wa kuiongezea uwezo *PCCB* wa nyenzo na fedha wakati huu wa Uchaguzi ili iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MWENYEKITI:** Sasa mchangiaji wetu wa mwisho ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Sophia Simba. Utakuwa na dakika ishirini katika kusaidiana kujibu hoja pia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikuombe radhi kwa kuchelewa kufika hapa, mambo naona yameenda haraka haraka, samahani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa. Aidha, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uongozi imara na kuendelea kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa na kuiongoza nchi yetu kwa amani na hekima kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mawaziri ambao tayari wameshawaliisha Bajeti zao hapa Bungeni na kuwaombea wale ambao hawajawaliisha, mambo yao yawe mazuri. Nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na iliyojitosheleza, yenye kuonesha mwelekeo wa dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka ujao wa fedha 2010/2011. Nampongeza pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa Bajeti nzuri ambayo inalenga kumkomboa Mtanzania kwa kuanisha misingi na mwelekeo wa Bajeti na uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011. Aidha, napenda kuwapongeza pia Mawaziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kujiunga na Bunge hili akiwemo Mheshimiwa Frederick Mwita Werema, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene na pia Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Naomba pia kutumia fursa hii, kumpongeza sana mtoa hoja, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa kuwasilisha hotuba yetu vizuri sana. Aidha, namshukuru kwa ushirikiano mzuri uliopo kati ya Ofisi zetu ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Wenyeviti wa Bunge, kwa kutuongoza vizuri katika Kikao hiki cha Bajeti na vikao vyote vilivyotangulia. Vilevile kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa miongozo na ushauri wao mzuri ambao umetuwezesha kufikia tulipo. Shukrani za pekee ziende kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, kwa hotuba iliyojaa changamoto nyingi ambazo tumezipokea. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao ambayo itasaidia katika kuboresha utendaji wetu wa kazi kwani inatoa changamoto kubwa katika suala zima la utawala wa sheria, uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wapokee vitabu ambavyo umevizungumzia kama hiki hapa ambavyo tumevisambaza hapa vinavyohusu Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wakati wa uchaguzi. TAKUKURU imeona ni vyema kutoa maelezo hayo kwa faida ya wale wanaotarajia kugombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa dhati wanawake wote wa Tanzania, kwa ushirikiano wao wa hali ya juu ambao wamenipa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mwenyekiti wao wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT). Napenda kuwahakikishia kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote ili kuhakikisha kwamba tunawakomboa wanawake wa Tanzania na kuwapatia maisha bora. Nipende kuwakumbusha wanawake kuwa tunaweza kuthubutu na mwaka 2010 ni mwaka wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nawashukuru watoto wangu na familia yangu kwa jinsi inavyonipa moyo na kunivumilia kwa kazi nyingi nilizonazo kwa kuwapa muda mfupi sana wa mapumziko nikiwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la utawala bora ni suala mtambuka, hivyo hugusa maeneo mengi ya utendaji wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Aidha, ni eneo ambalo linasemwa sana hapa Bungeni, nje ya Bunge na kwenye Vyombo vya Habari hususani masuala ya rushwa ambayo ni kero kubwa kwa Taifa letu. Napenda kutoa rai kwa Watanzania wote kukataa kutoa wala kupokea rushwa, kwani rushwa ni adui wa haki na ni lazima idhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne, imejizatiti katika eneo hili na inaendelea na mikakati madhubuti ambayo inalenga kuleta uadilifu katika utendaji wa Serikali na jamii kwa ujumla. Ili kuleta utawala bora katika nchi yetu, Serikali inaendelea na jitihada zake katika kuboresha utawala bora katika nyanja zote kwa mfano maboresho katika utumishi wa umma sekta ya fedha, Serikali za Mitaa pamoja na programu ya kupambana na umaskini kama vile MKUKUTA, TASAF na MKURABITA. Maboresho

haya, yanalenga kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa mipango ya Serikali. Aidha, kutungwa kwa Sheria mpya ya Rushwa pamoja na kuundwa kwa Kamati za Maadili katika Idara zote za Serikali, kuna lengo la kutathmini kila wakati maadili, hali ya rushwa pamoja na kuziba mianya ya rushwa na hii itasaidia sana katika kujenga maadili mema na hivyo kudhibiti tatizo la rushwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Naomba nianze kujibu yale ambayo Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ameyauliza. Kuna maeneo mawili makubwa ambayo Mheshimiwa Kiwelu ameyazungumzia. La kwanza, linahusu taasisi zinazoanzishwa na Wake wa Marais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi na kazi za kitaasisi na shughuli za Mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hazikutajwa katika nyaraka yoyote rasmi. Kwa maana hiyo, kwa mtazamo wa kitaasisi, nafasi ya Mke wa Mkuu wa Nchi, haina shughuli na nafasi rasmi na hali hii sio kwa Tanzania pekee. Nafasi ya Mke wa Rais wa Tanzania ni sawa na Wake wa Marais wa nchi nyingi duniani. Umoja wa Afrika kwa mfano umezesha kuundwa kwa Umoja wa Wanawake wa Marais wa Afrika dhidi ya UKIMWI ili kutoa fursa kwa Wake wa Marais kutoa mchango wao katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo kwa maana ya kupunguza maambukizi, kuhamasiha upimaji na utoaji wa tiba na huduma kwa wenye VVU. Aidha, Mke wa Rais hushiriki katika shughuli nyingi za kijamii za hisani na ili shughuli hizo ziweze kunufaisha vizuri zaidi zimeanzishwa taasisi kufanikisha shughuli za Mke wa Rais na taasisi hizo za hisani huchukua sura na mielekeo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hizo huendesha shughuli zake bila kutumia fedha kutoka kwenye Bajeti ya Serikali ama fedha yoyote ya Umma. Hazina uhusiano na fedha za Ikulu. Hizi ni taasisi zenye masharti makali yanayozuia matumizi ya fedha za umma. Taasisi hizi huchangiwa na taasisi za hiari na za kujitolea, Mashirika ya Kimataifa, sekta binafsi ambazo huingiza fedha zao katika kuunga mkono shughuli za taasisi hizo baada ya kuwa zimevutiwa na kuridhishwa na matokeo mazuri ya kazi za taasisi hizo. Taasisi hizi hukaguliwa kila mwaka na Wakaguzi wa Kujitegemea ili kutekeleza masharti muhimu ya uendeshaji na taarifa za ukaguzi hutolewa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya mtindo wa Mke wa Rais kusomewa ama kupatiwa taarifa za utendaji kazi katika Wilaya anapotembelea, ukweli ni kwamba Mke wa Rais hadai na hajapata kudai kupewa taarifa hizo. Lakini kama inatokea akapata taarifa hizo ni kwa sababu watendaji hutafuta fursa ya mchango wa Mke wa Rais katika maeneo yanayohusu maendeleo ya wananchi na changamoto zinazowakabili kama vile vifo vya akinamama wajawazito, athari za magonjwa kama Malaria na UKIMWI, mimba za utotoni ama za mashuleni na uwezesaji wanawake kiuchumi katika kupitia shughuli mbalimbali ukiwemo uanzishwaji wa SACCOS. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuunge mkono na nimpongeze sana Mheshimiwa Shibuda, ameyasema karibu yote. Mke wa Rais anafanya kazi nzuri na mke wa Rais aliyepita amefanya pia kazi vizuri na anastahili kupongezwa. Kwa kupitia Bunge lako na wanawake wa Tanzania, tunampongeza sana kwasababu ameamsha ari mpya ya wanawake kujali watoto wote kuwaona ni watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine limeulizwa na upinzani linahusiana na suala la Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Mfuko huu ni mfuko ambao ulianzishwa mwaka 1984 na ni mfuko ambao umekuwa haupokei ruzuku, ni *revolving fund*, unajitegemea na unafanya kazi nzuri na umeshafika maeneo mengi, lakini kwasababu *fund* yake ni ndogo, unakwenda pole pole. Ikumbukwe kwamba kuna mifuko mingi, na huu ni mfano wa mfuko mmojawapo ambao umeweza kujinunulia nyumba yake yenyewe na unaendesha kazi zake vizuri kabisa. Kwa hiyo, mfuko huu kama haujafika katika Wilaya yako, kuna wakati utafika. Mfuko huu umesaidia katika kuwakopesha hata wake wa maaskari, umesaidia katika kukopesha akina mama na kujenga nyumba za bei ya chini. Kwa hiyo, mfuko huo unafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo kujibu zile hoja zilizokuja kwa maandishi. Mheshimiwa Juma Killimbah – Mbunge wa Iramba Magharibi ameuliza swali, naomba mimi nimjibu moja kwa moja ili nisipoteze muda wa kulisoma hili swali. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge umepokelewa. Hata hivyo, Serikali kupitia vyombo vyake vinavyosimamia utawala bora vinaendelea kutoa mafunzo ya utawala bora kwa watumishi wote wa umma. Aidha, Kamati za maadili zilizoundwa katika sekta zote za umma zinasimamia kwa karibu masuala ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Khamis – Mbunge wa Jimbo la Mkoani, Suala lake lilihusu sana Wizara ya Sheria na Katiba. Hivyo basi, tutalichukua suala hili ili liende likajibiwe na Wizara husika huko. Nadhani utapata majibu mazuri zaidi, na Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame wa Mbozi ameulizia kuhusu masuala ya TAKUKURU na mimi ningependa kumjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU inazingatia taratibu za Sheria na Kanuni na siyo kukurupuka ili kutenda haki. Hivyo, zipo chunguzi mbalimbali ambazo zinachukua muda mrefu hadi kukamilika. Hivyo ni vyema kuwa na subira na siyo kwamba TAKUKURU inapuuza, inachukua muda mrefu kwa makusudi masuala yanayochunguzwa na TAKUKURU.

Waheshimiwa Wabunge, ni masuala ya makosa ya jinai na hivyo ni lazima kuwa na ushahidi wa kutosha ili kuyafikisha Mahakamani na masuala ya rushwa yanafanywa baina ya watu wawili na kwa usiri sana. Kwa hiyo, uchunguzi wake unachukua muda mrefu zaidi kuliko wa yule anayeiba kuku anaonekana wakati huo huo ameshika kuku.

Mheshimiwa Halima Mdee wa Kambi ya Upinzani anauliza tuhuma kuhusu wanasiasa kuhusu viwanja vya Dar es Salaam. Ningependa kumjibu kwamba hoja yako imepokelewa, lakini Mheshimiwa Halima Mdee ukiwa kama Mwanasheria, unaelewa kuwa masuala haya yatakapofika TAKUKURU ni lazima tutafute ushahidi mbalimbali.

TAKUKURU haitoi maamuzi ya kisheria. Kilichofanywa na Mkuu wa Mkoa, amechukua maamuzi ya kisheria na TAKUKURU itafanya kazi yake.

Nakushukuru kwa swali lako zuri, Mheshimiwa Bakari Faki, uliuliza tathimini ya rushwa nchini ikoje? Inazidi au inapungua? Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa hali ya rushwa inapungua kama inavyoonyeshwa katika kitabu cha hotoba jedwali Na.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanne ambaye ameuliza swali lake na hili swali ninadhani watu wengi wangependa kujua linahusiana na *TASAF*. Niwafahamishe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba *TASAF* imekaa na *World Bank* pamoja na Serikali pia kuzungumzia miradi ambayo haijamalizika. Ni kweli sababu mbalimbali zimesababisha miradi hii isikamilike ikiwemo ongezeko la bei za vifaa na pia uwezo mdogo wa wale waliokuwa wakisimamia. Benki ya Dunia imeshatoa fungu ambalo litasaidia kumaliza miradi hiyo, tayari ma-DED wamepelekewa taarifa ili waorodheshe ile miradi ambayo hajawa tayari ili ipate *allocation* katika hii *fund* ambayo itatoka katika hizi pesa ambazo zimetolewa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa muda wako ulionipa na ninaomba niseme ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa namuita Mheshimiwa Hawa Ghasia ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambaye pia ni mtoa hoja. Karibu sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya ambayo imeniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimetolewa. Naomba nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake aliyonionyesha kwangu kwa kuiteua kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kuendelea kuniamini kufanya kazi hii katika kipindi changu chote cha miaka mitano tangu nilipoingia madarakani. Nina imani kwamba katika kipindi chote cha uongozi wangu nimetekeleza majukumu ambayo amenikabidhi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushauri na maelekezo ambayo amenipatia katika kusimamia utumishi wa umma nchini. Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika hoja ambazo zimetolewa. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Sophia Simba kwa ushirikiano wake mkubwa wakati wote tuliifanya kazi pamoja na pia kwa kujibu hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kipindi chote. Naomba pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia bajeti yetu ya Ofisi ya Rais kwa kuzungumza nikianzia na Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutoa shukrani za dhati na za pekee kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na



Wajumbe wa Kamati hii kwa ushahuri na maelekezo ambayo wametupatia. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Bwana George Daniel Yambesi - Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Watendaji Wakuu pamoja na watumishi wote katika Utumishi wa Umma. Shukrani hizi zinatokana na ushirikiano wao mkubwa ambao wamenipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wananchi wenzangu wa Mtwara Vijijini kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na kutekeleza kikamilifu Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa muda wa miaka mitano. Napenda niwashukuru wazazi wangu, Mzee Abdulrahman Ghasia na Mama yangu Kashi Balozzi kwa malezi yao mema. Kwa namna ya pekee kabisa, napenda nimshukuru mume wangu Mr. Yahya Muhata kwa mapenzi yake makubwa kwangu na watoto wetu na uvumilivu mkubwa katika kipindi changu chote cha uongozi. Naomba aendelee kunipa ushirikiano na aendelee kunivumilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, napenda niwatambue Wabunge ambao wamechagua hotuba yetu nikianza na kwa kumtambua Mheshimiwa Ramadhani Maneno - Mbunge wa Chalinze ambaye amezungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge. Pia nimtambue na kumshukuru Mheshimiwa Grace Kiwelu ambaye amewakilisha Kambi ya Upinzani Bungeni kwa maoni yao na michango yao mizuri ambayo ninaamini kabisa itatusaidia katika kuboresha Utumishi wa Umma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue Wabunge waliochangia hotuba yetu ya bajeti ya mwaka 2010/2011 kwa kuongea na kuandika kama kama ifuatavyo:- Waliochangia kwa kuzungumza kwanza ni Mheshimiwa Halima Mdee - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Magdalena Sakaya - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwanne Mchemba - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Magale Shibuda - Mbunge wa Maswa na Mheshimiwa Sophia Simba - Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Utawala Bora).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwatambue waliochangia kwa maandishi Mheshimiwa Juma Killimbah - Mbunge wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Abbas Mtemvu - Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha - Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Juma Siraju Kaboyonga - Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Ali Khamis Seif - Mbunge wa Koani, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame - Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim - Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Omar Kwaang' - Mbunge wa Babati Mjini, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro - Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa Anna Abdallah - Viti Maalum, Mheshimiwa Godfrey Zambi - Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Mkiwa Adamu Kimwanga - Viti Maalum na Mheshimiwa Ameir ali Ameir - Mbunge wa Fuoni. (*Makofi*)

Wengineni Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi - Viti Maalum, Mheshimiwa Janeth Massaburi - Viti Maalum, Mheshimiwa Professor Philemon Sarungi - Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Viti Maalum, Mheshimiwa Shally Raymond - Viti Maalum, Mheshimiwa William Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa

Emanuel Luhahula - Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Professor Raphael Mwalyosi - Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Athumani Janguo – Mbunge wa Kisarawe na Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy – Viti Maalum. (*Makofi*)

Pia napenda kuwatambua Wabunge waliochangia Ofisi zetu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Wengine ni Mheshimiwa Willibrod Slaa - Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya - Viti Maalum, Mheshimiwa Said Nkumba - Mbunge wa Sikonge, Mheshimiwa Riziki Lulida - Viti Maalum na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim – Mbunge wa Mtambile. (*Makofi*)

Pia napenda kuwatambua waliochangia hotuba yetu kupitia hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwanza ni Mheshimiwa Mussa Azan Zungu - Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh – Viti Maalum, Mheshimiwa Professor Idris Ali Mtulia - Mbunge wa Rufiji, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya - Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhil - Viti Maalum na Mheshimiwa Said Arfi – Mbunge wa Mpanda Kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba yetu, napenda sasa nianze kujibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa kuanzia, naomba nianze kujibu hoja zile za ujumla. Kwanza, kuhusu tatizo la upungufu mkubwa wa Watumishi hususan katika Sekta ya Elimu, Afya na Kilimo. Kutokana na kupanuka kwa haraka kwa sekta za Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo kumekuwapo na tatizo la upungufu mkubwa wa wataalam katika soko la ajira. Upungufu huu umechangiwa na kuwepo kwa vyuo vichache visivyokuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya wataalam wa kissekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hili, Serikali imechukua hatua zifuatazo:- Kwanza, kupanua uwezo wa Taasisi za mafunzo zilizopo ili kukidhi mahitaji katika sekta za umma na sekta binafsi. Mheshimiwa Waziri wa Elimu ameelezea juhudi zinazochukuliwa katika kupanua vyuo vya mafunzo ambavyo vinatoa elimu na amekitaja Chuo Kikuu cha Dodoma. Sina haja ya kurudia hili. Lakini pia sekta ya Afya na yenyewe imepanua na kufufua vyuo ambavyo vilikuwa vimefungwa vya sekta hiyo ya Afya kutokana na kupanuka kwa uwezo wa Taasisi hizo, nafasi za Utumishi wa Umma wanaohitajika katika sekta hizo zimeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kutokana na kupanuka kwa Sekta za Elimu, pamoja na Kilimo, nafasi zinazotakiwa kujazwa na watumishi zimeongezeka na pia tumeweza kuongeza watumishi wa umma kama ifuatavyo:- Sekta ya Elimu kwa mwaka 2007 tumeweza kuongeza watumishi wapya 20,154; mwaka 2008/2009 tumeweza kuongeza watumishi 17,037; mwaka, 2009/2010 tumeweza kuongeza idadi ya watumishi 23,680 katika Sekta ya Afya; mwaka 2007/2008 tumeweza kuongeza Watumishi 4,187 na mwaka 2008/2009 watumishi 4,134.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010 tumeweza kuongeza Watumishi 6,810 na katika Sekta ya Kilimo na Mifugo mwaka 2007/2008 tumeweza kuongeza Watumishi 1,105; mwaka 2008/2009 tumeweza kuongeza watumishi 1,562 na mwaka 2009/2010 watumishi 1,678. Sekta ya Afya pia imeweza kufufua kozi za muda mfupi za miaka miwili ambazo zilikuwa zimefutwa hapo awali na kuweza kuzianzisha upya ambazo ni Wakunga wa Afya Vijijini, matabibu, wasaidizi Vijijini na Maafisa Afya Wasaidizi, vyote hivi vikiwa na lengo la kuongeza idadi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na tatizo ambalo limezungumzwa na wachangiaji wengi la kuchelewesha kuingiza watumishi kwenye *payroll*. Tatizo hili lilitokana na mawasiliano duni baina ya waajiri na waajiriwa wapya wenyewe kuchelewa ku-*report* katika Vituo vyao vya kazi, hivyo kupelekea kuchelewa kuingizwa katika *payroll* ili waweze kulipwa mishahara.

Pia kulitokana na matumizi hafifu ya teknohama katika kuandaa taarifa za malipo ya mishahara katika kukabiliana na tatizo hili. Mfumo wa kisasa wa teknolojia utaweza kukidhi taarifa za watumishi na mishahara, unahuishwa ambapo waajiri watawezesha wenyewe kuweza kuwaingiza watumishi bila kuhitaji kuleta taarifa zile kama ambavyo walikuwa wanaleta zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba ifikapo Novemba mwaka 2010 tatizo hili litakuwa limeondoka kabisa katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambazo zimetolewa katika hotuba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2010/2010, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza waliomba Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka iwezeshe kifedha na kiteknolojia. Pia watumishi katika eneo hili waendelezwe na tuone uwezekano wa Idara hii kuwa Mamlaka au Wakala inayojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kama ilivyo kwa Idara nyingine itaendelea kuwezesha kifedha, kiteknolojia kulingana na uwezo wa Serikali. Aidha, muundo wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma uko katika hatua za kuhuishwa. Moja ya shughuli zilizokwishafanyika ni pamoja na kutembelea Ofisi za Kanda za Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Mwanza, Mbeya, Dodoma na Arusha kwa lengo la kutathmini kazi zilizopo ili kubaini namna inavyoweza kufanyiwa kazi kama Idara inayojitegemea. Naomba pia kusahihisha kwamba Profesa Mwalyosi ni Mbunge wa Ludewa na siyo Makete, samahani Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ilipendekeza kwamba Serikali ipange upya mikakati maalum kwa ajili ya kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wa umma pamoja kujenga mikakati ya kudumu ya kuajiri Watumishi wa Umma. Serikali inazingatia umuhimu wa kuwaendeleza Watumishi wa Umma ili waweze kuendana na mabadiliko

yanayojitokeza na kufanya kazi zao kwa ufanisi. Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma inasisitiza kila mwajiri kutenga Bajeti ya kujenga uwezo kwa watumishi wake kila mwaka na pia kuwa na mpango wa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Waraka wa Utumishi No.4 wa mwaka 2005, unasisitiza Waajiri kuhakikisha kwamba Watumishi wanaojiriwa katika Utumishi wa Umma wanapatiwa mafunzo elekezi ili kuelewa wajibu wao katika Utumishi wa Umma. Kamati ya Katiba pia ilipendekeza kwamba majengo ya Utumishi wa Umma hususani mabweni yaongezwe sambamba na kuongeza uwezo wa udahili. Chuo cha Utumishi wa Umma kina mchango mkubwa sana katika kusimamia utendaji wa Watumishi wa Umma. Aidha, napenda nimhakikishie kwamba madarasa na mabweni katika matawi yetu matatu ya Tabora, Mtwara na Dar es Salaam yataendelea kuongezwa na kufanyiwa ukarabati. Pia tutaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Chuo cha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ilielekezwa kwamba iongeze umakini katika kusimamia utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za watumishi waajiriwa katika utumishi wa umma ili kupunguza kero za upotevu wa kumbukumbu muhimu. Suala hilo tunalichukua na tutalizingatia katika utendaji wetu wa kazi, lakini pia watumishi wa umma wanakumbushwa na wenyewe kutunza kumbukumbu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijibu hoja za Kambi ya Upinzani ambazo zimewasilishwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu Waziri kivuli wangu. Wakati anachangia hoja, Mheshimiwa Grace Kiwelu, alitaka kusikia kauli ya Serikali kuhusu Viongozi katika Taasisi za Umma wanaolipwa kinua mgongo na mshahara ya miezi sita kila baada ya miaka mitatu sambamba na waajiri kuendelea kuchangia mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 mwaka 1997 na Kanuni zake, Viongozi wa Wakala wanatakiwa kuajiriwa kwa mkataba wa vipindi maalum. Baada ya kumalizika kwa mikataba yao, viongozi hao hulipwa kiinua mgongo sawa na asilimia 25 ya mishahara waliyolipwa kwa kipindi chote cha mkataba. Aidha, wanaweza kuongezewa mikataba mingine baada ya kutimiza masharti ya ajira ya mikataba mipya itakayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatiwa kutolewa kwa waraka wa Katibu Mkuu - Utumishi kuhusu suala hili, Viongozi wa Wakala na baadhi ya Taasisi za Serikali wanatakiwa kuamua ama kuajiriwa kwa mkataba au kuajiriwa kwa masharti ya kudumu kama wanatosheleza sifa wanazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wanaoamua kuajiriwa katika masharti ya kudumu waajiri wao na wao wenyewe hawaruhusiwi kuchangia katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Hivyo, Serikali inapenda kutoa kauli kwamba Taasisi zinazoendelea kuchangia watumishi wa mkataba katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, wanafanya hivyo kinyume cha sheria na hatua zinapaswa kuchuliwa kusitisha utaratibu huo na kurejesha michango na mishahara iliyolipwa katika kipindi chote cha mikataba yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Kambi ya Upinzani ilizungumza ni kuhusu kuongeza kima cha chini cha mshahara kufikia Sh. 350,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kima cha chini cha mshahara kitaongezwa na kufikia Sh. 350,000/=, basi Serikali itahitaji shilingi trilioni 7.21 na wote tunafahamu kwamba bajeti yetu ya mwaka huu 2010/2011 mapato ya ndani ni shilingi trilioni sita. Kwa hiyo, ili tuweze kuwalipa watumishi wa umma, kima cha chini cha Sh. 350,000/= tutahitaji kuchukua mapato yetu yote ya ndani na ikiwezekana tukope na tuombe misaada ili tuweze kulipa kima hicho cha chini. Pia, tusimamishe huduma ambazo tunazitoa katika sekta ya afya, elimu na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashauri wenzangu Kambi ya Upinzani, pamoja na kwamba huu ni mwaka wa uchaguzi lakini ombi hili haliwezi kutekelezeka kama Rais ambavyo ametueleza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Grace na Mheshimiwa Mdee, hiki sio kitu cha kuombea kura mwaka huu. Sana sana tuwahimiza Watumishi wa Umma na sisi wenyewe tuwajibike ili tuweze kukuza uchumi na kuweza kulipa kima hicho ambacho kinapendekezwa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi na siwezi kuzijibu zote. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa watazipata kwa maandishi kabla ya Bunge hili kuahirishwa. Napenda kumalizia tena kwa kuwashukuru wananchi wa Mtwara Vijijini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na ushirikiano ambao wamenipa. Nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango ambayo wameitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunaendelea na hatua inayofuata.

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata Mwongozo wako. Bunge linatarajia kufanya maamuzi ya kupitisha Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jecha tupo katika Kamati hatupo katika Bunge naona unataka kuhoji jambo ambalo linahusu Bunge, labda kama una jambo ambalo linahusu Kamati.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kufanya maamuzi ya kupitisha maamuzi ya kupitisha Bajeti na huu ni utaratibu kupitisha bajeti ya Wizara inayohusika. Sasa kidogo nilitaka Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Nakuuliza tu ufafanue kwa sababu siyo nia yangu kuzuia, soma vizuri Kanuni zako, ujue unachokiongelea, ni cha Bunge au ni cha Kamati? Maamuzi yanafanywa na Bunge baadaye nitakapohoji ndipo tutakapokuwa tunafanya maamuzi. Saa hizi tupo katika kipindi cha Kamati ya Matumizi. Tuendeleee.

### **Fungu 20 - Ofisi ya Rais Ikulu**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... .. Sh. 8,810,623,000/=

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 30 – Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... .. Sh. 167,387,619,200/=

**MHE. JOHN. M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, kwa sababu sina uhakika kama mshahara wa Waziri ndiyo upo hapa, basi nitajielekeza kwenye hiyo *program* 10 kwenye *other operational expenses* ambazo nikihesabu kifungu 222900, nataka kutumia kifungu hiki. Wakati Kambi ya Upinzani inazungumzia juu ya Ofisi ya TAKUKURU, tumesisitiza kwamba pawepo na fedha za kutosha zaidi kwa mwaka huu wa uchaguzi, lakini nimeangalia katika mafungu yote haya ambayo yanahusu Wizara hii, huwezi ukaona ni wapi kuna kifungu kinachoshughulikia mambo ya TAKUKURU na tumeweka hata kifungu cha *TACAIDS* kushughulikia UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa jambo muhimu kama hili, kwa nini lisiwe na kifungu chake kinachojulikana? Hata leo tumeambiwa kwamba TAKUKURU imefanya kazi nzuri katika kuokoa fedha nyingi ambazo zimetajwa kama shilingi bilioni tisa, basi ingekuwa ni vizuri tukaangalia kwa mwaka huu kwamba hela inayokwenda kule inalingana pia na fedha ambayo inaokolewa. Kama Waziri hana Kifungu: Je, isingekuwa vizuri labda kwa miaka inayokuja pakawa wazi na kuwe na kifungu ambacho kinashughulikia tu kazi hii ili Bunge liongelele linatumia fedha ngapi kwa ajili ya shughuli hii muhimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Cheyo, ni mzuri, tutaufanyia kazi. Lakini kwa sasa kiwango ambacho wamepangiwa tunaamini tutajibana na kazi nzuri itafanywa ya kuhakikisha masuala ya rushwa katika uchaguzi yanashughulikiwa kikamilifu. Moja ya kazi tulizozifanya ni hivi vitabu ambavyo tumetayarisha.

Tumeshindwa kufanya semina kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, tumeona tusambaze vitabu ili muweze kuvisoma. Ushauri wako ni mzuri, tunashukuru.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance and Account* ... .. Sh. 386,331,000/=  
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... .. Sh. 402,415,600/=  
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* ... .. Sh. 256,762,300/=  
Kif. 1005 - *Management Inf. System Unit* ... .. Sh. 220,786,900/=  
Kif. 2001 - *Cabinet Secretariat* ... .. Sh.1,154,434,600/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - *Government Communication* ... .. Sh. 340,269,800/=

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia nipate kitu *specific* hapa, lakini kwa sababu naona kwenye *basic salary* kumewekwa *zero*, nilikuwa naomba nilizungumzie kwa ujumla wake.

**MWENYEKITI:** Uko kifungu kipi?

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natafuta kifungu *specific* katika hivi vidogo vidogo hapa, lakini sikipati moja kwa moja. Kwa hiyo, kwa sababu inahusu Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu, nilikuwa naomba nilielekeze moja kwa moja katika fungu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kurugenzi hii na hasa Mkurugenzi wake imewekwa pale kwa ajili ya kumsaidia Rais na Ikulu kwa ujumla katika kutoa taarifa kwa umma. Lakini katika kipindi kirefu sasa kumekuwa na *controversies* nyingi katika taarifa ambazo zinatoka hapa. Mifano michache tu wakati fulani kulikuwa na malumbano makubwa kuhusiana na muafaka. Mkurugenzi huyu aliwahi kuiathiri kwa kukanusha kuwepo kwa barua iliyopo Ofisi ya Rais na baadaye ikathibitishwa kwa *dispatch* ambayo ilipelekea *embarrassment* kubwa lakini lilikuwepo suala la Sheikh Yahya na utabiri wake akatoa kauli kuupongeza ambayo ilileta pia mtafaruku mkubwa katika Vyombo vya Habari na hata karibuni kulikuwa na malumbano baina yake na Waziri wa.....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jussa katika hatua hii tupo *very specific*. Kwa hiyo, unakwenda moja kwa moja kwenye fungu na swali lako linakuwa linajielekeza moja kwa moja katika jambo ambalo linahusiana na matumizi yaliyopangwa hapa. Kwa hiyo, nakupa nafasi tena uendeleo kama kuna jambo katika ukurasa huu na kifungu hicho *sub vote* 2002.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie kifungu cha 221200 *Communication and Information*. Kutokana na maelezo hayo niliyokuwa nimeyatoa inaonekana kuna *controversies* nyingi. Nilikuwa naomba tupate maelezo kwamba hivi Ofisi hii kweli inamsaidia Rais au imekuwa ni mzigo tu kwa Ikulu kiasi cha kuhalalisha matumizi yote haya makubwa?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba nimjibu kwamba, kauliza swali moja tu kwamba kitengo hiki kinamsaidia Rais, na mimi ninamjibu kwamba kitengo hiki kinamsaidia Rais vizuri sana. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - *Good Governance*... .. Sh. 453,760,900/=  
Kif. 2004 - *Public Service Appeal*... .. Sh. 367,320,600/=  
Kif. 2005 - *Public sector Reform*  
*Coordination Unit* ... .. Sh. 395,946,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.**

Kif. 1001 - *Adm and HR MGT*  
*Division* ... .. Shs 10,408,420,277/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hiyo hiyo *program 10, sub-vote 1001* mshahara wa Waziri.

Katika mchango wangu wa maandishi niliuliza kama pensheni ya watumishi wa umma itapandishwa. Lakini pia nilisema kwamba mwaka 2008/2009 Bunge hili lilipandisha kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu karibu shilingi 21,000 mpaka kwenye shilingi 51,000. Lakini nikasema kwa sababu pia mshahara unaelekea kupanda, je, isingekuwa busara tena pensheni kwa watumishi wa umma pia ikapanda kutoka kiwango hicho ambacho kwa kweli kidogo walau kiende juu hata kama ni kwa asilimia 50. Sikupata majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sikutoa ufafanuzi kwa sababu muda ulikuwa hautoshi. Lakini nimwambie ni kweli tunafahamu kwamba kima cha chini cha pensheni ni kidogo na utaratibu wa kuongeza hauendani na ongezeko la mishahara. Lakini bado tunalichukulia na tutaendelea kulifanyia kazi.



**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba majibu yetu atatuletea. Lakini kwenye hiki kitabu kwenye *program 10, sub-vote 1001, item ya 220100* ambayo inasema *office and general supplier and services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliotangulia ilikuwa ni shilingi milioni 41 lakini mwaka huu ime-*shoot* na wakati huo huo kwenye *item 227500 other suppliers and services* ambayo ina shilingi bilioni 7. Kwa hiyo, mimi nilitaka kujua kwa nini ime-*shoot* hadi hapo hii ya kwanza na hii ya pili ambayo *other suppliers and services* ina tofauti yake ya ni nini? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si kwamba imepanda sana. Lakini ukiangalia mwaka 2008/2009 ilikuwa shilingi milioni 110 na mwaka 2010 ni shilingi milioni 123. Huu mwaka 2009/2010 ni kutokana na makosa, sisi *system* imeshindwa kuvuta zile takwimu zote na kuziweka hapa lakini kiwango kilichopo hakina tofauti sana isipokuwa hii takwimu iliyotokea hapa tu ina matatizo.

**MWENYEKITI:** Bado liko la pili la kuhusu *item 227500* ambayo mwaka jana na mwaka juzi ilikuwa 0 sasa ina bilioni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki kinawahudumia wastaafu. Lakini pia kimewekwa hapo kwa makosa kimetoka pale *item 260500* ukiangalia pale iko 0. Kwa hiyo, *figure* za pale chini ndio zimekuja hapa.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize hapo hapo *sub-vote 1001*, kifungu kidogo cha 2100 cha mishahara wa Waziri. Katika hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa aliahidi kwamba Serikali imekubali kuongeza kiwango cha mishahara na kwamba ingetangazwa na Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anawasilisha Bajeti hii. Lakini hotuba nzima hatukusikia. Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jussa unajua jimbo lako ndiyo hili sasa mbona unauliza uliza sana maswali kuhusu jimbo? (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati nasoma hotuba yangu nimesema kwamba Serikali imekubali kuongeza kima cha chini sawa na makubaliano yetu na Vyama vya Wafanyakazi. Kwa kufanya hivyo Bajeti ya mishahara mwaka huu imeongezeka kwa shilingi bilioni 558 ukilinganisha na ya mwaka jana. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and accounts Unit* ... .. Sh. 207,727,820/=  
 Kifungu 1003 - *Information, Education and Communication*... .. Sh. 83,824,400/=  
 Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*... Sh. 97,654,000/=  
 Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit* ... .. Sh. 76,721,000/=  
 Kifungu 1006 - *Planning Division* ... .. Sh. 277,439,648/=Kifungu 2001 – *Policy development*  
 Kifungu 2002 – *Management Services Division* ... Sh. 299,948,400/=  
 Kifungu 2003 – *Establishment Division*... .. Sh. 773,528,150/=Kifungu 2004 – *Ethic Promotion D*  
*Development Division*... .. Sh. 2,579,547,584/=  
 Kifungu 3002 – *Tanzania Public Service College* ... .. Sh. 0/=  
 Kifungu 3004 – *Diversity Management Unit* ... .. Sh. 97,695,522/=  
 Kifungu 4002 – *Management Information System Division*... .. Sh. 282,457,000/=  
 Kifungu 4003 – *Records and Archives Division* ... Sh. 698,668,623/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

### **Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... .. Sh. 1,257,916,270/=  
 Kifungu 1003 – *Finance and Accounts* ... .. Sh. 707,485,930/=  
 Kifungu 1004 – *Information, Education and Communication* ... .. Sh. 105,330,800/=  
 Kifungu 1005 – *Procurement and Management Unit*... .. Sh. 86,493,000/=  
 Kifungu 1006 – *Internal Audit* ... .. Sh. 49,208,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

### **Fungu 66 - Tume ya Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management Division* ... .. Sh. 1,212,081,000/=  
 Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* ... .. Sh. 275,551,100/=  
 Kifungu 1003 – *Planning and Monitoring Division* ... .. Sh. 368,692,000/=  
 Kifungu 1004 - *Information, Education and Communication Unit* ... .. Sh. 174,095,000/=

Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit* ... .. Sh. 131,948,000/=  
 Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*...Sh. 266,299,000/=  
 Kifungu 1007 – *Library and Documentation*... ..Sh. 124,876,000/=  
 Kifungu 1008 - *Management Information System*... ..Sh. 115,064,000/=  
 Kifungu 2001 – *Macro Economic Cluster* ..... Sh. 604,187,000/=  
 Kifungu 2002 – *Productive Sector Cluster* ... .. Sh. 630,892,000/=Kifungu 2003 - *Infrastructure and Service Cluster* ... ..Sh. 676,392,000/=  
 Kifungu 2004 – *Social Service and Demographic Cluster*... ..Sh. 633,548,000/=  
 Kifungu 2005 – *International Trade and Eco. Relation C* ... ..Sh. 546,202,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

### **Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management Division* ... .. Sh. 2,210,029,560/=  
 Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*... ..Sh. 51,825,600/=Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*... ..Sh. 15,719,880/=  
 Kifungu 1004 – *Education, Information and Communication* ... ..Sh. 11,850,360/=  
 Kifungu 1005 – *Legal Service* ... .. Sh. 16,817,160/=Kifungu 1006 – *Procurement Management*  
 Kifungu 1007 – *Management Information Systems*... ..Sh. 51,319,440/=  
 Kifungu 1008 – *Internal Audit* ... .. Sh. 31,074,040/=  
 Kifungu 2001 – *Recruitment Management Division* ... ..Sh. 576,491,040/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 2002 – *Quality Control* ... .. Sh. 24,273,120/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vifungu vingi kuanzia 1005, 1006, 1007, 1008 mpaka hicho 2002 lakini nimeona nielimishwa kwa sababu vifungu hivyo vimewekewa mishahara tu yaani kazi zake hazijaonyeshwa kama ilivyo ada kwenye vifungu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kile kifungu 2001 ambacho kuna *basic salaries, office and general suppliers and services traveling* na vifungu vya aina hiyo. Lakini fungu hilo na fungu vile pale juu vina fungu moja moja tu kwa maana ya

mishahara tu. Sasa nilitaka kujua hizi shughuli nyingine zinafanywa kwenye vitengo vipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zote zitafanywa na Idara ya Utawala isipokuwa mishahara tu ndiyo italipwa kwenye vifungu vyao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and HR Management*

*Division* ..... Sh. 2,618,899/=

Kifungu 2001 – *Civil Service* ... Sh. 239,941,500/=

Kifungu 2002 – *Local Government Service* ..... Sh. 331,512,980/=

Kifungu 2003 – *Teachers' Service* ... Sh. 4,405,277,750/=

Kifungu 2004 – *Fire and Immigration Service*... Sh. 182,410,400/=

Kifungu 2005 - *Health Service* ... Sh. 192,823,120/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning* ... Sh. 67,292,079,000/=

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumsaidia Mkuu wa Jimbo langu ili apate kufanya kazi vizuri. *Sub vote 1003* kifungu cha 6203 *Support to Prevention of Corruption Bureau*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani liliuliziwa *specifically* suala la rada na Mheshimiwa Waziri ametujibu majibu ya jumla jumla. Lakini katika hili la rada kwa sababu mmesema uchunguzi unaendelea, lakini katika hili *Head Office* Uingereza tayari imekamilisha uchunguzi huu na tulikuwa tukiambiwa kwamba ilikuwa inashirikiana na taasisi hii kwa upande wa Tanzania na pia mhusika mmoja ambaye alitajwa kwa mfano bwana Sailes Bithilanya ambaye ameambiwa alichukua *payment* ya bilioni 12 katika zile, tunaomba maelezo zaidi kuhusu kesi ilipofikia katika kifungu hiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jussa naomba utoe *clarification* kidogo unaulizia kuhusu suala la kesi inayoendelea mahakamani? Si unajua kanuni zetu? Hebu fafanua kidogo kabla sijapeleka upande wa pili.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kesi haiko mahakamani. Lakini ni suala ambalo limekuwa katika uchunguzi na muda mrefu, madai

ya Kambi ya Upinzani ni kwamba suala hili sasa lifikishwe mahakamani lieleweke. Suala la rada bado halijafikishwa mahakamani.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Ikulu kwamba wakati ukifika tutafika mahakamani kwa kishindo. Lakini hatuwezi kwenda mahakamani kwa sababu bado kuna taarifa ambazo tunazitafuta hasa baada ya wenzetu wa Uingereza kufanya mapatano na wale ambao pia ni watuhumiwa. Tunakuomba uwe na subira.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 -Administration and HR Management

Division ... .. Sh. 4,997,890,650/=

Kifungu 1002 – Finance and Accounts Unit ... .. Sh. 30,000,000/=Kifungu 1003 – Information, Education

Communication..... Sh. 717,840,000/=

Kifungu 1004 – Procurement Management ... .. Sh. 30,000,000/=

Kifungu 1005 – Internal Audit Unit ... .. Sh. 0/=

Kifungu 1006 – Planning Division ... .. Sh. 1,849,980,000/=

Kifungu 2001 – Policy Development Division... .. Sh. 895,550,500/=

Kifungu 2002 – Management Services Division...Sh. 1,359,042,200/=

Kifungu 2003 – Establishment Division ... .. Sh. 847,044,200/=

Kifungu 2004 – Ethic Promotion Division ... .. Sh. 523,748,000/=

Kifungu 3001 – Human Resources Development

Division... ..Sh. 5,272,100,500/=

Kifungu 3002 – Tanzania Public Service College ... .. Sh. 0/=

Kifungu 3004 – Diversity Management Unit ... .. Sh. 744,594,750/=Kifungu 4002 – Management Information

System Division.....Sh. 2,228,809,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4003 – Records and Archives Division... Sh. 3,075,000,000/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa ili niweze kuhoji kwa vifungu ambavyo viko nyuma lakini nafikiri nitumie tu kifungu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vifungu vingi vina fedha ambazo ni za nje tofauti fedha za ndani shilingi bilioni 5.3, fedha za nje shilingi bilioni 17.2. Tunajua kabisa ofisi hii iko kwenye kazi kubwa kwa ajili ya mabadiliko yanayoendelea Serikalini. Sasa wasiwasi wangu tukitumaini fedha nyingi kiasi hicho kutoka nje zisipokuja ina maana kazi Serikali itasimama, mabadiliko yanayoendelea Serikali. Waziri anatuhakikishia namna gani kwamba fedha zitakuja? Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hata akiangalia naona ni kwamba *Public Service Reform* ni katika maboresha ya utumishi wa umma na tayari Benki ya Dunia ndio inayogharamia mpango huu kupitia *Basket Fund* na fedha zake zipo kwa kipindi chote cha miaka mitano.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and General* .... Sh. 1,190,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango**

Kifungu 1001- *Administration and Management Division*... Sh. 0/=  
Kifungu 1003 - *Planning and Monitoring* ... .. Sh. 0/=  
Kifungu 1004 - *Information, Education & Communication Unit* ... .. Sh. 0/=  
Kifungu 2001- *Macro Economy Cluster* ... .. Sh. 0/=  
Kifungu 2002 - *Productive Sector Cluster* ... .. Sh. 0/=  
Kifungu 2004 - *Social Service and Demographics Cluster* ... .. Sh. 177,000,000 /=  
Kifungu 3001 - *Social Service and HR Development* ... .. Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 67- Ofisi ya Rais- Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management Division*... .. Sh. 1,000,000,000/=

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001- *Administration and General*... .. Sh. 93,075,000/=

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge Lilirudia)*

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Miongozo miwili, ataanza Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha halafu baadae Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakaribia kupitisha maamuzi ya matumizi ya Wizara hii ambayo ipo mbele yetu tunayojadili leo. Lakini nikiangalia katika ukumbi wako ni kwamba Bunge lako halijatimiza akidi kwa mujibu wa Kanuni ya 77(2), na ni kwa nia njema kabisa kwamba kama tutapitisha maamuzi haya chini ya akidi ya Bunge itakuwa tumezivunja Kanuni za Bunge, lakini kadhalika tutakuwa tumefanya maamuzi ambayo sio halali. Naomba mwongozo wako ili tumsaidie Mheshimiwa Waziri.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama kuomba mwongozo wako kwa Kanuni hiyo hiyo ya 77(1) na (2) nikitoa hoja kwamba niombe kwa sababu ya idadi tuliyonayo hapa ndani kwamba idadi yetu ni ndogo, najua kwamba kuna Kamati zinazoendelea ili kama tuweze kupata mwongozo wako kama hawa waitwe ili tuweze kufikia idadi ili tuweze kupitisha hoja hii au uihirishie hoja hii hadi hapo idadi itakapopatikana kwa kikao kingine. Nilitaka kuomba mwongozo wako au pengine ikilazimu unaweza kuelekeza tuhesabiwe au wengine waitwe kengele ipigwe.

**MWENYEKITI:** Sasa mwongozo wangu ni ufuatao, namuonba Katibu agonge kengele ili baadhi ya Wabunge ambao wapo nje ya ukumbi huu waweze kujiunga nasi na tutasubiri kwa dakika tano wakati kengele ikiendelea kugonga, baada ya hapo nitatoa mwongozo wa namna ya kuendelea.

*(Hapa kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge waliopo nje ya ukumbi waingie ndani ya ukumbi wa Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, zile dakika nilizotoa zinatoshia, sasa kufuatana na Kanuni ya 68(4) kuhusiana na mambo haya ya utaratibu, Spika anaweza ama papo hapo kutoa uamuzi wake juu ya jambo la utaratibu lililotajwa au kuahirisha uamuzi ili alifikirie zaidi jambo hilo na kutoa uamuzi na baadae kutoa sababu za uamuzi huo vyovyote atakavyoamua. Mimi sasa natumia Kanuni hiyo kuamua kwamba tunaendelea na shughuli, uamuzi nitautoa baadae. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu limepitia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu, Fungu 20 na Fungu 30, Menejimenti ya Utumishi

wa Umma Fungu 32, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Fungu 33, Tume ya Mipango Fungu 66, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Fungu 67 na Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94 kifungu kwa kifungu bila marekebisho yoyote. Sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Sasa natoa uamuzi wangu kama nilivyotakiwa pale mwanzo, wewe mtoto wewe. Hiyo nanukuu maneno ya Mheshimiwa Mbunge jana aliyesema kwamba mtoto acha kupiga mayowe. Ahsante sana.

Sasa uamuzi nautoa kufuatana na Kanuni ya 72(1), “Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatana Bungeni na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho.” Mwisho wa kunukuu Kanuni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kutangaza kwamba makadirio yanayohusiana na Wizara hii ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yamepitishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Matangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kwa kazi nzuri mnayofanya hapa Bungeni ile Mifuko ya *CDCF* awamu ya pili imeshaingiziwa fedha zake zote kwenye akaunti ya kila Halmashauri. Nimepewa taarifa hapa kwamba *CRDB* wamefungua leo wapo, kwa hiyo Waheshimiwa mkitoka hapa sio mbaya kupitia maeneo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na *Order Paper* ya leo na shughuli zilizopangwa, zote zimekamiliwa na mimi nawapongeza sana kwa ushiriki wenu makini. Katika shughuli ambazo zimepangwa tumemaliza vizuri kwa amani na kwa hiyo sasa naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho kutwa Jumatatu, tarehe 21 Juni, 2010 saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.33 mchana Bunge lilihairishwa mpaka siku ya Jumatatu,  
Tarehe 21 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*



